**3 FEBRUARI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

**MKUTANO WA KUMI**

**Kikao cha Nne – Tarehe 3 Februari, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022.

**MHE. IDD K. IDD K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mpina.

Na. 48

**Tatizo la ajira nchini**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Je, ni vijana wangapi hawana ajira nchini na Serikali imewaandaaje kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi?

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri. Hamna majibu? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuna

marekebisho ambayo ningeomba radhi kwa Bunge lako tukufu ili tuweze kupata *version* ambayo ni sahihi zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Unaomba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Ninaomba kuna marekebisho kwenye swali hilo…

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo mtajibu baadae?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya dakika chache tu.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis.

Na. 49

**Elimu juu ya dawa za kulevya kwa vijana**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa vijana walio mashuleni juu ya kujikinga na dawa za kulevya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)**alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa na kuzindua Mwongozo wa Utoaji Elimu Kuhusu Dawa za Kulevya nchini ambao ulizinduliwa tarehe 2 Julai, 2022 na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye kilele cha siku ya Taifa ya Kupinga Dawa za Kulevya, Jijini Dar es Salaam. Mwongozo huo tayari umeanza kutumika kuelimishia walimu wa shule za msingi na sekondari pamoja na asasi za kiraia zinazojihusisha na utoaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ya jamii wakiwemo vijana waliopo mashuleni, juu ya tatizo la dawa za kulevya nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shomar.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa vitendo vya kikatili vya kupiga wanafunzi vimekuwa vingi katika shule. Je, Wizara ya Elimu italiambia nini Bunge hili, usalama wa wanafunzi wanapokuwa shuleni?

(b) Kwa kuwa, walimu wanaofanya vitendo hivyo, wanaangaliwa wanapokuwa wanakwenda shuleni kwamba hawana viashiria vya ulevi hata

wakafanya vitendo vya kikatili vya namna hiyo?*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwenye suala la Walimu na matendo yanayokithiri ya kupiga wanafunzi tayari Wizara ya Elimu imekwisha kuanza kuchukua hatua mahsusi za kufanya ufatiliaji kwenye maeneo yote ambayo tumekuwa tukipata taarifa kwamba wanafunzi wanatendewa visivyo, kinyume na utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo katika hatua nyingine kupitia Wizara yetu Ofisi ya Waziri Mkuu, tunaweza tukashirikiana vizuri na Wizara ya Elimu ili kuweza kubaini kama matendo hayo ya wale watuhumiwa ambao wanaonekana wametenda matendo ya ukatili kwa watoto, kama itaonekana kwamba wana viashiria vya ulevi basi tutachukua hatua kuweza kuhakikisha kwamba masuala haya hayajitokezi tena katika nchi yetu na kuchukua hatua zinazostahili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais Mheshimiwa Tendega.

Na. 50

**Kugawa upya Halmashauri nchini**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itazigawa upya Halmashauri nchini ili Wananchi wapate huduma kwa urahisi kutokana na jiografia za Halmashauri hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu na mwenye swali Namba 52 ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikigawa maeneo mapya ua Utawala zikiwemo Halmashauri kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya huduma na kiutawala katika mamlaka mpya ambazo hazina miundombinu hiyo muhimu ili kuziwezesha kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa jumla ya majengo ya utawala 109 yenye thamani ya shilingi bilioni 356.8 yanaendelea kujengwa kote nchini,

lengo la Serikali kwa sasa ni kukamilisha miundombinu katika mamlaka zilizopo kabla ya kuanzisha mamlaka mpya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kujibu maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Halmashauri zimekuwa kubwa mno na nyingine zimekuwa zina maeneo makubwa sana kijiografia, lakini nyingine zina Majimbo matatu, nyingine zina Majimbo mawili na kupata huduma wanapata katikati ambako ni Mjini.

(i) Je, serikali sasa haioni haja ya kufuata uhalisia na urahisi wa kupata huduma katika ugawaji wa Halmashauri hizo?

(ii) Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba katika utengaji wa fedha za maendeleo jiografia za Halmashauri zetu iwe ni mojawapo ya kigezo cha kuzingatiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali wawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tuna Halmashauri ambazo zina maeneo makubwa kijiografia, lakini kuna Halmashauri ambazo zina Majimbo zaidi ya moja na ni kweli kuna changamoto ya umbali kutoka baadhi ya maeneo ya Halmashauri kufika kwenye Makao Makuu ya Halmashauri hizo. Serikali kwa sasa sote ni mashahidi kwamba mamlaka nyingi zimeanzishwa hazina majengo muhimu ya utawala, hazina miundombinu muhimu ya huduma za jamii. Kwa hiyo, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kukamilisha kweye mamlaka zilizopo na baada ya hapo taratibu zitafuatwa ili kupata mamlaka nyingine na kusogeza huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; Serikali imekuwa ikipeleka fedha kwa kuzingatia jiografia kwa maana ukubwa wa maeneo, ndiyo maana hata kwenye Mfuko wa Jimbo, kigezo mojawapo ni ukubwa wa eneo la Halmashauri husika lakini hata kwenye fedha za barabra kwa maana ya *TARURA* kigezo mojawapo ni hicho. Kwa hiyo, Serikali inazingatia pia ukubwa wa kijiografia wa maeneo husika. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali namba 52 na swali namba 51 kaa *standby.* Mheshimiwa Waitara.

Na. 52

**Kata za Sirari na Nyamongo Kupandishwa Hadhi**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, ni lini Kata za Sirari na Nyamongo zitapandishwa hadhi na kuwa Mamlaka za Miji Midogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kufikia mwezi Januari, 2023, nchi yetu ina jumla ya Halmashauri za Miji 21 na Mamlaka za Miji Midogo 71.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mwongozo wa uanzishaji wa mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2014, utaratibu wa kuomba kuanzisha Mamlaka za Miji Midogo huanza na mikutano ya kujadili. Mikutano hiyo hufanywa katika ngazi ya vijiji, kisha Kamati ya ushauri ya Wilaya *(DCC)*, Kamati ya ushauri ya Mkoa *(RCC)* na kuwasilishwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusudio la kuanzisha Mamlaka za Miji Midogo katika Kata za Sirari na Nyamongo mchakato wake uliishia kwenye Kamati ya Ushauri ya Wilaya kwa kikao kilichofanyika mwaka wa fedha 2011/2012. Hivyo, Halmashauri inashauriwa kutimiza matakwa ya mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mpango wa Serikali kwa sasa ni kukamilisha kwanza miundombinu kwa mamlaka zilizopo kabla ya kuanzisha mamlaka mpya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maeneo yote hayo mawili ya Sirari na Nyamongo ni ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali, sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri kama yupo tayari majibu haya haya tuyapeleke pale Sirari na Nyamongo akayaseme mwenyewe? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba arudie sijamsikia vizuri swali lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, rudia swali lako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nimesema kwamba pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwa kuwa maeneo haya ya kuwa Mamlaka ya Miji, Sirari na Nyamongo ni ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali. Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimwa Mizengo Pinda mwaka 2011 na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mwaka 2020.

Je, Waziri yupo tayari tuongozane kwenda Sirari na Nyamongo na majibu haya akayatoe kwa wananchi yeye mwenyewe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo tayari tuongozane na Mheshimiwa Mbunge na bahati nzuri wiki mbili zilizopita tulikuwa Tarime Vijijini tumefanya ziara pamoja na niko tayari turejee tena Tarime kwenda Sirari na Nyamongo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri yupo tayari yamekwisha, mengine basi baadae. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Katika Miji Midogo iliyoko nchini sasa hivi kumekuwa kuna sintofahamu kati ya Mamlaka ya Miji Midogo na Halmashauri kuhusu nani hasa akusanye mapato yapi? Je, Serikali sasa iko tayari kutoa mwongozo unaoeleweka ili mamlaka zote mbili zijue mipaka yake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi tuna mamlaka za Miji Midogo 71 kote nchini…

**NAIBU SPIKA:** Serikali ijiandae swali namba 48 sasa hivi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi miji hii midogo inawajibika katika Halmashauri Mama na inatekeleza majukumu yake chini ya usimamizi wa Halmashauri Mama. Kwa hiyo, haina mamlaka ya moja kwa moja mpaka pale itakapopata sifa ya kuwa Halmashauri ya Mji. Kwa hiyo, ikiwa Mamlaka ya Mji mdogo bado haina mamlaka ya moja kwa moja na wao siyo *Accounting Officers,* kwa hiyo tutaendelea kuhakikisha kwamba kwanza tunawawezesha kwa kuwajengea uwezo lakini ku-*harmonize* mahusiano kati ya Halmashauri Mama lakini na Mamlaka za Mji Mdogo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka Serikali ilikuwa haijajiandaa na swali namba 48 sasa wako tayari. Mheshimiwa Waziri swali limeshaulizwa.

Mheshimiwa Waziri.

Na. 48

## 3 FEBRUARI, 2023

## Tatizo la Ajira Nchini

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza: -

Je, ni Vijana wangapi hawana ajira nchini na Serikali imewaandaaje kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2021 unaonesha kuwa vijana wenye umri wa miaka 15-35 ambao wana ukosefu wa ajira ni 1,732,509. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 12.2 ya nguvu kazi, maana ya vijana walio katika umri huo na wapo katika mfunzo au hawana ulemavu unaosababisha wasijishughulishe na shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kuhakikisha kwamba Vijana wanaendelezwa ipasavyo kushindana katika soko la ajira la ndani na nje ya nchi, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeweka mkakati wa kitaifa wa kukuza ujuzi wa miaka 10 mwaka 2016/2017 – mwaka 2025/2026. Kupitia

mkakati huu, Serikali imefanya maboresho ya miundombinu ya mitaala katika ngazi za Elimu ya Juu, Elimu ya Kati, na Mafunzo Stadi ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, sambamba na maboresho hayo, Serikali imetoa mafunzo ya kuwezesha vijana walio nje ya mafunzo rasmi ili kumudu ushindani katika soko la ajira, yakiwemo mafunzo ya uanagenzi, mafunzo ya uzoefu wa kazi *(internship)* kwa wahitimu, mafunzo ya urasimishaji ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu *(RPL)*, na mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya vitalu nyumba. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Moja; Serikali ina makakati gani wa dharura wa kudhibiti biashara holela, uingiaji wa mikataba mibovu na usimamizi hafifu wa sheria ambazo kasoro hizo zinasababisha ajira nyingi za Watanzania kupotea?

Mbili; kwa nini Serikali isiachane na utaratibu wa sasa hivi wa baadhi ya ajira kupatikana kwa njia ya uteuzi na badala yake ajira zote zikapatikana kwa njia ya ushindani, ajira za Viongozi na ajira za Watendaji, Mawaziri, Wakurugenzi na Makatibu Wakuu na Watendaji wengine wote wa Serikali ili kuiwezesha Serikali kupata Viongozi wenye uwezo usiotiliwa mashaka katika nafasi mbalimbali za Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ameeleza ni mkakati gani ambao Serikali imeendelea kuchukua kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hakuna mikataba mobovu pia utumiaji mzuri wa fedha ambazo zinaenda kwenye maeneo ya uwekezaji ili kuweza kulinda ajira za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayofuraha kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali kupitia vyombo vyake muhimu imekwisha kuanza kuchukua hatua na mtakumbuka Mheshimiwa Rais katika nyakati zote amekuwa akichukua hatua katika kuimarisha vyombo vyetu vinavyosimamia sheria, ikiwemo Mahakama lakini pia Polisi, TAKUKURU kwa maana ya *PCCB (Prevention and Combating Corruption Bureau)* ambayo inapambana na maswala ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine Serikali imeendelea kuweza kuchukua hatua kwa wale ambao wamekuwa wakiingiza katika mikataba mobovu, hatua mbalimbali zimekwisha kuchukuliwa na Serikali tayari ina Mahakama maalum kuchukua hatua kwenye masuala ya rushwa. Kwa mfano, tunayo Mahakama ambayo inasimamia masuala ya

makosa ya kiuchumi, ambayo hii mojawapo ni kudhibiti haya ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake pili ameeleza kwamba ajira kwa nini zisipatikane kwa njia ya ushindani badala ya uteuzi jinsi ilivyo. Kwa sasa, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaeleza namna na mfumo wa uendeshaji wa Serikali na inatambua uwepo wa ajira ambazo zinapatikana kwa utaratibu ambao Mheshimiwa Mbunge ameusema wa ushindani lakini pia zipo ajira zinazopatikana kwa njia ya uteuzi kulingana na *provisions* zilizopo katika Katiba, zipo pia ajira ambazo zinapatikana kwa utaratibu wa kuomba ama kuzipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo katika kupanua wigo wa ajira, Serikali imekwisha kuchukua mikakati ya kuhakikisha tunatafuta ajira ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, umejibu vizuri sana. Ahsante sana inatosha.

Waheshimiwa tunaendelea swali namba 51, Mheshimiwa Genzabuke.

Na. 51

**Vibali kuajiri walimu nchini**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatoa vibali ili kuajiri walimu na kuondoa upungufu wa walimu uliopo nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutatua na kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu nchini kwa kutoa vibali vya ajira za walimu ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliajiri walimu 14,949 na mwaka wa fedha 2021/2022 iliajiri walimu 9,800.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na mpango wa kuajiri watumishi wakiwemo walimu ili kukabiliana na upungufu kulingana na mahitaji na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante mwanzoni nilisema Spika, nafanya marekebisho. Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa walimu wa hisabati, na wanafunzi wamekuwa wakishindwa kufanya vizuri kutokana na ukosefu wa walimu wa hisabati. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha shule zote nchini

zinapatiwa walimu wa hisabati kama ilivyowahi kufanya kwenye somo la sayansi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kuna shule hazina walimu hususani wa somo la hisabati na upungufu umekuwa mkubwa. Ndiyo maana katika mpango wetu, ambapo tumeomba kibali Utumishi, tutakapokuwa tumepata sehemu yake ni kuajiri walimu wa sayansi hususani walimu wa hisabati ili kuhakikisha kwamba tunakabiliana na hii changamoto iliyopo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo**.**

*(Hapa Mhe. Mrisho Gambo alichelewa kuitikia Kiti)*

**NAIBU SPIKA:** Gambo! Vipi mzee, umeamkaje leo?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimwa Naibu Spika, na mimi napenda kuuliza swali la nyongeza; kwa maana ya kwamba tunafahamu changamoto ya walimu wa sayansi kwenye Jimbo la Arusha Mjini

ni kubwa sana na hata kwa nchi nzima. Je, Serikali ina mpango gani wa kuja na mkakati Madhubuti wa kuondoa changamoto ya walimu wa sayansi wa nchi nzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba mpango wa Serikali namba moja ni kuajiri ajira mpya ambazo sehemu kubwa itakuwa ni kuchukua walimu wa sayansi. Mpango wa pili ni kuhakikisha kwamba sasa hivi sisi Ofisi ya Rais-TAMISEMI tukishirikiana na Wizara ya Elimu matarajio yetu ni kuanza kuwatumia hao walimu waliomaliza ambao watakuwa wanajitolea wenye *professiona*l hiyo kuhakikisha kwamba tunaondoa hiyo changamoto. Kwa hiyo tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba masomo ya sayansi tunapaa walimu na vifaa vilevile ili kuhakikisha wakati wote yanakuwa yanafundishwa, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Rais Utawala Bora. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji.

Na. 53

## Wananchi ambao Hawakuingizwa kwenye Mfuko wa *TASAF* – Mwera

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuwasaidia Wananchi wa Mwera ambao hawakuingizwa *TASAF* na wanaishi chini ya viwango vya umaskini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unatekelezwa katika halmashauri 184 za Tanzania Bara na Unguja na Pemba katika vijiji, mitaa na shehia zote 410 (shehia 259 kwa Unguja na 151 kwa Pemba).

Kundi la kwanza la wanufaika wa *TASAF* waliingia kwenye Mpango mwaka 2014. Hata hivyo, si maeneo yote yalifanikiwa kuingia katika kipindi hicho. Kundi la pili liliandikishwa na kuanza kupata ruzuku mwaka 2021, ambapo Mwera waliandikishwa walengwa 924. Kundi hili ni la Walengwa ambao hawakuwa wamefikiwa katika kipindi cha kwanza na hivyo kukamilishwa kwa asilimia 100 ya idadi ya

mitaa, vijiji na shehia zote nchini kuwa na wanufaika wa *TASAF* ikiwemo Jimbo la Mwera.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zahor.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ningeomba Serikali itusaidie kufahamu.

Je, kwa wale ambao walikuwemo kwenye mfuko wa *TASAF* lakini hawaku–*qualify* kuondoka lakini hawakurudishwa tena kwenye mfuko huu kwenye muda huu? Tafadhali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zahor Haji, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa walengwa ambao walikuwemo kwenye mpango wa *TASAF* lakini baadae ikaonekana hali zao zimeimarika na kutolewa haijazuiwa wao kurudishwa kwenye mpango wa *TASAF* pale ambapo watakuwa wameshuka chini ya vile vigezo ambavyo vimewekwa vya mtu kuonekana ana hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba nitakaa na Mheshimiwa Zahor Haji ili tuweze kuona ni namna gani wataalamu wetu wa *TASAF* wanaweza

kwenda pale Mwera na kuangalia hizo kaya ambazo zilitolewa na ziweze kurudi katika mpango wa *TASAF*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Mheshimiwa Kimei.

Na. 54

**Manufaa ya Mifuko ya Uwezeshaji wa Wajasiriamali Jimboni Vunjo**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza: -

Je, wananchi wa Vunjo wamenufaika vipi na Mifuko ya Uwezeshaji ya Wajasiriamali kama *NEEC*, *NEDF*, *SELFU* na *TAFF*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko na programu za uwezeshaji zimetoa manufaa makubwa katika kuwezesha mikopo, ajira, kipato kwa wananchi wakiwemo wananchi wa Vunjo. Mifuko na programu za uwezeshaji zimetoa jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 5.68 tangu kuanzishwa

kwake. Mathalani katika Jimbo la Vunjo, kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022 mfuko wa *NEDF* umetoa mikopo 11 yenye thamani ya milioni 25.2 na Mfuko wa *TAFF* umetoa ruzuku yenye thamani ya shilingi milioni 20, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, inasikitisha sana, nashukuru sana ametoa majibu ya swali hilo. Hata hivyo inasikitisha sana kwamba mifuko hii inajikita kwenye majiji na kwenye manspaa ambazo zina uwezo mkubwa kwa zile asilimia zao 10 kutoa mikopo kwa vijana, wanawake na walemavu. Wamejikita huko sasa, ni ile ile dhana kwamba watu wanaohitaji zaidi ni vijijini lakini hii mifuko hailengi wale wa vijijini.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuhakikisha kwamba mifuko hii inabadilisha misimamo yake au mitizamo yake na kulenga zaidi Halmashauri kwenye wilaya za vijijini? Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha mifuko hii ili kupunguza gharama za uendeshaji na pia kutoa usawa zaidi na ufanisi katika kutoa mikopo yake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kimei, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika moja ya mikakati ambayo tunaifanya Serikali ni kuona namna gani mifuko hii ya uwezeshaji itawasaidia zaidi wananchi walioko katika maeneo ya vijijini na ndio maana moja ya mifuko hii au pesa zinazotolewa kwa wajasiliamali ile asilimia 10 ina gusa katika Halmashauri zote ambazo zinagusa pia vijijini. Pia zaidi tutaangalia na hii mifuko mingine ikiwemo ya *NEDF*, *SELFU* na *TAFF* iweze kufika kule vijijini kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili tayari tumeshaanza na kazi hiyo inafanyika, kuona namna ya kuunganisha mifuko inayotoa fedha au inahudumia shughuli zinazofanana na taarifa hiyo tayari inakamilika iko kwenye hatua za mwisho kuona mifuko ipi itaunganishwa ili kupunguza wingi wa mifuko hii, ambayo inahudumia watu wanaofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali inaonesha kusua sua kwa ufanisi wa mifuko hii, na ni tangu Bunge la Kumi na Moja tumekuwa tukizunngumza kuhusu kuunganisha mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, mifuko ya ujasiriamali.

Je, ipi kauli ya Serikali, kwa kutumia muda mrefu kiasi hiki, wanasemaje kuhusiana na kuharakisha

mchakato kwa sababu ni fedha za Serikali zinazoenda huko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema Serikali tumeshaanza na tumeshafika hatua ya mwisho. Naamini katika mwaka wa fedha ujao kutakuwa na taarifa kamili ya nini mfuko huu pia utapunguzwa. Kwa sababu tuna mifuko zaidi ya 72 lakini kati ya hiyo tisa ni ya sekta binafsi, 63 ndiyo ya Serikali. Kwa hiyo, tunaanza kwanza hii ya Serikali 63 tuone namna gani tunapunguza ili iweze kuwa na tija kama ambavyo Bunge lako limeendelea kushauri, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi hiyo hiyo. Mheshimiwa Neema Mgaya.

Na. 55

**Utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa Liganga na Mchuchuma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kuona mradi unganishi wa Linganga na Mchuchuma unatekelezwa mapema iwezekanavyo. Serikali imefanya uthaminishaji mpya katika eneo la mradi baada ya ule wa kwanza kwisha muda wake kwa mujibu wa sheria na zoezi la kuhuisha tathmini ya taarifa za wananchi lilikamilika mwezi Disemba, 2022. Pia tumehuisha majadiliano na mwekezaji wa mradi ili kuhakikisha majadiliano yanakamilika kwa wakati pasipo kuleta hasara kwa Taifa na kutoa fedha za kutengeneza miundombinu kwa maana sehemu korofi za barabara katika eneo la Milima ya Kemilembe Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa Mradi huo kwa Taifa letu, napenda kuwahakikishia kuwa juhudi zinazofanyika hivi sasa zitawezesha utekelezaji wa mradi huo haraka.

Mheshimiwa naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa usemi wa majadiliano unaendelea na umekuwa wimbo wa muda mrefu; na kwa kuwa mradi huu nji muhimu sana kwa Taifa letu ikiwa ni sambamba na kupata ajira 5,000 zilizo rasmi na zisizo rasmi 25,000 na vile vile tunatambua kwamba, baada ya miaka 15 makaa ya mawe yatakuwa hayana soko tena duniani kutokana na teknolojia zinazoendelea.

Je, Serikali inaweza ikatupa muda *specific time* lini mtamaliza majadiliano na muwekezaji huyu ili tuende awamu nyingne na mradi huu, uweze kutekelezeka kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Neema William Mgaya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka wakati tunawasilisha Taarifa ya Kamati kwenye Bunge lako tumeeleza kwa kirefu jinsi ambavyo Serikali imechukua jitihada za maksudi kuhakikisha tunakamilisha mapema majadiliano haya, lakini changamoto ilikuwa kwa upande wa wawekezaji hawa ambao tuliingia nao mkataba kabla. Hata hivyo tunaamini katika mwaka wa fedha ujao (2023/2024), *In Shaa Allah,* tutaweza kukamilisha kwa sababu tayari tuko kwenye hatua nzuri zaidi ili tuweze kufikia hatma ya majadiliano haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri haya majibu mnayo sasa huu ni mwaka wa 10 ndio hivyo hivyo. Huu ni mwaka wa 10 kila mkija mnajibu hivyo hivyo. Na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kama si vita hii ya Ukraine makaa haya yasingekuwa na *market* sana duniani (*Makofi*)

Kwa hiyo wote mnaohusika mnaweza mkaja kuwajibishwa kutokana na haya mambo mnayafanya. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Madini, Mheshimiwa Kishoa.

Na. 56

**Kuiwezesha GST kufanya utafiti wa madini**

**MHE. NUSRAT S. HANJE K.n.y MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuiwezesha *GST* kufanya utafiti wa madini yanayohitajika kwenye soko la dunia kutengeneza nishati safi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa ni asilimia 16 tu ya nchi yetu ndiyo imefanyiwa utafiti wa kina kubaini aina na kiasi cha madini mbalimbali yanayopatikana kwa kutumia teknolojia ya urushwaji wa ndege *(High Resolution Airborne Geophysical Survey)*. Teknolojia hiyo hutoa picha ya chini ya ardhi inayoonesha mikondo na miamba inayobeba madini ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara ya Madini imekwisha andaa mpango mkakati wa utafiti utakaowezesha kutafiti asilimia 50 ya nchi yetu ili kupata na taarifa za kina ikiwemo za madini ya nishati safi. Mpango huo umekwisha kuainishwa na maeneo ya kipaumbele kulingana na aina ya madini yanayohitajika zaidi nchini kwa sasa. Ili kufanikisha azma hiyo, Wizara inajadiliana na sekta binafsi zinazoonesha nia ya kushirikiana na *GST* ili kuwezesha utafiti wa kina wa madini mkakati wa teknolojia ya utafutaji, uvunaji na uongezaji thamani madini ya mkakati kwa kuwa ni gharama kubwa sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kishoa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini ni kweli kwamba *GST* ina uwezo mdogo sana wa kiteknolojia kulingana na maendeleo makubwa teknolojia duniani. Sasa Serikali ina mkakati gani wa dharura kuiokoa ***GST*** kiteknolojia kwa sababu uwezo wake ni mdogo sana kiasi kwamba hata *minerals* zile *certified mineral chemicals* ambazo zinasaidia kuthibitisha ubora wa sampuli haina uwezo uo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura kuokoa *GST?*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia swali la pili, mpaka sasa Serikali imetoa leseni ngapi ambazo ziko kazini sasa hivi za madini ya kimkakati ambayo tunategemea *GST* itusaidie kuyabaini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, la uwezo mdogo wa *GST* wa kufanya utafiti, naomba nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba *GST* kama taasisi ya utafiti itashirikiana na sekta binafsi. Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, tunazo kampuni mbalimbli ambazo ziko ndani na nje ya nchi ambazo zinafanya kazi ya utafiti kusaidia Taifa letu. Hivi sasa tumeshazungumza na kampuni mbalimbali kubwa duniani kwa akjili ya kufanya utafiti huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwamba tumetoa leseni ngapi; tumeshatoa leseni kadhaa, naweza nisijue kwa idadi, lakini madini yote ya mkakati anayoyafahami iwe *nicke*l, iwe *graphite* iwe *rare earth,* iwe *helium* na kadhalika; yote haya kuna leseni na makampuni mbalimbali yanaendelea na utafiti hapa nchini. Kwa hiyo naomba nimuhakikishie, *demand* ya madini mkakati ambayo anahitaji sasa hivi ni jambo ambalo halikuwa la muda mrefu, na

wawekezaji wengi walikuwa *busy* na madini mengine. Sasa hivi muelekeo mkubwa ni kufanya haya madini mkakati na kampuni nyingi zipo zinafanya hizi kazi. Baada ya muda ataona migodi mingi inajengwa kama ambavyo kabanga inajengwa kulee…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ahsante ushajibu vizuri sana ahsante.Mheshimiwa Kishoa, aah! tayari eh? Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Katika Jimbo la Sikonge wananchi wangu wanaendelea kuamini kwamba katika Mlima wa Kipanga, Milima ya Kisanga na Mapori ya Ipembampazi kuna madini; na hili suala limeulizwa tangu enzi za Mheshimiwa Said Nkumba akiwa madarakani.

Je, Serikali itakuja lini sasa kuja kufanya utafiti ili kuitikia wito wa wananchi kwamba kule kuna madini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba yapo maeneo mbalimbali Mkoa wa Tabora ambayo yanaaminika kuwa na madini na bahati mbaya hayajafanyiwa utafiti wa kina. Taasisi yetu ya utafiti *GST* iko katika Mikoa ya Kusini. Nataka nimhakikishie, baada ya kumaliza mzunguko wa Kanda ya Kusini

tutawapeleka na Mkoa wa Tabora, ikiwemo eneo la Sikonge ili waweze kufanya utafiti wa awali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Kamani.

Na. 57

**Gawio la Makampuni Binafsi**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Makampuni Binafsi yanayouza Hisa na hayajatoa gawio miaka mingi pamoja na kujiendesha vizuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji wa gawio kwa wanahisa wa kampuni unafanyika kwa kuzingatia Kifungu cha 180 cha Sheria ya Kampuni, Sura 212.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria hii, Serikali haiwezi kuingilia maamuzi na taratibu za kampuni kulipa gawio. Aidha, napenda kutoa rai kwa wanahisa wa kampuni mbalimbali kushiriki vikao vya mwaka vya wanahisa katika kampuni zao ili

kuwa sehemu ya maamuzi yanayotolewa kwenye Mikutano Mikuu wa Mwaka

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini bado jukumu la msingi la kulinda maslahi na vipato vya Watanzania linabaki kuwa la Serikali, basi swali langu la kwanza; je, Serikali inatambua uwepo wa makampuni haya ambayo Watanzania wamewekeza kwa kununua hisa yanafanya biashara, yanatengeneza faida na bado hayalipi magawio kwa Watanaznia hawa waliowekeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali inasemaje au ina mkakati gani wa kuja na mpango madhubuti na wa wazi wa kuhakikisha kwamba inalinda maslahi ya Watanzania hawa waliowekeza dhidi ya wizi huu wa kuaminiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kamani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza tumepokea shauri hilo na tunafuatilia mara moja. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge tuwe na mashirikiano ya pamoja katika kuzitambua kampuni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nielekeze *DSE* na *CMA* kufanya uchunguzi juu ya tuhuma hii ya wizi na mara tu zitakapobainika hatua za kisheria zitachukuliwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nafahamu pamoja na kwamba sheria hiyo ipo na sisi ndio tunaosimamia utawala wa sheria, lakini nafikiri pia makampuni haya yanasimamiwa kwa *regulation* za taratibu zetu za nchi.

Sasa tunaomba kujua Serikali ina mpango gani sasa wa kuitisha taarifa za mashirika hayo ili kujua wametoa gawio kiasi gani na tangu walipoanza kuuza hisa wametoa gawio kiasi gani na kuwapa wananchi taarifa nini hatma yao? Tuna makampuni kwa mfano, *Vodacom,* tunaomba kujua hasa…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa umeshauliza swali moja inatosha.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni shauri na shauri lake tumelichukua, tunaenda kulifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa mujibu wa Sheria ya *EPOCA* inasema kwamba walau asilimia 25 ya Makampuni ya Simu yawe yameji-*register* kwenye soko la hisa. Je, ni lini makampuni ambayo bado hayajaji-*register* yatafanya jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Hili swali la takwimu eeh? Sasa nafikiri Mheshimiwa Waziri hilo swali lichukue, halafu utakaa naye Mbunge utamweleza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Sasa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Lugangira.

Na. 58

**Kuzitambua kisheria, kuzilinda, kuhifadhi na kusajili mbegu za asili**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha mbegu za asili zenye virutubisho zinatambulika kisheria, zinalindwa, zinahifadhiwa na kusajiliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha Kitengo cha Taifa cha Hifadhi ya Nasaba za Mimea chini ya Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania *(TPHPA)* kwa ajili ya kuzitambua na kuzihifadhi nasaba za mimea ikiwemo mbegu za asili za mazao ya kilimo zilizopo nchini. Hadi kufikia Desemba, 2022, sampuli 10,000 ya nasaba za mimea zimekusanywa kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini na kuhifadhiwa katika Benki ya Taifa ya Kuhifadhi Nasaba za Mimea iliyopo Makao Makuu ya *TPHPA* - Arusha. Serikali imeanza kutekeleza taratibu za kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Hifadhi ya Nasaba za Mimea ambayo itabainisha taratibu za kisheria za kuzitambua, kuzisajili, kuzihifadhi na kutumia mbegu za asili za mazao zilizopo nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo

maswali mawili ya nyongeza. Swali kwa kwanza; kwa kuwa tayari ipo Sheria ya Mbegu ya Mwaka 2003 ambayo ilifanyiwa maboresho mwaka 2014, je, kwa nini Serikali ianzishe upya mchakato wa kuleta sheria mpya badala ya kuongeza kwenye hii Sheria ya Mbegu iliyopo ya mwaka 2003 utambuzi wa mbegu za asili kwa kuwa sheria hii inatambua mbegu za kisasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; naipongeza Serikali imeanzisha hiki Kitengo cha Taifa cha Kuhifadhi Vinasaba vya Mimea ikiwemo mbegu za asili, lakini tokea mwaka 2005 zaidi ya miaka 15, Sheria ya *National Plant Genetic Resource Act* bado haijawahi kupitishwa, kwa hiyo kitengo hiki kimsingi hakina meno wala hakiwezi kutambua wala kulinda mbegu za asili ikiwemo na hivi vinasaba na ikiwemo pia kulinda hakimiliki ya mbegu zetu za asili…

**NAIBU SPIKA:** Swali.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Je, Serikali itailleta lini Bungeni Sheria hii ya *National Plant Genetic Resource* ili tuweze kuhakikisha kwamba kitengo hiki kinafanya kazi ipasavyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anakuwa mfuatiliaji mzuri wa masuala haya, lakini swali lake la kwanza ni kwamba, tumepokea wazo lake la maboresho ya sheria iliyopo lakini pamoja na hiyo sheria aliyouliza katika swali lake la nyongeza ni sheria ambayo ndio itakuja hasa kuja kuzitambua na vilevile kuzungumzia usajili wa mbegu za asili, ambao sheria hii mpaka hivi sasa ipo katika ngazi ya *IMTC*. Tunaamini kabisa taratibu zinaendelea vizuri na sheria hii italetwa hapa Bungeni ili iweze kupitishwa na basi tuwe tuna sheria ambayo itakuwa inatambua lakini vilevile ambayo itakuwa ina usajili mbegu za asili kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mnzava kwa niaba ya Mheshimiwa Reuben.

Na. 59

**Mpango wa Serikali juu ya upatikanaji wa chakula kwa wananchi**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO K.n.y. MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia upatikanaji wa chakula cha bei nafuu kwa wananchi walioathirika na ukame nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.
**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* imeendelea kutoa chakula na kukiuza chini ya bei ya soko. Hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2023, kiasi cha mahindi tani 24,975 zimepelekwa na kuuzwa katika Halmashauri 60 nchini katika vituo vya mauzo 116. Katika Halmashauri ya Korogwe, kituo cha mauzo kimefunguliwa eneo la Masewa tarehe 27 Januari, 2023. Jumla ya tani 32 zimepelekwa na tani 10 zimeshanunuliwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Reuben.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa niulize swali moja la nyongeza. Korogwe Vijijini inazo Tarafa tatu ambazo zina jiografia ngumu sana, Tarafa ya Magoma, Mombo na Bungu. Mheshimiwa Mbunge Mnzava anataka kujua kwa nini Serikali isiweke kituo kingine cha pili katika eneo la Makuyuni ambako ndio Makao Makuu ya Halmashauri ili iweze kuhudumia Tarafa zilizobaki za Mombo na Mashewa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo la Makuyuni tutaipeleka hii *selling point* yetu na niwaondoe hofu wananchi wa Korogwe Vijijini watanunua mahindi kupitia eneo hilo la Makuyuni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Tunaishukuru Serikali kwa kutoa chakula cha gharama nafuu. Je, Serikali ina mkakati gani kwa kaya ambazo hazina uwezo wa kununua chakula kwa sasa ili itoe chakula cha msaada?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taratibu ambazo huwa zinapelekea Serikali kufikia hatua hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameiomba, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, zipo taratibu za kwenda ofisi ya Waziri Mkuu ambayo pia wao wamekuwa wakiwasiliana nasi juu ya namna ya kupeleka chakula hiki cha msaada katika baadhi ya maeneo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga jiandae, Mheshimiwa Njau.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza

swali la nyongeza. Katika Jimbo langu la Kalenga hasa Tarafa ya Kalenga tulipata shida ya mvua na tayari kata zile tumeshaleta maombi. Je, ni lini sasa Wizara itatupelekea chakula kwa haraka ili wananchi wangu wasife?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama maombi yake yamekwishawasilishwa ndani ya Ofisi ya *NFRA,* nataka nimhakikishie ndani ya siku mbili zijazo, mahindi yatamfikia katika jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa upandaji wa chakula unategemea gharama kubwa wanazozitumia wananchi katika kulima kwa maana ya kuchelewa kupeleka mbolea. Je, ni nini mkakati wa muda mrefu wa Serikali katika kuhakikisha wanapeleka mbolea kwa wakati ili wananchi waweze kulima kwa faida?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumepata changamoto katika msimu huu wa upatikanaji wa mapema wa mbolea hasa ile ya kupandia, kukuzia na kunenepeshea. Nataka nimwondoe hofu kwa mfumo ambao tumeuweka kwenye msimu ujao, tutahakikisha wakulima wanapata pembejeo hizo kwa wakati ili waendane na msimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ya Nanyumbu inakabiliwa na njaa kubwa kutokana na shambulio la panya ndani ya Wilaya yangu. Tuliandika barua tupatiwe chakula cha bei nafuu hadi sasa hivi hatuna majibu. Je, ni nini kauli ya Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Mhata, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimaliza kujibu maswali haya mimi na Mbunge tutakaa nione barua yake imefikia wapi, lakini nataka nimuahidi kwamba nitampelekea mahindi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante mtakaa, mtazungumza. Ahsante. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Tauhida Gallos.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Tauhida Gallos…

**NAIBU SPIKA:** Subiri, subiri, Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri, Mheshimiwa Antony Mavunde, nataka tuweke jambo hili vizuri kuhusiana na suala hili la njaa. Maeneo mengi Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakitoa taarifa kwamba, kuna shida ya upungufu wa chakula na kwa sababu hiyo sisi kwa mujibu ya Sheria ya Maafa, masuala ya chakula au upungufu wa chakula tunayachukulia kama ni maafa. Kwa tafsiri hiyo utaratibu wake ni kwamba, Halmashauri, Mkurugenzi anaandika barua kwa utaratibu wa kuleta kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kupitia Mkoani, halafu barua ile inapelekwa kwa Waziri Mkuu, kwa ajili ya kupata kibali sasa ili chakula kile kiweze kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaotumika sasa ni kama kila mmoja anaenda tu kiholela hivi, lakini kimsingi jukumu la kutoa kibali cha kwa ajili ya chakula ya bei nafuu au cha msaada ni jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu itakachofanya ni kuwaelekeza Wizara ya Kilimo ili Wizara ya Kilimo sasa waielekeze *NFRA* kwenda kuangalia maeneo ya kupeleka, kuuzia kile chakula au mtu atakayenunua kile chakula na kwenda kukiuza kwa bei nafuu iliyopangwa. Kwa hiyo niwaombe sana ni kutokana na kukiukwa utaratibu huo, ndio maana mambo hayaendi pamoja na kuwa kwamba barua zimeandikwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, *Chief Whip* umeliweka vizuri sana na ahsante sana. Kwa hiyo misafara kwa Waziri wa Kilimo sasa basi, nendeni kwa, pelekeni barua kutoka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zenu.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Tauhida, kwa niaba yake.

Na. 60

**Kulinda miundombinu ya maji nchini**

**MHE. ASYA SHARIF OMAR K.n.y. MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kulinda miundombinu ya maji nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali ni kuhakikisha miundombinu ya maji inayojengwa inatunzwa na kulindwa ili kutoa huduma endelevu. Katika kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi, Serikali ilitunga Sheria Na.5 ya Mwaka 2019 ambayo inakataza kuharibu, kuvamia au kufanya shughuli za kibinadamu katika maeneo yenye miundombinu ya

maji. Kupitia sheria hiyo ni kosa la jinai kuharibu miundombinu ya maji. Aidha, Serikali inaendelea kujenga uzio kwenye miundombinu ya maji ikiwemo matanki ya kuhifadhia maji na mitambo ya kutibu maji. Vilevile, elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji nchini inaendelea kutolewa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kwa niaba ya Tauhida.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pamoja na majibu yake mazuri labda atueleze Mheshimiwa kuna mkakati gani wa wale wananchi ambao wanaharibu kwa makusudi miundombinu hii ya maji nchini na hasa tukizingatia matumizi ya maji ni makubwa, lakini pia na mahitaji makubwa kwa wananchi wetu mjini na vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Sijamwelewa.

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia tena swali lako.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nilisema nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako, lakini pia nina swali la nyongeza kwamba, mna mkakati gani wa kuwachukulia hatua wale wananchi ambao wanaharibu kwa makusudi miundombinu ya maji tukizingatia mahitaji ni makubwa ya wananchi mjini na vijijini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tauhida ambalo limeulizwa kwa niaba yake, kwanza nipokee pongezi lakini mkakati ambao tunaendelea nao ni kuchukua sheria. Sheria ziko bayana, kwa hiyo yoyote ambaye atakutwa sheria itafuata mkondo wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha usanifu wa matenki na michoro ya miundombinu katika Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria inayoenda katika Miji ya Urambo, Sikonge na Kaliua inaisha? Kwani usanifu huu ulitakiwa uishe Desemba, 2022 na ukizingatia Miji hii tayari ipo kwenye *exemption* ya kodi ili Mkandarasi aweze kwenda *site* na wananchi wa maeneo haya waweze kupata maji kwa urahisi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jacqueline, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu ulipaswa kukamilika Desemba na sasa ni Januari, tuko mwishoni kabisa kukamilisha na lengo letu ni kuhakikisha dhumuni la kupeleka maji maeneo haya

aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge tunakwenda kukamilisha kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ikiwa wananchi wanapoharibu miundombinu ya maji wanachukuliwa hatua, je, ni ipi kauli ya Serikali pale ambapo miradi au miundombinu inapokuwa imekamilika watu wa mwenge wanapokuja kuzindua mradi, maji yanatoka lakini baada ya wiki mbili, hakuna maji tena, mnachukua hatua gani kwa udanganyifu wa wakandarasi wao ambao wanaidanganya jamii na hakuna maji na limekuwa ni jambo ambalo limezoeleka kwenye miradi mingi ya maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, udanganyifu wa aina hii Mheshimiwa Waziri alishaukomesha kwa kutuma vikosi kazi kuhakikisha mradi kama umezinduliwa unabaki kuwa endelevu. Nitafuatilia mradi huo anaouongelea Mheshimiwa Mbunge kujua tatizo ni nini ili kuhakikisha huduma iliyokusudiwa inapatikana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa George Malima.

Na. 61

## Kuanza kazi kwa visima vilivyochimbwa Mji wa Mpwapwa

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza:-

Je, ni lini visima viwili vilivyochimbwa katika Mji wa Mpwapwa Mwaka 2021 vitaanza kufanya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka fedha 2022/2023, Serikali imepanga kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kutoka kwenye visima viwili vilivyochimbwa katika Mji wa Mpwapwa mwaka 2021. Kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilometa 48.8, ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 200,000 na ujenzi wa vituo 18 vya kuchotea maji. Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa Ujenzi zinaendelea na ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2023 na kukamilika mwezi Aprili mwaka 2024. Kukamilika kwa mradi huu kutanufaisha wananchi wapatao 21,360 waishio kwenye Kata za Vihangwe na Mpwapwa Mjini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlima. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza: Sambamba na visima hivi viwili kuchimbwa Mpwapwa Mjini, lakini mwaka wa 2021 kilichimbwa kisima kimoja katika Shule ya Sekondari ya Berege na mpaka sasa hivi akijaanza kufanya kazi: Je, ni lini kisima hiki nacho kitaanza kutoa huduma kwa wanafunzi wale wa Shule ya Sekondari ya Berege?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, kuna Miradi mitatu ya maji inatekelezwa katika Jimbo la Mpwapwa katika Kata ya Ving'hawe, Lupeta na Kijiji cha Igojiwani Kata ya Mima, lakini kasi ya utekelezaji wake imekuwa hafifu; je, nini tamko la Wizara kuhusu utekelezaji hafifu wa miradi hii? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Naomba arudie la kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Swali la kwanza naomba urudie.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema, sambamba na uchimbaji wa visima hivi viwili katika Mji wa Mpwapwa pia kilichimbwa kisima kimoja katika Shule ya Sekondari ya Berege na kisima hiki mpaka sasa hakijaanza kufanya kazi: Ni lini kisima hiki kitaanza kutoa huduma kwa wanafunzi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge George Malima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema, miradi yote ambayo imeanza kutekelezwa Waheshimiwa Wabunge ni lazima ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ambao utekelezaji wake Mheshimiwa Mbunge George ameuona ni hafifu, tutausimamia. Mradi namna mkataba umesainiwa tutajitahidi ukamilishwe ndani ya wakati. Kwa kisima kilichochimbwa shuleni, pia ni moja ya mikakati ya Wizara kuhakikisha maeneo kama haya ya shule au hospitali na vituo vya afya yanapata huduma ya maji safi na salama bombani. Hivyo kisima hiki kilichochimbwa pia tunakuja kukifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa agizo kupitia Bunge lako Tukufu, Watendaji wa Mkoa wa Dodoma wanaofanya kazi maeneo haya, wahakikishe wanatoa hizi sintofahamu haraka iwezekanavyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wananchi wa Kijji cha Kigorogoro Kata ya Kibale kwa muda mrefu walikuwa na changamoto ya maji ya kisima. Kilichimbwa kisima, lakini kilipoanza kutoa maji, yakawa ni maji yenye chumvi kali wananchi wakashindwa kuyatumia. Naomba kuuliza swali: Ni

lini wananchi wa Kijiji cha Kigorogoro watachimbiwa kisima kingine ambacho hakina maji ya chumvi, ukizingatia wapo kwenye ukanda wa Mto Kagera? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo kisima kimechimbwa na maji yakaonekana siyo rafiki kwa matumizi ya binadamu huwa tunayaacha na kutafuta mbadala wake. Ninaamini maeneo hayo watendaji wahusika wanaendelea kutafuta eneo mbadala na maji safi na salama lazima yaweze kuwafikia wananchi wa Kigorogoro.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka maji katika Kata ya Kwai, Kwekanga pamoja na Makanya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Shekilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hizi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge Shekilindi, nimeongea naye

juzijuzi na nimemhakikishia kwamba kazi hii tutaenda kuifanya. Tumeshakubaliana kwamba tunakwenda kuangalia mradi na tutahakikisha unatimizwa kufanyiwa kazi yake kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kuuliza, katika Wilaya ya Meatu tuna shida sana ya maji. Kwa Mkoa mzima wa Simiyu Wilaya ya Meatu inaongoza: Je, ni lini Serikali italeta maji safi na salama katika Wilaya Meatu ili wananchi wa kule wanufaike? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Simiyu una bahati sana. Una mradi mkubwa ambao unaenda kutekelezwa kwa kutumia kigezo cha mabadiliko ya tabia ya nchi. Mradi ule utafikisha maji maeneo ya Meatu, Maswa na maeneo yote yaliyo karibu kuhakikisha wananchi wanapelekewa maji safi na salama. Nafahamu Mheshimiwa Minza nawe pia umefuatilia sana suala hili, na nilifika Meatu na tunaendelea na kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lemburis.

**MHE. NOAH L. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna mradi wa vijiji tisa vya Oldonyo Sambu, Lengijave na Oldonyo-Wass ambao wanasumbuliwa na maji ya *fluoride* na imekuwa ikisuasua utekelezaji wake: Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha mradi huu ambao wananchi wanateseka na maji ya *fluoride? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Noah, Mbunge wa Arumeru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tulipata tatizo na changamoto hii bado ipo, lakini sisi kama Wizara tayari tuna hatua mbalimbali tumeshazichukua na fedha tunatarajia mgao ujao. Mheshimiwa Mbunge nawe katika mradi ule tutapata. Lengo ni kuona tunatekeleza miradi mikubwa ambayo maeneo yake, maji yake chini hayana *fluoride* ili tuweze kunusuru watoto wanaoweza kuzaliwa na ulemavu na watu wote ambao wanateseka na maji yenye *fluoride. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, niulize swali dogo moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jimbo la Kibamba maeneo ya King'azi A, B na maeneo ya Manzese Malamba Mawili ni maeneo ambayo wananchi wanaendelea kukosa maji safi na salama kwa kutumia maji ya chumvi ya visima vifupi; na ahadi ya Serikali ni kujenga tenki kubwa la ujazo siyo chini ya lita milioni kumi pale Kilimahewa: Je, ni lini sasa Serikali itaanza kutekeleza mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri lini? Kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tenki lipo kwenye hatua za mwisho kabisa kuja kuanza kutekelezwa, usanifu umekamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa sana ya maji kwenye Kata ya Mtambula katika Jimbo la Mufindi Kusini; je, Serikali haioni wakati umefika sasa kuwapelekea maji sasa wananchi wa kata hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari tumeona umuhimu na tupo katika taratibu za kuhakikisha hayo maeneo uliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, tunayaletea maji safi na salama yakiwa bombani.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Getere.

Na. 62

**Kauli Juu ya Maeneo ya Serikali na Taasisi**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, Serikali ina kauli gani juu ya maeneo ya ardhi yanayotumika na Serikali au Taasisi zaidi ya miaka 12 yakiwa hayana hatimiliki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo

ya Makazi, naomba kujibu swali Na. 62 lililoulizwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa maeneo mengi yanayomilikiwa na Taasisi za Umma yana hatimiliki. Hata hivyo, Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikitoa maelekezo kwa Taasisi na Idara za Umma kuhakikisha maeneo yao yanapangwa, kupimwa na kupatiwa hatimiliki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, napenda kupata ufafanuzi, mwaka 1974 mpaka 1980 kulikuwa na *program* ya Serikali kupitia Wizara ya Mifugo ya kuwasaidia wanakijiji wa Kijiji cha Mekomariro kunenepesha mifugo yao, na baada ya miaka hiyo Serikali ikaacha maeneo hayo. Ni miaka 43 sasa maeneo hayo yanatumiwa na wanakijiji, na eneo lililokuwa linatumiwa na Wizara ya Mifugo halina hati wala halina *GN*.

Ni kwa nini sasa wananchi wenye maeneo hayo bado wanasumbuliwa na Serikali kwamba eneo hilo ni la Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuna maeneo ya migogoro ya Mekomariro, Sirorisimba na Lemololi Mahanga, Ng'oroli na Mahanga, ni lini

Serikali itaenda kuwasaidia maeneo hayo kuyapima na kuyapa hati za kimila? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili yaliyoulizwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la shamba la kule Mekomariro ambalo linaonekana halina hati, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo halina ukweli wowote kwa sababu shamba lile tunavyofahamu Serikali, linayo hati. Ila tunatambua ukweli kwamba upo mgogoro baina ya shamba hilo na wananchi katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili juu ya lini sasa Serikali itaenda kumaliza jambo hilo? Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kumaliza kujibu maswali hapa, tutakaa mimi na yeye sasa tukubaliane ni lini twende katika eneo hilo ili kumaliza yale ambayo yanaendelea kuleta mgogoro katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani halafu Mheshimiwa Midimu jiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwulize Naibu Waziri wa Ardhi, Serikali inapeleka lini fedha za upimaji wa ardhi katika Halmashauri ya Ushetu hasa katika kata zinazokua kwa kasi; Kata ya Igwamanoni, Kata ya Idahina, Nyankende pamoja na Burungwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maombi ya wananchi wa Ushetu juu ya kupimiwa eneo lao yalishawalishwa kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, tutakapokuwa tumeshapata fedha hizo, tutaleta fedha Ushetu ili sasa maeneo yale yaweze kupimwa, kupangwa na kumilikisha wananchi wetu ili maendeleo yaweze kupatikana kama ambavyo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyoelekeza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba sasa swali langu namba…

**NAIBU SPIKA:** Subiri kwanza, mwenye Wizara amesimama. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka pengine nitoe ufafanuzi kuhusiana na hizi pesa ambazo halmashauri zinaomba kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha. Naomba watambue, fedha aliyotoa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ile Shilingi bilioni 50 inakwenda kwenye Halmashauri kulingana na maandiko wanayotoa. Fedha ile inakwenda kusaidia kwenye Halmashauri ambazo ndiyo zenye mamlaka ya Upangaji. Kwa hiyo, tunategemea ile pesa isihesabike kama ndiyo fedha inayokwenda kukamilisha kazi, isipokuwa Halmashauri zinatakiwa kutenga fedha ya ndani kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya ardhi. Kwa hiyo ile isihesabiwe kama ndiyo fedha ambayo inategemewa sana katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mamlaka za Upangaji, sisi tuna-*support* kuongeza kile ambacho ninyi mmetenga kwa ajili ya maendeleo ya Ardhi na siyo kwamba tunatoa bajeti kwa ajili ya ku-*fulfill* mpango mzima wa kupanga katika maeneo yenu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zeeland.

Na. 63

**Utatuzi wa migogoro ya wafugaji na wakulima - Mvomero**

**MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua migogoro ya Wakulima na Wafugaji Kata za Hembeti, Mkindo, Sungaji, Mtibwa, Kanga, Mziha na Doma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali Na. 63 la Mbunge wa Mvomero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa migogoro ya wakulima na wafugaji katika Kata za Hembeti, Mkindo, Sungaji, Mtibwa, Kanga, Mziha na Doma Wilayani Mvomero. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo hatua ya mwaka 2013 ya kutenga kwa kutumia fedha za ndani kwenda kutatua migogoro katika jumla ya vijiji 72 kati ya vijiji 130 vilivyomo katika Wilaya hiyo ambavyo vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Kwa kuwa Mvomero ni miongoni mwa Wiliya

ambazo bado zina changamoto ya migogoro ya wakulima na wafugaji: Je, Serikali inamkakati gani wa kuendelea kuyafuta mashambapori yaliyopo Mvomero ili muweze kuwagawia wananchi na kupunguza tatizo hili la migogoro ya wakulima na wafugaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Mvomero bado tuna migogoro ya ardhi pamoja na kwamba imepungua.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kuongozana nami baada ya Bunge hili kwenda kutatua migogoro hii Mvomero? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Zeeland Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na jambo la mashamba, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilishakagua mashamba 75 na katika hayo, mashamba 15 yalishatolewa ilani ya kuendelea kufuatiliwa katika maana ya kufutwa au kuona utaratibu mwingine wowote, utakaofanyika. Katika hatua hizo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pale tutakapokuwa tumekamilisha taratibu nyingine zote tutamjulisha kwa niaba ya wananchi wake ili aweze kujua hatua Serikali ilizochukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kuongozana mimi naye kwenda Jimboni kwa ajili ya kutatua migogoro hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari baada ya hapa, kwa sababu ni njia ya kwenda Jimboni kwangu, nami nitasimama Mvomero pale tuweze kutengeneza mambo mazuri ili kuweka hali ya usalama na watu wetu wakae vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Wizara ya Habari na Mawasiliano. Mheshimiwa Kamamba

Na. 64

**Hitaji la mawasiliano ya simu katika Kata za Buyungu**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Je, lini minara ya mawasiliano itapelekwa Kata za Nyamtukuza, Nyabibuye, Gwarama, Kasuga, Rugenge, Gwanumpu, Katanga na Magunzu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI,** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya *Vodacom* imetekeleza miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano ya simu katika Kata za Nyamtukuza, Nyabibuye, Gwarama, Gwanumpu, Rugenge na Mugunzu. Miradi hii imetekelezwa kati ya mwaka 2016 na 2019 ambapo ujenzi wa minara katika Kata hizi umekamilika na inatoa huduma kwa teknolojia ya *2G* na *3G*.

Mheshimiwa Naibu Spika,  kwa upande wa Kata ya Katanga na Kasuga, Serikali itafanya tathmini ya hali halisi ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano Kata hizi katika mwaka wa fedha 2023/2024, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamamba.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kakonko au Jimbo la Buyungu lina Kata 13. Kata zenye uhakika wa mawasiliano ni tano tu. Kutokana na hali hii, ndiyo imepelekea kuleta swali hapa Bungeni.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa kata nane ambazo ni Nyamutukuza, Nyabibuye, Gwarama, Kasoga, Rugenge, Gwanombo, Katanga na Mgunzu ambazo bado zina matatizo ya mawasiliano ya simu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kufuatana nami

Buyungu ili aweze kuliona na kubaini tatizo hili ambalo nalitaja sasa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Aloyce kwa kazi kubwa anayoifanya, na kwa kweli ameendelea kushirikiana na Wizara kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto za mawasiliano ndani ya jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika Jimbo ambalo lina Kata 13, Kata tano zina uhakika lakini vile vile kuna Kata karibia tano nyingine ambazo mawasiliano yapo lakini bado kuna changamoto mbalimbali ambazo naamini baada ya kuzifanyia kazi tatizo lake litaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie fursa hii, kwa sababu kwa uwepo wa *TCRA* kwa mujibu wa Sheria Na. 12 ya mwaka 2003, inaipa *TCRA* mamlaka ya kuhakikisha huduma ya mawasiliano inatolewa kwa ubora unaotakiwa. Sasa niwatake waende katika Jimbo la Buyungu wahakikishe kwamba wanaenda kufuatilia na kuangalia *quality of service* kama inaridhisha katika jimbo hili ili wananchi wa Buyungu waweze kupata huduma ya mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile jambo lingine, Kata ya Katanga, Kasuga pamoja na Kata ya Gorama ambapo Mheshimwa Mbunge ndipo anapotoka; Gwarama ni kweli kabisa hakuna kabisa mawasiliano, lakini hii Kata imeingizwa katika mradi wa *Special Zone and Boarders* ambapo utaanza kutekelezwa muda siyo mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine Kata ya Katanga, Kasuga pamoja na Kata ya Gwarama ambapo Mheshimwa Mbunge ndiyo anapotoka. Gwarama ni kweli kabisa hakuna kabisa mawasiliano lakini hii Kata imeingizwa katika mradi wa *Special Zone and Boarders* ambapo utaanza muda si mrefu katika kutekelezwa. Mkandarasi katika eneo hilo amepatikana *(Vodacom)* na kwa hiyo tunaamini ndani ya miezi miwili, mitatu, ujenzi wa minara katika maeneo haya utakuwa umeshaanza na kwa hakika vijiji ambavyo viko katika Kata ya Katanga ambavyo ni vijiji viwili, Kata ya Kasuga vijiji vinne na Gwarama vijiji vitatu, tunaamini kwamba, wananchi wa maeneo haya watanufaika na huduma ya mawasiliano. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, Waziri amejibu mambo mengi sana mazuri na amechukua muda mwingi. Kwa hiyo, nafasi zitakuwa ni chache, Mheshimiwa Chege, Mheshimiwa Oliver, Mheshimiwa Sillo. Naanza na Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Bukura kwa maana ya Kirongwe, Roche, Goribe na Ikoma ni Kata

zilizoko mpakani na Mheshimiwa Waziri nafikiri unazifahamu hizi, lakini ni Kata ambazo hazina huduma yoyote ya mawasiliano. Pamoja na kwamba, Mkandarasi amepatikana ninataka nijue *commitment* yenu ni lini Mkandarasi huyu ataanza ujenzi wa minara kwenye maeneo haya ya mpakani kati ya Tanzania na Kenya?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani sijamsikia vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Hajakusikia vizuri Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Bukura kwa maana ya Kirongwe, Roche, Ikoma, Goribe ni Kata ambazo ziko mpakani kati ya Tanzania na Kenya. Mheshimiwa Waziri wewe unazifahamu hizi kwa sababu ulishatembelea maeneo haya:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nijue pamoja na kwamba, Mkandarasi amepatikana ni lini ujenzi wa minara utaanza kwenye maeneo haya kwa ajili ya kuboresha mawasiliano kati ya mpaka wa Kenya na Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika,

ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Mheshimiwa Mbunge jana tuliwasiliana na nikamhakikishia ndani ya miezi miwili mitatu tayari ujenzi utaanza. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa sana kwenye mitandao ya simu, hasa *Vodacom,* ukiwa unaongea ina-*stuck* au inakoroma huku inaendelea ku-*charge*. Ningependa kujua nini tatizo katika mitandao hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, *frequency* na *strength* ya *line* zenu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya kwa Mkoa wa Kagera, vilevile suala hili Mheshimiwa Waziri tayari ameshaunda timu ya kuzunguka nchi nzima kujiridhisha na huduma za mawasiliano nchini. Ni kweli kabisa kumekuwa na changamoto kama hizo, lakini tunaamini timu hii itakapokamilisha kazi yake basi tutachukua hatua stahiki ili wanchi wapate mawasiliano ya uhakika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sillo.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika Jimbo la Babati Vijijini kwenye Kata za Gidas na Ufana na kuahidi kwamba, ataleta minara ya mawasiliano. Je, ni lini ahadi hii itatimizwa ili wananchi wapate mawasiliano? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa nimeshafika katika Jimbo la Babati Vijijini na katika Kata ambazo Mheshimiwa Sillo ameziongelea, tayari zimeingizwa kwenye mradi wa Tanzania kidijitali, tenda hiyo ilifunguliwa Tarehe 31 Januari, hivyo tunasubiri majibu ili tujue kwamba, ni Mkandarasi gani anapatikana kwa ajili ya vijiji hivyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mheshimiwa Taya.

Na. 65

**Kuinua ushiriki wa michezo kwa watu wenye ulemavu**

**MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuinua ushiriki wa Watu wenye Ulemavu katika michezo ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa wavu na pete?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa haki sawa ya ushiriki katika michezo kwa makundi yote ikiwemo watu wenye ulemavu. Moja ya mikakati ya Serikali katika kuinua ushiriki wa watu wenye ulemavu hususani kwenye mpira wa miguu, wavu na pete ni pamoja na kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kushirikisha watu wenye ulemavu katika michezo, kusajili vyama na vilabu vya michezo kwa watu wenye ulemavu, kushirikisha michezo ya watu wenye ulemavu katika matukio yote ya michezo hususani yanayoandaliwa na Serikali, hii ni pamoja na kuziwezesha timu za Taifa za watu wenye ulemavu zinaposhiriki katika mashirikisho mbalimbali ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa michezo imeendelea kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya michezo yenye mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taya.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu zuri:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza; kwa kuwa, Serikali inafahamu fika michezo sanaa na tamaduni ni moja ya suluhu ya kuongeza ajira katika nchi yetu. Sasa Serikali haioni sababu ya kuipa kipaumbele michezo, sanaa, ili waweze kutatua tatizo la ajira kwa watu wenye ulemavu?.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Ni vijana wangapi wa Tembo *Warriors* wmepata ajira baada ya kombe la dunia? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khadija, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Khadija kwa kuwa, yeye ni mdau wa Wizara yetu..

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri jibu swali la kwanza tu, swali la pili linahitaji takwimu kwa hiyo, utajibu baadae.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa naibu Spika, ahsante. Swali lake la kwanza alipenda kufahamu ni kwa kiasi gani Wizara tunahakikisha kwamba, tunaendelea ku-*promote* michezo hii ya wtu wenye ulemavu katika maeneo mbalimbali:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu inahakikisha na tunashirikiana na vyama mbalimbali, katika miundombinu tunahakikisha watu wenye ulemavu wanapewa kipaumbele, hata katika ujenzi wetu wa shule 56, miongoni mwa shule ambazo tumezitenga zipo za watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, tunaendelea kuwashirikisha na kuwajengea miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili. Alipenda kufahamu wenzetu wa Tembo *Worriers*…

**NAIBU SPIKA:** Hili ni swali la takwimu kwa hiyo usilijibu.

Mheshimiwa Waziri ahsante, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ally Makoa.

Na. 66

**Wananchi walioharibiwa mazao na tembo – Kondoa Mjini**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, ni Wananchi wangapi Kondoa Mjini walioharibiwa mazao yao na tembo wamehakikiwa na lini watalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya tarehe 25 na tarehe 28 Septemba, 2022, Wizara ilifanya uhakiki wa madai ya kifuta jasho ya wananchi 274 wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa walioharibiwa mazao yao na tembo. Baada ya uhakiki huo kukamilika, Wizara iliwalipa wananchi 198 wa Vijiji vya Chemchem, Tungufu, Tampori, Mulua na Iyoli mwezi Novemba, 2022. Jumla ya shilingi 40,013,750 ikiwa ni kifuta jasho kutokana na madhara yaliyosababishwa na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imepokea madai mengine mapya ya wananchi 28 wa vijiji vya Unkuku, Kwapakacha, Serya, Damai, Chemchem na Mulua ambayo yamewasilishwa hivi karibuni. Madai hayo yanaendelea kufanyiwa kazi na malipo yatafanyika baada ya taratibu stahiki kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Moja; kwa kuwa kiwango wanacholipwa wakulima walioharibiwa mazao na wanyama ni kidogo sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadili sheria, ili kuweza kuwalipa wananchi kulingana na thamani ya mali zao zinazoharibiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, pamekuwa pakitokea matukio haya ya tembo mara kwa mara katika maeneo hayo hususan Kijiji cha Chemchem, ni lini Serikali sasa itatujengea kituo cha Askari wa Hifadhi, ili kuweza kuzuia athari zaidi katika mzao ya wananchi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Kilango.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza mawili, ya Mheshimiwa Ally Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wananchi wamekuwa wakilipwa kiwango kidogo. Na kiwango hiki cha kifuta machozi ama kifuta jasho ni ile tu kutoa pole kwa wananchi na kuweka mazingira ya ushirikiano baina ya uhifadhi na wananchi, lakini tulipata maelekezo katika Bunge lako hili Tukufu wakati wa bajeti kwamba, tupitie kanuni za sheria hizi

na tayari Wizara imeshaanza kuzipitia kwa ajili ya kurejea upya kanuni hizi, ili kifutajasho basi kiweze kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ninamuahidi Mheshimiwa Mbunge wa Kondoa Mjini, Mheshimiwa Ally Makoa kwamba, katika bajeti hii ya 2022/2023 tumeoanga kujenga vituo 13, vituo hivi vitapelekwa katika Jimbo lake ili tuweze kupeleka Askari waweze kuendelea na zoezi la kuzuia wanyamapori wakali na waharibifu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Waziri umeshafika kwenye Jimbo langu ndani ya Kata ya Maore, umeona ni kiasi gani wananchi wangu wanauawa na kuharibiwa mazao yao. Je, huoni umuhimu sasa kujenga kituo pale ndani ya Kata ya Maore ili uepushe maisha ya wananchi wangu na hatari? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mama Anne Kilango, Mbunge wa Same, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilifika katika eneo hilo la Maore na kuna changamoto kubwa

sana ya wanyama wakali na waharibifu. Tuliahidi kujenga bwawa lakini pia tutapeleka kituo ambacho kitasaidia hawa wananchi kupunguza adha hii ya wanyama wakali na waharibifu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Raymond.

Na. 67

**Kiasi cha ngozi kinachozalishwa kwa mwaka**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, ni kiasi gani cha ngozi kinazalishwa kwa mwaka mzima na kutumika nchini na kiasi gani ghafi kinauzwa nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inazalisha wastani wa vipande milioni 13.6 vya ngozi kwa mwaka. Kati ya vipande hivyo, milioni 4.2 ni vya ng’ombe, vipande milioni 6.9 ni vya mbuzi na vipande milioni 2.5 ni vya kondoo. Kwa sasa, tunavyo viwanda vitatu vinavyofanya kazi ya usindikaji wa ngozi katika hatua ya kati *(wet blue)* na hatua ya mwisho *(finished leather)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngozi zinazosindikwa katika hatua ya kati ni vipande 51,866 vya ngozi ya ng'ombe na vipande 262,229 vya mbuzi na kondoo. Usindikaji hadi hatua ya mwisho ni vipande 145,000 vya ngozi ya ng'ombe na vipande 259,000 vya ngozi ya mbuzi na kondoo. Pia, kuna wasindikaji wadogo wanaosindika na kutengeneza bidhaa za ngozi maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inauza nje ya nchi ngozi ghafi na iliyosindikwa hatua ya awali, wastani wa vipande 1,630,740 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 10.5 kwa mwaka. Ngozi hiyo, inauzwa katika nchi za Nigeria, Afrika ya Kusini, Ghana, Togo, Pakistan, Marekani, Italia, Dubai na China, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, nchi yetu inauza ngozi ya bilioni 10 tu kwa mwaka, lakini nchi hii-hii ndiyo ambayo imebarikiwa kuwa na mifugo mingi zaidi.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuongeza uzalishaji huo kwenye hivyo vituo viwili ambavyo vina-*process* mpaka mwisho ikiwepo *Himo Tanneries* na *Moshi Leather Industries* ili waweze kukidhi uhitaji wa nchi hii baada ya kufunguliwa

kiwanda cha uzalishaji wa *Kilimanjaro International Leather Industries?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ina mkakati gani kutoa elimu kwa wananchi wake ili kuhakikisha kwamba, mifugo inatoa ngozi bora na salama katika kipindi chote cha mwaka, ili kutoa ajira zaidi kwa vijana, wakiwemo vijana wa Kilimanjaro? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli lengo letu kama Serikali ni kuona uzalishaji kwenye viwanda vyetu vya ndani unaongezeka, jitihada kadhaa zinafanywa, ikiwemo kuondoa changamoto na kuboresha mazingira ya biashara. Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kushughulikia changamoto hizo ikiwa ni pamoja na ile ya kuondoa tozo na kodi mbalimbali zenye kuweka mkwamo wa upatikanaji wa malighafi na ushindani kwenye biashara. Baada ya kuyafanya haya tunayo imani kuwa, viwanda vyetu sasa vitapokea malighafi nyingi kutoka kwa wazalishaji ili kuviwezesha kufanyakazi yake kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili; ni mkakati gani juu ya elimu ni kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais

Samia Suluhu Hassan imetenga fedha, mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kutoa elimu kwa wachunaji wa ngozi, lakini pia vilevile kununua vifaa kama *computers,* ili tuweze kuwa na *record* ya uzalishaji sahihi wa ngozi na hatimae kuwawezesha kuwaingiza katika masoko ikiwemo viwanda vyetu ambavyo vinazalisha hapa nchini, ambavyo tayari Mheshimiwa Shally Raymond ameshavitaja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu mazuri mnayojibu Bungeni, lakini niwaombe tu kuzingatia muda na maelekezo ya Mheshimiwa Spika ya kulinda muda wakati mnajibu majibu yenu.

Waziri huna sababu ya kurudia swali la Mbunge, unaporudia swali la Mbunge unatumia muda mwingine kwa hiyo, nenda moja kwa moja mjibu ili utoe nafasi ya Kiti kiweze kuwa na nafasi kubwa ya kutoa nafasi nyingine kwa Waheshimiwa Wabunge wengine. Hongereni sana kwa majibu yenu mazuri katika Bunge.

Wageni waliopo Bungeni; Wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni Ndugu Mary Chatanda, Mwenyekiti wa UWT Taifa, karibu sana Mheshimiwa Chatanda, jumba hili ni lako, wewe ni mzoefu, umekaa nasi hapa vipindi takribani vitatu, kwa hiyo,

unalielewa vizuri jumba hili, karibu sana na hongera sana. *(Makofi)*

Tunae Mheshimiwa Riziki Kigwande, Naibu Katibu Mkuu UWT Tanzania Bara na Ndugu Dotto Maganga, Msaidizi wa Mwenyekiti wa UWT, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wafuatao; wageni watano wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mbunge, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni viongozi wa CCM kutoka Mkuranga, Mkoa wa Pwani, ahsanteni. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Patrobass Katambi, Mbunge, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambao ni *Club* ya *Rotary* na wanataaluma chipukizi wanaojihusisha na kutoa mafunzo ya kuendeleza taaluma ya ujuzi wa uongozi kwa vijana kutoka Jiji la Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 52 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Mbunge ambao ni wanafunzi wanaosoma kozi ya sheria katika Chuo Kikuu cha *St. Augustine* cha Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunae mgeni wa Mheshimiwa Jafari Chege, Mbunge ambaye ni mpiga kura wake kutoka Rorya, Mkoa wa Mara, *Engineer* Lucas Magacha. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Florence Kyombo, Mbunge, ambaye ni kada wa CCM kutoka

Misenyi, Mkoa wa Kagera, Ndugu Alex Baliagati, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, Mbunge kutoka Chama cha Ushirika – Kahama, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 90 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi *Arusha Modern* ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao watumishi watano kutoka Kampuni ya *Car and Rental Company Limited* ambao ni wauzaji wa Bajaj na pikipiki, wapo viwanja vya Bunge kuonesha bidhaa zao, karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo; Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kanuni kuwa leo siku ya Ijumaa, tarehe 3 Februari, 2023 saa tano kamili asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati ya Kanuni kitakachofanyika *Speaker's Lounge*. Wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria; saa tano kamili asubuhi hii.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Yahaya Massare. *(Makofi)*

**MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli Zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023 kwa mujibu wa matakwa ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Naomba taarifa hii pia iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyo kwenye kitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama inavyoelekezwa katika masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa Kamati; kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Tatu, Kanuni ya 10 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la

Juni, 2020, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kusimamia shughuli za taasisi mbili ambazo ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya *(DCEA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hii imeipa Kamati majukumu yafuatayo: -

a) Kusimamia utekelezaji wa masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;

b) Kusimamia shughuli zote za Serikali za kudhibiti na kutokomeza Ugonjwa wa Kifua Kikuu;

c) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI, Kifua Kikuu na udhibiti wa dawa za kulevya;

d) Kujadili hatua za kudhibiti UKIMWI, kifua kikuu na dawa za kulevya;

e) Kushughulikia bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; na

f) Kushughulikia magonjwa yasiyoambukiza ambayo yanachangia vifo vingi sana kwa wananchi kwa kukosa ufahamu juu ya magonjwa haya pamoja na kutokufanya mazoezi na kutokuwa na desturi ya kupima afya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia na mbinu zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati ni pamoja na: -

a) Vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za Wizara na taasisi mbalimbali kwa lengo la kufahamu utendaji kazi lakini pia kufahamu mafanikio na changamoto;

b) Ziara za kukagua shughuli zinazotekelezwa katika kushughulikia masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, dawa za kulevya na magonjwa yasiyoambukiza ili kujiridhisha katika hatua zilizofikiwa katika utekelezaji; na

c) Kushiriki semina, warsha na makongamano mbalimbali kuhusiana na masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, dawa za kulevya na magonjwa yasiyoambukiza kwa lengo la kujengewa uelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili; uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Katika kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023, Kamati imetekeleza shughuli zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vipindi viwili tofauti Kamati ilifanya ziara kwa lengo la kuona na kujifunza na kukagua utekelezaji wa afua za UKIMWI, Kifua Kikuu na dawa za kulevya zinazotekelezwa na Wizara, taasisi na Mamlaka za Serikali. Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Geita, Mara, Mwanza na Morogoro ambapo Kamati ilitembelea maeneo ya

migodi, vituo vinavyotoa huduma ya *CTC,* magerezani, vituo vinavyotoa huduma ya *methadone* kwa waraibu, konga za WAVIU, mialo ya wavuvi wa samaki pamoja na wanufaika wa Mradi wa Timiza Malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara Kamati ilibaini masuala yafuatayo: -

a) Ongezeko la maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI; hali ya maambukizi ya VVU bado ipo juu kwa Mkoa wa Geita (asilimia 6.4) na Mkoa wa Mwanza imeongezeka kutoka asilimia 4.7 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 5 mwaka 2016/2017 ukilinganisha na hali ya maambukizi Kitaifa ya asilimia 4.7. Kamati inaona ipo haja ya Mamlaka husika kuweka nguvu zaidi katika mikoa hii pamoja na mikoa mingine ambayo maambukizi yanaongezeka ili kupunguza maambukizi mapya.

b) Ukosefu wa elimu kuhusu UKIMWI katika maeneo ya mialo; katika baadhi ya mialo ambayo Kamati iliitembelea elimu kuhusu UKIMWI bado haijawafikia ipasavyo na hivyo watu wengi hawachukui tahadhari ya kujikinga na maradhi haya. Kamati inaziomba mamlaka husika kuhakikisha zinatoa elimu ya UKIMWI katika maeneo haya na si kusubiri ujio wa Kamati ya Bunge ndipo watembelee maeneo husika.

c) Ugonjwa wa Kifua Kikuu; kiwango kikubwa cha wagonjwa wa Kifua Kikuu Kikuu katika Mkoa wa Mara kwani katika mwaka 2021 kati ya watu 100,000 waliopimwa watu 146 waligundulika

kuwa na Ugonjwa wa Kifua Kikuu. Chanzo kimetajwa katika taarifa yetu. Na katika Mkoa wa Mwanza kati ya watu 100,000 waliopimwa, watu 145 ni wagonjwa wa Kifua Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa mashine za *X- Ray;* makopo au vifaa vya kuchukulia sampuli za makohozi na vitendanishi vya maabara;

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, msongamano wa wafungwa na mahabusu ambao kwa kiasi kikubwa umekuwa unachangia maambukizi kuenea kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Kamati kuwa changamoto hizi zifanyiwe kazi ili kupunguza maambukizi ya Kifua Kikuu nchini. Aidha, kampeni mbalimbali za uhamasishaji na upimaji wa *TB* na VVU katika msongamano wa watu na sehemu hatarishi ziendelee nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa lishe katika magereza; Kamati imebaini kwamba wafungwa na mahabusu wanapewa chakula cha aina moja tu ambacho ni ugali na maharage kila siku, hali ambayo inafanya wazidi kudhoofika kiafya kwani dawa wanazotumia ni kali na zina nguvu sana. Ipo haja sasa ya Serikali kuhakikisha lishe bora inatolewa kwa WAVIU waliopo magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa yasiyoambukiza; Kamati imebaini kuwa wapo wananchi wa kawaida, wafungwa na mahabusu wanaokabiliwa na magonjwa kama kisukari, kansa, shinikizo la damu, moyo na mengineyo. Serikali kwa

kushirikiana na sekta husika wahakikishe elimu ya kutosha inatolewa shuleni, vyuoni na kwenye jamii juu ya umuhimu wa vyakula visivyofaa na kufanya mazoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, walengwa wa Mradi wa Timiza Malengo; Kamati imebaini kuwa Mradi wa Timiza Malengo ambao unaolenga kuwafikia wasichana balehe na wanawake vijana kwa afua mbalimbali umekuwa na changamoto kutokana na walengwa wengi wa mradi kukosa viambatisho muhimu vinavyohitajika wakati wa kufungua akaunti ambavyo ni Kitambulisho cha Taifa *(NIDA)* na cheti cha kuzaliwa; na mahitaji ya walengwa ni makubwa kuliko rasilimali zilizopo na hivyo kushindwa kuwafikia wahitaji wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS);* Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa mbalimbali kutoka *TACAIDS* kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa za utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (Fungu 92) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; pamoja na makadirio ya

mapato na matumizi ya mafungu hayo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Taarifa za kina za uchambuzi wa bajeti ya Tume (Fungu 92) pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati yaliwasilishwa katika Mkutano wa Bajeti uliomalizika Juni, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Desemba 2022); katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania – *TACAIDS* (Fungu 92) iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 14.9. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kufikia Desemba, 2022, Tume imepokea kiasi cha shilingi bilioni 5.6 sawa na asilimia 37.6 tu ya bajeti iliyoidhinishwa, kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haijaridhishwa na utolewaji wa fedha hizi hususan za matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo ambazo kwa utaratibu zilipaswa kuwa zimetolewa kwa asilimia 50 kufikia Desemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Januari, 2022: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya maazimio 10 yaliyotolewa kwa Wizara hii maazimio matano yalitelekezwa katika Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Uchambuzi wa Kamati wa taarifa ya mwisho ya utekelezaji wa maazimio haya inaonesha kuwa, utekelezaji wa maazimio yote matano unaridhisha. Aidha, maazimio mengine mawili yanayohusu utoaji

wa elimu, utekelezaji wake ni endelevu. Kamati inaendelea kusisitiza masuala hayo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (*NMSF* 2018/2019 – 2022/2023); mkakati huu uliandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa Mwitikio Shirikishi wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI nchini unaunganisha mipango kazi ya wadau wa UKIMWI ili kuchangia katika kufikia malengo tuliyojiwekea. Aidha, mkakati huu ni zana ya *TACAIDS* na wadau wa maendeleo katika kufuatilia utekelezaji wa mwitikio wa UKIMWI kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea taarifa ya hatua iliyofikiwa. Hata hivyo, Kamati imebaini masuala mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi yakiwemo:-

i. Mkazo zaidi unahitajika kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya VVU na vifo vitokanavyo na UKIMWI;

ii. Kunahitajika jitihada zaidi ili watu wengi waweze kujua hali zao za maambukizi kwani 95 ya kwanza bado ipo chini; na

iii. Ipo haja ya kuendelea kuimarisha mikakati ya upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi na utekelezaji wa masuala ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Februari 2022. Jumla ya maazimio matano yaliyoelekezwa katika Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kati maazimio matano yaliyotolewa, maazimio matatu utekelezaji wake unaridhisha. Maazimio mawili yanayohusu Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nchini utekelezaji wake bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imejulishwa kuwa fedha za maendeleo zimepangwa kutengwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Aidha, maazimio mengine matatu yanayohusu mafunzo na elimu utekelezaji wake nao unaridhisha na ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Desemba 2022), Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shiingi bilioni 11.9 ambazo zote ni kwa ajili matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kufikia Desemba 2022, mamlaka imepokea kiasi cha shilingi bilioni 5.3 sawa na asilimia 44.8 ya bajeti iliyoidhinishwa, kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba mbili. Ni rai ya Kamati kuwa fedha zote zilizopangwa kwa mamlaka hii zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hali ya magonjwa ya akili yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya; kuna mahusiano ya karibu kati ya magonjwa ya akili na matumizi ya dawa za kulevya na vilevi vingine. Magonjwa ya akili yanaweza kusababisha matumizi ya dawa za kulevya, wakati huo huo matumizi ya dawa za kulevya yanaweza kusababisha kutokea kwa magonjwa ya akili. Kutokana na mahusiano hayo, waraibu wengi wa dawa za kulevya pia wanakabiliwa na magonjwa ya akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa hatua mbalimbali ambazo Serikali inachukua kukabiliana na magonjwa ya akili na uraibu wa dawa za kulevya. Hata hivyo Kamati imebaini changamoto mbili zifuatazo: -

i. Uwepo wa magonjwa mengine licha ya uraibu wa dawa za kulevya miongoni mwa waraibu wa dawa za kulevya kama vile UKIMWI, magonjwa ya akili na magonjwa yasiyoambukiza, na hivyo kuathiri matibabu; na

ii. Uwepo wa mahitaji mengine ya kijamii kwa waraibu na wagonjwa wa akili nchini kama vile mahitaji ya kisheria, elimu, ajira, chakula na malazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Wizara ya Afya, utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022; Kamati

ilitoa maoni mawili ambayo yaliazimiwa na Bunge ambayo yanahusu Kifua Kikuu na magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa utekelezaji wa azimio la Kifua Kikuu unaridhisha. Aidha, kwa azimio la magonjwa yasiyoambukiza Kamati haijaridhishwa. Ipo haja ya kuanzisha tume maalum ya kuratibu masuala ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Serikali katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza; magonjwa yasiyoambukiza yamekuwa yakiongezeka nchini na inakadiriwa kuwa asilimia 26 ya watu wazima wana Shinikizo la Juu la Damu, asimilia 9 wana tatizo la Kisukari na kuna visa vipya vya Saratani vipatavyo 42,000 kila mwaka. Aidha, asilimia 33 ya vifo vyote vilivyotokea nchini mwaka 2018 vilisababishwa na magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mikakati ambayo Serikali imeweka katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza, bado takwimu za MTUHA zinaonesha kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa kwa asilimia 9.4 kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa kuanzisha chombo maalum cha kuratibu mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza na kiwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya uratibu mzuri wa sekta zote zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hatua iliyofikiwa katika kuhuisha na kujumuisha masuala ya UKIMWI kwenye taasisi na sekta zote ambazo zina mazingira yenye vichochezi vikuu vya UKIMWI zikiwemo ujenzi, uchukuzi, uvuvi na madini; Sheria ya UKIMWI ya Mwaka 2008 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, Sura ya Tatu inaelekeza kuhuisha na kujumuisha huduma za VVU na UKIMWI mahala pa kazi kwa Wizara, taasisi na sekta zote ambazo zina mazingira yenye vichochezi vikuu vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi inayofanywa na Wizara katika kujumuisha masuala haya katika Sekta husika, Kamati imebaini upatikanaji mdogo wa fedha za ndani kwa ajili ya mwitikio wa UKIMWI; baadhi ya taasisi za Umma hazizingatii ipasavyo matakwa ya Sera na Sheria ya UKIMWI katika kutekeleza afua za UKIMWI mahali pa kazi pamoja na kutengewa fedha; na utoaji wa chakula lishe katika Gereza la Isanga, Dodoma kwa ajili ya mahabusu na wafungwa wanaoishi na VVU.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa, magereza yote nchini yana jumla ya wafungwa na mahabusu waliogundulika kuwa na VVU waliopo kwenye dawa wapatao 888. Aidha, katika Gereza la Isanga wafungwa na mahabusu wanaotumia dawa ni 53. Afua mbalimbali zimekuwa zikitolewa kwa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mikakati hii, Kamati imebaini kuwa lishe inayotolewa haitoshelezi mahitaji ya wafungwa WAVIU na hii ni kutokana na bajeti ndogo inayotengwa, lakini pia

magereza haziwekezi katika kilimo na ufugaji ili kuweza kujitosheleza katika mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; huduma zinazotolewa kwa vijana wanaoishi na VVU/UKIMWI walioko katika Kambi za JKT kwa mujibu wa sheria; Jeshi la Kujenga Taifa hupokea vijana ambao wamehitimu kidato cha sita kwa ajili ya mafunzo bila kujali hali ya afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2021, Jeshi la Kujenga Taifa limechukua vijana kwa mujibu wa sheria na hali yao ya maambukizi ni kama inavyoonekana kwenye taarifa. Aidha, Kamati imebaini kuwa bado elimu kuhusu umuhimu wa kujua afya ni ndogo, lakini pia fedha za utekelezaji wa afua ya UKIMWI hazitoshelezi mahitaji. Kamati inaona kuna haja ya kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kupima na namna ya kujikinga na maambukizi mapya kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati, Tume ya Kudhibiti UKIMWI:-

a) Upatikanaji wa Fedha za ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI: -

Kwa kuwa, fedha za ndani zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa afua za UKIMWI hazitoshelezi mahitaji kulingana na ukubwa wa tatizo na vile vile hazitolewi kwa wakati;

Na kwa kuwa, kuendelea kutegemea fedha kutoka kwa wafadhili wa nje haitoi uhahika wa mapambano endelevu dhidi ya maambukizi ya VVU na Ugonjwa wa UKIMWI ambayo yanahitaji rasilimali fedha za uhakika na za kutosha;

Na kwa kuwa, Utekelezaji duni wa afua za UKIMWI unasababisha kuendelea kuchochea maambukizi;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali: -

i. Kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa afua hii ya UKIMWI;

ii. Wizara ya Fedha ihakikishe fedha zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa afua za UKIMWI zinatolewa kwa wakati ili kunusuru afya za wananchi; na

iii. Mpango mkakati wa kupata vyanzo vingine vya ndani vya mapato uwekwe kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(c) Ongezeko la Maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI:

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko la Maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI kwa baadhi ya mikoa kama vile Mikoa ya Geita na Mwanza;

Na kwa kuwa ongezeko hilo la maambukizi linasababisha Taifa kupoteza nguvu kazi na

kuongeza gharama na mzigo kwa Taifa wa manunuzi ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI;

Kwa hiyo basi Kamati inaishauri Mamlaka husika kuweka mikakati ya kutoa elimu na afua mbalimbali katika mikoa hii ili kupunguza maambukizi mapya.

(c) Ukosefu wa Elimu ya UKIMWI katika Maeneo ya Mialo:

Kwa kuwa katika maeneo mengi ya mialo wananchi hawana elimu ya kutosha kuhusu UKIMWI;

Na kwa kuwa ukosefu huo wa elimu unasababisha wananchi kuwa na mwitikio mdogo wa upimaji wa VVU, matumizi hafifu ya kondomu, kushindwa kuchukua hatua ya kujikinga na hivyo kuchochea ongezeko la maambukizi ya VVU;

Kwa hiyo basi Mamlaka husika zitoe kipaumbele katika maeneo haya kwa kuhakikisha afua zote ikiwemo kutoa elimu itakayosaidia kupunguza maambukizi.

(d) Utekelezaji wa Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (*NMSF* 2018/2019 – 2022/2023);

Kwa kuwa malengo ya utekelezaji wa malengo ya Mkakati huu ambayo ni kupunguza maambukizi mapya ya VVU, maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto, idadi ya vifo vinavyotokana na UKIMWI, unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya WAVIU yanapaswa kufikiwa Mwaka huu wa 2023;

Na kwa kuwa maambukizi mapya ya VVU, maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto, idadi ya vifo vinavyotokana na UKIMWI na unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya WAVIU miongoni mwa jamii bado vyote vipo juu;

Kwa hiyo basi Serikali ihakikishe inaweka mkazo zaidi ili kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya VVU, maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto na vifo vitokanavyo na UKIMWI. Aidha, elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu kupunguza unyanyapaa.

(e) Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza:

Kwa kuwa bado wananchi wengi hawana uelewa juu ya namna ya kujikinga na athari kubwa za magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza;

Na kwa kuwa asilimia kubwa ya mgonjwa haya yamekuwa ni tishio kwa afya za Watanzania wengi kwani yamekuwa yanachangia takribani asilimia 33 ya vifo vyote nchini ambapo Tatizo la shinikizo la juu la damu ni chanzo kikuu cha pili cha vifo kwa watu wote wenye umri zaidi ya miaka 50 hapa nchini;

Na kwa kuwa magonjwa haya yanaligharimu Taifa fedha nyingi kutokana na gharama kubwa na ni miongoni mwa sababu kubwa ya kurudisha nyuma uchumi wa mtu mmoja, familia na Taifa kwa ujumla. Tathmini za haraka za matibabu zilizofanywa na Chama cha Kisukari nchini ili kutambua gharama ilibainika kuwa zaidi ya Shilingi bilioni 290 zinahitajika kwa mwaka kama gharama za dawa kwa wagonjwa milioni 1.5 ya watu wenye kisukari na

shinikizo la juu la damu pekee. Gharama hizi ni karibu sawa na asilimia 20 ya bajeti ya Wizara ya Afya.

Hivyo basi Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Mkazo wa elimu uendelee kutolewa kwa jamii ili kufahamu sababu na madhara yanayotokana na magonjwa haya pamoja na umuhimu wa kujikinga; na

(ii) Michezo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ikiwemo kukimbia mchakamchaka virudishwe kama ilivyokuwa zamani ili kuwajenga kiafya na kiakili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ugonjwa wa Kifua Kikuu:

Kwa kuwa bado kuna kiwango kikubwa cha wagonjwa wa Kifua Kikuu katika baadhi ya Mikoa ambacho kinachochewa na masuala mbalimbali kama vile msongamano wa watu, wafungwa na mahabusu katika magereza; upungufu wa vifaa kama mashine za *X-Ray*, makopo au vifaa vya kuchukulia sampuli za makohozi na vitendanishi vya maabara;

Na kwa kuwa ipo hatari ya kuongezeka kwa wagonjwa wengi na vifo na hivyo kupunguza nguvu kazi ya Taifa, lakini pia kuongeza mzigo wa kugharimia matibabu;

Hivyo basi Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kununua vifaa kama *X-ray machines,* makopo

ya sampuli na ujenzi wa magereza ili kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; Sera ya Taifa ya kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya nchini.

Kwa kuwa mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini umechukua muda mrefu na haujakamilika;

Na kwa kuwa kukosekana na kuendelea kuchelewa kwa Sera hii kunaweza kupelekea kukosa mwongozo sahihi katika vita dhidi ya dawa za kulevya kwa ujumla wake;

Na kwa kuwa Kamati inatambua mchakato wa utungwaji wa Sera hiyo kwa sasa upo katika hatua ya kupata maoni ya wadau;

Hivyo basi Kamati inaishauri Serikali iharakishe mchakato huu ili kuwezesha Mamlaka kuwa na mwongozo sahihi ambao utasaidia kulinusuru Taifa na janga hili la matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umuhimu wa Serikali kutenga bajeti ya Mipango ya Maendeleo;

Kwa kuwa bado Mamlaka haitengewi fedha za utekelezaji wa mipango ya maendeleo;

Na kwa kuwa kukosekana kwa fedha za maendeleo kunapelekea Mamlaka kushindwa kuwasaidia Waraibu wa Dawa za Kulevya ambao wengi ni vijana pamoja na kushindwa kununua vifaa muhimu vya udhibiti wa dawa za kulevya nchini;

Hivyo basi Serikali itenge fedha za kutosha ili kuwezesha Mamlaka:-

(i) Kuanzisha miradi itakayowasaidia waraibu wa dawa za kulevya ili wasiweze kurudi katika matumizi ya dawa za kulevya; na

(ii) Kuboresha miundombinu ya udhibiti wa dawa za kulevya kwa mfano, ununuzi wa boti na mashine za ukaguzi katika viwanja vyetu vya ndege, bandari na kwenye mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne, Hitimisho; nakushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi *(ndc)* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Namshukuru sana Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein *(ndc);* Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Magili; Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Happiness Ndalu, Ndugu Asia Msangi na Ndugu Pamela Pallangyo na Msaidizi wa Kamati

Ndugu Catherine Kitutu kwa kuratibu vizuri shughuli zote za Kamati wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu) Mhe. George Boniphace Simbachawene na Manaibu Mawaziri Mheshimiwa Ummy Khamis Nderiananga na Mheshimiwa Patrobas Katambi kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Namshukuru pia Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Godwin O. Mollel kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati wote walipohitajika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Pamoja nao Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hizi mbili ambao ni Dkt. John Jingu na Profesa Abel Makubi pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko; Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kamishna Jenerali Gerald Kusaya; na Watendaji wote wa Wizara, Tume na Mamlaka kwa ushirikiano wanaoipatia na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali wakati wa vikao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa umakini na kujitoa kwao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo. Majina yao yaingizwe katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haya, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako lipokee, lijadili na kuikubali taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2022 HADI JANUARI, 2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka kuhusu majukumu na shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023. Taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu (3) kama inavyoelekezwa katika masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Sehemu ya Kwanza

inahusu utangulizi ambapo inafafanua muundo, majukumu pamoja na maelezo ya jumla kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati. Sehemu ya Pili inazungumzia uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati na Sehemu ya Tatu Kamati imetoa mapendekezo na hitimisho.

### 1.1. Muundo na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Tatu, Kanuni ya 10 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Taasisi mbili ambazo ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya *(DCEA)*.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni hii imeipa Kamati majukumu yafuatayo:-

a) kusimamia utekelezaji wa masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;

b) kusimamia shughuli zote za Serikali za kudhibiti na kutokomeza ugonjwa wa kifua kikuu;

c) kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI, kifua kikuu na udhibiti wa dawa za kulevya;

d) kujadili hatua za kudhibiti UKIMWI, kifua kikuu na dawa za kulevya;

e) kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; na

f) Kushughulikia Magonjwa Yasiyoambukiza ambayo yanachangia vifo vingi sana kwa wananchi kwa kukosa ufahamu juu ya magonjwa haya pamoja na kutokufanya mazoezi na kutokuwa na desturi ya kupima afya mara kwa mara.

**1.2. Njia na mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni, Katiba lakini pia ustawi wa wananchi, njia na mbinu zifuatazo zilitumika katika kutekeleza majukumu hayo ya Kamati:-

a) Vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi mbalimbali kwa lengo la kufahamu utendaji kazi lakini pia kufahamu mafanikio na changamoto;

b) Ziara za kukagua shughuli zinazotekelezwa katika kushughulikia masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevya na Magonjwa Yasiyoambukiza ili kujiridhisha katika hatua zilizofikiwa katika utekelezaji; na

c) Kushiriki semina, warsha na makongamano mbalimbali kuhusiana na Masuala ya UKIMWI,

Kifua Kikuu, Dawa za Kulevya na Magonjwa Yasiyoambukiza kwa lengo la kujengewa uelewa.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023 Kamati imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Ziara katika maeneo mbalimbali yanayojihusisha na mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevya kwa lengo la kujifunza na kuona ili kuweza kutoa ushauri kuhusiana na maeneo hayo;

(b) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(c) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba 2022);

(d) Kupokea na Kuchambua Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kuhusu hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Maazimio ya

Bunge kutokana na Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022; na

(e) Kupokea, Kuchambua na Kujadili Taarifa mbalimbali kutoka Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na Wizara mbalimbali kuhusu utekelezaji wa afua za UKIMWI na udhibiti wa dawa za Kulevya.

**2.1 Ziara zilizofanywa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika vipindi tofauti Kamati ilifanya Ziara kwa lengo la kuona, kujifunza na kukagua utekelezaji wa afua ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevya zinazotekelezwa na Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali. Itakumbukwa kuwa utekelezaji wa shughuli hizi ni mwitikio wa mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu pamoja na biashara na matumizi ya Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, Ziara hizo zilifanyika katika Mkoa wa Geita, Mara, Mwanza na Morogoro ambapo Kamati ilitembelea maeneo ya migodi, vituo vinavyotoa huduma ya CTC, magerezani, vituo vinavyotoa huduma ya methadone kwa waraibu, konga za WAVIU, mialo ya wavuvi wa samaki pamoja na wanufaika wa Mradi wa Timiza Malengo.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara Kamati ilipata fursa ya kuona na kukagua utekelezaji wa afua mbalimbali. Aidha, Kamati ilibaini masuala yafuatayo:-

**a) Ongezeko la Maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI**

Hali ya Maambukizi ya VVU bado ipo juu kwa Mkoa wa Geita **(asilimia 6.4)** na Mkoa wa Mwanza imeongezeka kutoka **asilimia 4.7** mwaka 2011/2012 hadi **asilimia 5** mwaka 2016/2017 ukilinganisha na hali ya maambukizi Kitaifa ya **asilimia 4.7. Kamati inaona ipo haja ya Mamlaka husika kuweka nguvu zaidi katika Mikoa hii pamoja na mikoa mingine ambayo maambukizi yanaongezeka ili kupunguza maambukizi mapya.**

**b) Ukosefu wa Elimu kuhusu UKIMWI katika Maeneo ya Mialo**

Katika baadhi ya mialo ambayo Kamati iliitembelea elimu kuhusu UKIMWI bado haijawafikia ipasavyo na hivyo watu wengi hawachukui tahadhari ya kujikinga na maradhi haya. Ukosefu wa elimu umekuwa ukisababisha mwitikio mdogo wa upimaji wa VVU katika mialo na kambi za wavuvi na matumizi hafifu ya Kondomu. **Kamati inaziomba Mamlaka husika kuhakikisha zinatoa elimu ya UKIMWI katika maeneo haya na si kusubiri ujio wa Kamati ya Bunge ndipo watembelee maeneo husika.**

**c) Ugonjwa wa Kifua Kikuu**

Ugonjwa wa Kifua Kifuu bado ni changamoto kwa Taifa letu kutokana na yaliyobainika wakati wa Ziara kama ifautavyo:-

i) Kiwango kikubwa cha wagonjwa wa Kifua Kikuu katika Mkoa wa Mara kwani katika Mwaka 2021 kati ya **watu 100,000 waliopimwa watu 146** waligundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu (Chanzo: *District Health Information Software 2 - DHIS2-ETL)* na Mkoa wa Mwanza kati ya **watu 100,000 waliopimwa watu 145** ni wagonjwa wa Kifua Kikuu**;**

ii) Upungufu wa mashine za X- Ray;

iii) Ukosefu wa makopo au vifaa vya kuchukulia sampuli za makohozi na vitendanishi vya maabara;

iv) Ukosefu wa fedha za kuwahudumia wagonjwa wa Kifua Kikuu; na

v) Msongamano wa wafungwa na mahabusu ambao kwa kiasi kikubwa umekuwa unachangia maambukizi kuenea kwa kasi.

**Ni rai ya Kamati kuwa changamoto hizi zifanyiwe kazi ili kupunguza maambukizi ya Kifua Kikuu nchini. Aidha, kampeni mbalimbali za uhamasishaji na upimaji wa TB na VVU katika msongamano wa watu na sehemu hatarishi ziendelee nchi nzima. Kwa kufanya hivi watu wengi watapata uelewa kuhusu ugonjwa huu na athari zake kwa jamii.**

### d) Ukosefu wa Lishe katika Magereza

Lishe ni kitu muhimu kwa Waathirika wa Virusi vya UKIMWI kwani inawasaidia kuweka afya vizuri

wanapokuwa wanatumia dawa za kufubaza virusi *(ARVs)*. Kamati imebaini ya kwamba wafungwa na mahabusu wanapewa chakula cha aina moja tu ambacho ni ugali na maharagwe kila siku hali ambayo inafanya wazidi kudhoofika kiafya kwani dawa wanazotumia ni kali na zina nguvu sana. **Ipo haja sasa ya Serikali kuhakikisha lishe bora inatolewa kwa WAVIU waliopo magerezani.**

**e) Wafungwa na mahabusu kujilipia gharama za matibabu**

Kamati ilielezwa uwepo wa changamoto ya Magereza kudaiwa kulipia gharama za matibabu inapotokea wafungwa na mahabusu wanapokwenda kupata matibabu katika vituo vya afya. **Kamati inaona jambo hili siyo sahihi hivyo Mamlaka husika zichukue hatua na wafungwa wote wapatiwe huduma ya bima ya afya itakayowasaidia pindi wanapopata maradhi.**

**f) Magonjwa Yasiyoambukiza**

Magonjwa Yasiyoambukiza yanaendelea kulitikisa Taifa hivi sasa. Kamati imebaini kuwa wapo wananchi wa kawaida, wafungwa na mahabusu wanaokabiliwa na magonjwa kama kisukari, kansa, shinikizo la damu, moyo na mengineyo. Sababu kubwa za magonjwa haya ni miili kukosa mazoezi, ulaji usiofaa na msongo wa mawazo. **Elimu zaidi kuhusu magonjwa yasiyoambukiza inahitajika katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vya elimu ya juu. Serikali kwa kushirikiana na sekta husika wahakikishe elimu ya kutosha inatolewa kwa**

**jamii juu ya umuhimu wa vyakula visivyofaa na kufanya mazoezi**.

**g) Walengwa wa Mradi wa Timiza Malengo**

Kamati imebaini kuwa Mradi wa Timiza Malengo ambao unelenga kuwafikia Wasichana Balehe na Wanawake Vijana kwa afua mbalimbali umekuwa na changamoto kutokana na walengwa wengi wa Mradi kukosa viambatisho muhimu vinavyohitajika wakati wa kufungua akaunti ambavyo ni Kitambulisho cha Taifa (NIDA) na Cheti cha Kuzaliwa (RITA); na mahitaji ya walengwa ni makubwa kuliko rasilimali zilizopo na hivyo kushindwa kuwafikia wahitaji wengi.

**2.2 Uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa mbalimbali kutoka TACAIDS kama ifuatavyo:-

**a) Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, mara baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (**Fungu 92**) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; pamoja na makadirio ya mapato na

matumizi ya mafungu hayo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao hivyo, Kamati ilipata wasaa mzuri wa kuchambua, kuhoji na kujadili utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, Kamati ilipata wasaa wa kuchambua, kuhoji, kujadili na hatimaye kutoa maoni, ushauri na mapendekezo muhimu kwa mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za kina za uchambuzi wa Bajeti ya Tume **(Fungu 92)** pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yaliwasilishwa katika Mkutano wa Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muhtasari katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI **(Fungu 92)** imeongezeka kwa **asilimia 29** kutoka **Shilingi 4,317,818,000.00** mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 14,981,224,000** mwaka 2022/2023. Ongezeko zaidi ni kwenye fedha za Maendeleo za nje kwa **asilimia 81** na fedha za maendeleo za ndani kwa **asilimia 47. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwenye miradi ya maendeleo na kusisitiza kuwa fedha hizi zitolewe kwa wakati ili shughuli zilizokusudiwa ziweze kutekelezwa kikamilifu.**

**b) Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2022)**

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Mwezi Januari, 2023, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai hadi Disemba, 2022) ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) – Fungu 92.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania – TACAIDS (Fungu 92) iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 14,981,224,000**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 2,979,018,000.00** ni za Matumizi ya Kawaida zinazojumuisha Mishahara **Shilingi 1,766,272,000.00** na **Shilingi 1,212,746,000.00** za Matumizi Mengineyo. Aidha, **Shilingi 12,002,206,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo ambazo zinajumuisha **Shilingi 1,880,000,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 10,122,206,000.00** fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kufikia Disemba, 2022, Tume imepokea kiasi cha **Shilingi 5,627,972,000.00** sawa na **asilimia 37.6** tu ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha hizo zinajumuisha Mishahara **Shilingi 818,008,500.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 425,056,000.00.** Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 4,384,907,500.00**, kati ya fedha hizo **Shilingi 939,992,000.00** ni fedha za ndani kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI na **Shilingi 3,444,915,500.00** ni fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji huo wa fedha umewezesha Tume kutekeleza majukumu mbalimbali

iliyojiwekea ambayo Kamati ilipata fursa ya kuyapitia ambayo bado utekelezaji wake unaendelea. Hata hivyo, **Kamati haijaridhishwa na utolewaji wa fedha hizi hususan za Matumizi mengineyo na Miradi ya Maendeleo ambazo kwa utaratibu zilipaswa kuwa zimetolewa kwa asilimia 50 kufikia Disemba, 2022.**

**KIELELEZO NA.1 : UPATIKANAJI WA FEDHA KWA KIPINDI CHA JULAI - DISEMBA, 2022 (TUME YA KUDHIBITI UKIMWI FUNGU 92)**




| | MISHAHARA | OC | Maendeleo | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| KILICHOIDHINISHWA | 1,766,272,000 | 1,212,746,000 | 12,002,206,000 | 14,981,224,000 |
| KILICHOPOKELEWA | 818,008,500 | 425,056,000 | 4,384,907,500 | 5,627,972,000 |
| ASILIMIA | 46.3 | 35.0 | 36.5 | 37.6 |

**Chanzo: Taarifa ya TACAIDS na usanifu wa Kamati**

**c) Hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Januari, 2022**

**Mheshimiwa Spika**, katika vipindi tofauti Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kuhusu hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Januari, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya Maazimio 10 yaliyotolewa kwa Wizara hii Maazimio 5 yalielekezwa katika Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini (TACAIDS). Uchambuzi wa Kamati wa Taarifa ya mwisho ya utekelezaji wa Maazimio haya ambayo ilipokelewa na kuchambuliwa na Kamati mwezi Januari, 2023 inaonesha kuwa, utekelezaji wa Maazimio yote matano (5) unaridhisha. Maazimio matatu (3) yanayohusu bajeti (fedha) utekelezaji wake unaonekana dhahiri kwani bajeti imeongezeka kwa kiasi ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Aidha, maazimio mengine mawili (2) yanayohusu utoaji wa elimu utekelezaji wake ni endelevu. **Kamati inaendelea kusisitiza masuala hayo katika Taarifa hii.**

**d) Kupokea na kujadili Taarifa kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF 2018/2019 – 2022/2023)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Nne wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF IV). Mkakati huu ambao uliandaliwa kuwezesha utekelezaji wa Mwitikio Shirikishi wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI nchini unaunganisha mipango kazi ya wadau wa UKIMWI ili kuchangia katika kufikia malengo tuliyojiwekea. Aidha, Mkakati huu ni zana ya TACAIDS na wadau wa maendeleo katika kufuatilia utekelezaji wa mwitikio wa UKIMWI kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Mkakati huu ambao malengo yake ni pamoja na kupunguza idadi ya maambukizi mapya kutoka 81,000 (mwaka 2017) hadi 27,500 (mwaka 2023); Kutokomeza maambukizi kutoka kwa

mama kwenda kwa mtoto hadi kufikia chini ya **asilimia 5** mwaka 2023 kutoka asilimia 7.6 (mwaka 2017); Kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na UKIMWI kutoka vifo 33,800 (mwaka 2017) hadi vifo 32,000 (mwaka 2023); na Kutokomeza unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya WAVIU ifikapo 2023 utekelezaji wake umekuwa na mafanikio.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa ya hatua iliyofikiwa, hata hivyo, Kamati imebaini masuala yafuatayo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi:-

i) Mkazo zaidi unahitajika kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya VVU na vifo vitokanavyo na UKIMWI;

ii) Kunahitajika jitihada zaidi ili watu wengi waweze kujua hali zao za maambukizi kwani 95 ya kwanza bado ipo chini;

iii) Ipo haja ya kuendelea kuimarisha mikakati ya upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za UKIMWI; na

iv) Ipo haja ya kuongeza nguvu zaidi katika kuyafikia makundi mbalimbali hasa vijana, wanaume, watoto na makundi maalum.

### 2.3 Uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023, Kamati imepata wasaa wa kukutana,

kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa mbalimbali kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kama ifuatavyo:-

**a) Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vya Kamati vilivyofanyika kuanzia mwezi Machi, 2022, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (**Fungu 91**) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Taarifa ya kina kuhusu bajeti hii iliwasilishwa katika mkutano wa bajeti uliomalizika mwezi Juni, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muhtasari Kamati ilibaini kuwa Bajeti imeongezeka kwa **asilimia 40.39** kutoka **Shilingi 8,529,797,000** mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 11,974,701,000.** Ongezeko zaidi ni kwenye Matumizi Mengineyo (OC) kwa **asilimia 59.7** na hususan Kasma 31121 ya Vyombo vya Usafiri kutoka **Shilingi 1,000,000.00** hadi **Shilingi 660,000,000.00** na Kasma 31122 ya Mashine na Vifaa visivyo vya usafiri kama vifaa vya kisayansi vya utambuzi wa dawa za kulevya kutoka **Shilingi 187,650,000.00** Mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 411,049,000.00** Mwaka 2022/2023. ***Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Mamlaka. Ni rai ya Kamati kuwa fedha hizi zitumike kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa na pia ihakikishe kuwa fedha hizi zinatoka kwa wakati.***

**b) Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2022)**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shiingi 11,974,701,000.00** ambazo zote ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zinajumuisha Mishahara **Shilingi 2,127,286,000.00** sawa na **asilimia 18** ya bajeti na Matumizi Mengineyo **Shilingi 9,847,415,000.00** sawa na **asilimia 82** ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kufikia Disemba 2022, Mamlaka imepokea kiasi cha **Shilingi 5,358,890,614.13** sawa na **asilimia 44.8** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi 1,063,643,000.00** sawa na **asilimia 50** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 4,295,247,614.00** sawa na **asilimia 44** ya Bajeti iliyoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

**Mheshimiwa Spika**, fedha hizo zilizopokelewa zimetumika kutekeleza kazi mbalimbali za Mamlaka ilizojipangia ambazo Kamati ilielezwa na kuzichambua. **Ni rai ya Kamati kuwa fedha zote zilizopangwa kwa Mamlaka hii zitolewe zote kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

**KIELELEZO NA. 2: UPATIKANAJI WA FEDHA KWA KIPINDI CHA JULAI - DISEMBA, 2022 (MAMLAKA YA KUDHIBITI DAWA ZA KULEVYA FUNGU 91)**




**Chanzo: Taarifa ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Usanifu wa Kamati**

**c) Hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022 ilitoa Maoni mbalimbali ambayo yaliazimiwa na Bunge lako Tukufu. Jumla ya Maazimio matano (5) yalielekezwa katika Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Januari, 2023, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Maazimio hayo na kubaini kuwa kati ya Maazimio 5 yaliyotolewa, Maazimio (3) utekelezaji wake unaridhisha. Maazimio mawili (2) yanayohusu Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za

Kulevya Nchini utekelezaji wake bado unaendelea. Kamati imejulishwa kuwa fedha za maedeleo zimepangwa kutengwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 hivyo basi Kamati inaendelea kusisitiza katika Taarifa hii kuhusu utengaji wa fedha hizo. Maazimio mengine matatu yanoyohusu mafunzo na elimu utekelezaji wake nao unaridhisha na ni endelevu.

**d) Kupokea na kujadili Taarifa kuhusu hali ya Magonjwa ya akili yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya na hatua zinazochukuliwa ili kupunguza tatizo hilo**

**Mheshimiwa Spika**, kuna mahusiano ya karibu kati ya magonjwa ya akili na matumizi ya dawa za kulevya na vilevi vingine. Magonjwa ya akili yanaweza kusababisha matumizi ya dawa za kulevya wakati huo huo matumizi ya dawa za kulevya yanaweza kusababisha kutokea kwa magonjwa ya akili. Kutokana na mahusiano hayo, waraibu wengi wa dawa za kulevya pia wanakabiliwa na magonjwa ya akili.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati kuhusu taarifa hii umebaini kuwa zipo sababu mbalimbali zinazopelekea kutokea kwa magonjwa ya akili na dawa za kulevya. Sababu hizo ni pamoja na uwepo wa vinasaba (*genetics*), sababu za kibailojia (*biological*), sababu za kijamii (*social*) na kisaikolojia (*psychological*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa hatua mbalimbali ambazo Serikali inachukua kukabiliana

na Magonjwa ya Akili na Uraibu wa Dawa za Kulevya. Hata hivyo Kamati imebaini changamoto mbili zifuatazo:-

i) Uwepo wa magonjwa mengine licha ya uraibu wa dawa za kulevya miongoni mwa waraibu wa dawa za kulevya kama vile UKIMWI, magonjwa ya akili na magonjwa *yasiyoambukiza (Non Communicable Diseases - NCDs)* na hivyo kuathiri matibabu; na

ii) Uwepo wa mahitaji mengine ya kijamii kwa waraibu na wagonjwa wa akili nchini kama vile mahitaji ya kisheria, elimu, ajira, chakula na malazi.

### 2.4 Wizara ya Afya

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023, Kamati ilipata wasaa wa kukutana na Wizara ya Afya na kupokea taarifa mbalimbali kama ifuatavyo:-

**a) Hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022**

**Mheshimiwa Spika,** katika Taarifa ya Mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni Mwezi Februari, 2022, Kamati ilitoa maoni mawili (2) ambayo yaliazimiwa na Bunge ambayo yanahusu Kifua Kikuu na Magonjwa Yasiyoambukiza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa maazimio na kubaini kuwa utekelezaji wa Azimio la Kifua Kikuu unaridhisha. Aidha, kwa Azimio la Magonjwa Yasiyoambukiza Kamati inaona pamoja na jitihada ambazo Serikali imechukua lakini bado suala la kuanzisha Tume Maalum itakayoratibu masuala ya Magonjwa Yasiyoambukiza utekelezaji wake hauridhishi. Kamati inaendelea kulisisitiza suala hili kwenye Taarifa hii.

**b) Mkakati wa Serikali katika kukabiliana na Magonjwa yasiyoambukiza**

**Mheshimiwa Spika**, Magonjwa yasiyoambukiza (MYA) yamekuwa yakiongezeka nchini na inakadiriwa kuwa **asilimia 26** ya watu wazima wana shinikizo la juu la damu, **asimilia 9** wana tatizo la sukari (*diabetes)* na kuna visa vipya vya saratani vipatavyo **42,000** kila mwaka. Aidha, **asilimia 33** ya vifo vyote vilivyotokea nchini mwaka 2018 vilisababishwa na Magonjwa Yasiyoambukiza.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hii na katika kuhakikisha kunakuwa na kasi ya udhibiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza, Serikali ilizindua Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magojwa Yasiyoambukiza *(TaNCDA)* Mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Mikakati ambayo Serikali imeweka katika kukabiliana na Magonjwa Yasiyoambukiza, bado takwimu za MTUHA zinaonesha kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa kutoka jumla ya **wagonjwa 2,535,281** waliotibiwa kwa Mwaka 2017 na kufikia **wagonjwa**

**3,440,708** mwaka 2021, sawa na ongezeko la **asilimia 9.4** la **wagonjwa 905,427** ndani ya kipindi cha miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo:-

i) Upatikanaji wa dawa za Magonjwa Yasiyoambukiza katika Vituo vya kutolea huduma za afya bado ni changamoto;

ii) Elimu kuhusu namna ya kujikinga na Magonjwa Yasiyoambukiza inapaswa kuingizwa kwenye mitaala kuanzia elimu ya msingi hadi Vyuo Vikuu na itolewe katika maeneo yote ya mjini na vijijini;

iii) Kuna umuhimu wa kuanzisha chombo maalum cha kuratibu mapambano dhidi ya Magonjwa Yasiyoambukiza na kiwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya uratibu mzuri wa Sekta zote zinazohusika; na

iv) Bajeti ndogo isiyotosheleza gharama kubwa za matibabu ya Magonjwa Yasiyoambukiza.

**c) Udhibiti wa maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI kwa Wananchi waliohamishwa katika Kijiji cha Msomera, Kata ya Misima, Wilaya ya Handeni kutoka eneo la Hifadhi ya Ngorongoro**

**Mheshimiwa Spika,** Kijiji cha Msomera kina Zahanati moja ambayo inatoa huduma za kinga pamoja na matibabu kwa wale wanaogundulika na magonjwa. Katika kukabiliana na maambukizi mapya ya

VVU/UKIMWI kutokana na kuhamishiwa kwa wananchi katika Kijiji hiki, Kamati ilielezwa jitihada mbazo Serikali imefanya kuwa ni pamoja na:-

i) Kusambaza Kondomu katika ngazi ya jamii inayoizunguka. Aidha, Wizara imetenga makasha ya kondomu yapatayo 50 ambayo yatapelekwa na kufungwa katika viijiji vinne maeneo ya kimkakati kwa kila kata ndani ya mwezi mmoja;

ii) Wizara kwa kushirikiana na mdau wa AMREF imechapisha vipeperushi na kuvisambaza katika mkoa mzima wa Tanga vikiwemo vya VVU na UKIMWI, UVIKO 19 na ebola; na

iii) Huduma za upimaji wa VVU zinatolewa kwa hiari na bila malipo katika Zahanati ya Msomera na kupitia huduma mkoba.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada hizo zinazofanywa na Serikali, Kamati imebaini kuwa miundombinu kama vituo vya afya bado ni vichache na kuna upungufu wa wahudumu wa afya wanaosaidia kuhudumia WAVIU na wagonjwa wengine.

**d) Hatua iliyofikiwa katika kuhuisha na kujumuisha masuala ya UKIMWI *(Mainstreaming)* kwenye taasisi na sekta zote ambazo zina mazingira yenye vichochezi vikuu vya UKIMWI zikiwemo ujenzi, uchukuzi, uvuvi na madini**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya UKIMWI ya Mwaka 2008 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, Sura ya Tatu

*(PART III-Public Education and Programmes on HIV and AIDS)* inaelekeza kuhuisha na kujumuisha huduma za VVU na UKIMWI mahala pa kazi kwa Wizara, Taasisi na Sekta zote ambazo zina mazingira yenye vichochezi vikuu vya UKIMWI. Serikali imeandaa miongozo mbalimbali kwa lengo la kuhuisha na kujumuisha afua za VVU na UKIMWI katika sekta hizo. Miongozo hiyo ni pamoja na Mwongozo wa Kudhibiti UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukiza kwenye Sekta ya Uvuvi, Madini na Migodini, mwongozo wa kudhibiti UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Kitini cha Kufundishia Mwongozo wa Kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza Katika Utumishi wa Umma (2015) na Miongozo Elekezi ya Stadi za Kazi na Elimu ya Via vya Uzazi *(Comprehensive Sexual Education – CSE)* ambayo itajumuishwa katika mitaala ya Elimu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa namna ambavyo Wizara imekuwa ikiratibu afua za kinga, tiba na matunzo katika maeneo ya kazi. Aidha, katika maeneo yenye vichocheo vikubwa huduma zifuatazo zimekuwa zikitolewa:-

i) Maeneo ya Migodi huduma za VVU zinatolewa ikiwa ni pamoja na Upimaji wa VVU, huduma za Tiba na Matunzo ikiwemo utoaji wa ARVs, huduma za Tohara, huduma za JIPIME, huduma za dawa kinga *(PrEP)* na magonjwa mengine ya ngono;

ii) Maeneo ya Uvuvi huduma za VVU na UKIMWI katika vituo vya huduma za afya vilivyopo karibu

nao. Kwa upande wa visiwa huduma za VVU na UKIMWI kwa njia ya Huduma Mkoba ngazi ya jamii na baadhi ya maeneo kama visiwa vya Ziwa Victoria Mkoani Mwanza huduma hutolewa kwa kutumia usafiri wa boti maalum (Fikia boat);

iii) Maeneo ya ujenzi wa miradi mikubwa na midogo sambamba na utoaji wa elimu, ugawaji wa kondomu na huduma za upimaji. Huduma hizi kwa ujumla zimekuwa zikiwalenga wafanyakazi, wafanyabiashara na jamii inayozunguka maeneo ya miradi; na

iv) Kwa upande wa uchukuzi, zipo afua zinazowafikia madereva wa malori hasa wa masafa marefu ambapo hivi sasa kuna vituo 16 vinavyotoa huduma jumuishi katika njia kuu za usafirishaji.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi inayofanywa na Wizara katika kujumuisha masuala haya katika Sekta husika, Kamati imebaini yafuatayo:-

i) Mwitikio mdogo wa Sekta binafsi katika kutoa huduma za VVU na UKIMWI katika maeneo yao;

ii) Upatikanaji mdogo wa fedha za ndani kwa ajili ya mwitikio wa UKIMWI;

iii) Baadhi ya Taasisi za Umma hazizingatii ipasavyo matakwa ya Sera na Sheria ya UKIMWI katika kutekeleza Afua za UKIMWI mahali pa kazi pamoja na kutengewa fedha; na

iv) Watumishi wengi wa Umma hawapo tayari kupima maambukizi ya UKIMWI na kuweka wazi hali ya afya zao ili waweze kunufaika na huduma zinazotolewa kwa walioathirika.

### 2.5 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - utoaji wa chakula lishe katika Gereza la Isanga Dodoma kwa ajili ya mahabusu na wafungwa wanaoishi na VVU

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa kuhusu utoaji wa chakula lishe katika Gereza la Isanga Dodoma kwa ajili ya mahabusu na wafungwa wanaoishi na VVU kwa kuzingatia kauli ya Magereza Jihudumie.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa, Magereza yote nchini yana jumla ya wafungwa na mahabusu waliogundulika kuwa na VVU waliopo kwenye dawa wapatao 888. Aidha, katika Gereza la Isanga Wafungwa na Mahabusu wanaotumia dawa ni 53. Katika kukabiliana na magonjwa nyemelezi wafungwa na mahabusu wamekuwa wakipatiwa Tiba kwa kuzingatia mwongozo wa matibabu ya magonjwa nyemelezi. Baadhi ya Magonjwa hayo ni Kifua Kikuu (TB), magonjwa mbalimbali ya ngozi na vichomi (PCP). Dawa kinga za kifua Kikuu TPT zinaendelea kutolewa kwa wagonjwa wote ambao wamepimwa na kuthibitishwa kuwa hawana ugonjwa wa TB. Aidha, lishe nyingine kama mboga za majani na maziwa yamekuwa yakitolewa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mikakati hii, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa lishe

inayotolewa haitoshelezi mahitaji ya Wafungwa WAVIU na hii ni kutokana na bajeti ndogo inayotengwa lakini pia Magereza haziwekezi katika kilimo na ufugaji ili kuweza kujitosheleza katika mahitaji yao**.**

**2.6 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Huduma zinazotolewa kwa vijana wanaoishi na VVU/UKIMWI walioko katika Kambi za JKT kwa mujibu wa sheria**

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Kujenga Taifa hupokea Vijana ambao wamehitimu kidato cha sita. Vijana hao huripoti Makambini kwa ajili ya mafunzo bila kujali hali ya afya zao, wote hujumuishwa kuhudhuria mafunzo hayo, ingawa kabla ya kuanza mafunzo wote hulazimika kupimwa afya zao, wale ambao watagundulika kuwa wajawazito tu ndio hurejeshwa nyumbani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miaka mitatu, yaani kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2021, Jeshi la Kujenga Taifa limechukua vijana kwa mujibu wa sheria ambapo Mwaka 2019 vijana 20,413; Mwaka 2020 vijana 21,383 na Mwaka 2021 vijana 25,503. Hali ya maambukizi kwa vijana waliokuwa Makambini kwa mujibu wa sheria kwa miaka hiyo mitatu ni kama ifuatavyo: Mwaka 2019 kati ya vijana 20,413 waliopimwa vijana 60 walikutwa na maambuzi; mwaka 2020 kati ya vijana 21,383 waliopimwa vijana 45 walikutwa na maambukizi na mwaka 2021 kati ya vijana 25,503 waliopimwa vijana 42 walikutwa na maambukizi.

**Mheshimiwa Spika**, vijana wenye Virusi vya UKIMWI katika Jeshi la Kujenga Taifa wanapatiwa huduma mbalimbali kama vile ushauri nasaha kabla ya kupimwa VVU; Kupatiwa/kuanzishiwa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI *(ARV);* Kupatiwa vipimo muhimu kabla ya kuanza dawa na hata baada ya kuanza dawa vipimo kama vya figo *(Renal function test),* maini *(Liver function test)* na *CD4 Count* na *Viral load* (Wingi wa virusi kwenye damu) pamoja na kupimwa magonjwa nyemelezi kama Kifua Kikuu *(TB Screening),* Homa ya Uti wa mgongo ya fungus *(Cryptococal meningitis)* na kutibiwa magonjwa nyemelezi *(Optunistic infections)* endapo watakutwa nayo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na huduma hizo zinazotolewa na Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati imebaini kuwa bado elimu kuhusu umuhimu wa kujua afya ni mdogo lakini pia fedha za utekelezaji wa afua hazitoshelezi mahitaji. **Kamati inaona kuna haja ya kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kupima na namna ya kujikinga na maambukizi mapya kwa vijana.**

## 2.7 Semina na Mafunzo

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023 Kamati iliweza kupata semina mbalimbali ambazo zililenga kuipatia fursa ya kukutana na kufanya majadiliano ya kina na kujengewa uelewa na Wadau mbalimbali katika Masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevya na Magonjwa Yasiyoambukiza.

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli ulio wazi semina hizi zimeisaidia sana Kamati kupata uelewa wa kina kuhusiana na utekelezaji wa afua mbalimbali za Sekta tunazozisimamia. Kamati inawashukuru sana wadau wote ambao wamekuwa mara kwa mara wanakutana na Kamati kwa ajili ya kujadiliana na kujenga uelewa mpana. Kamati inapenda kuwatambua Wadau hao muhimu ambao ni pamoja Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Wizara ya Afya, Shirika la Walter Reed, *ICAP, TanCDA,* UNICEF na UN – Women. Kamati itaendelea kutoa ushirikiano wakati wote wadau hawa wanapotaka kukutana na Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea taarifa hizo za uchambuzi wa shughuli za Kamati kwa Kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao: -

### 3.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)

#### a) Upatikanaji wa Fedha za ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI

**KWA KUWA,** fedha za ndani zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa afua za UKIMWI hazitoshelezi mahitaji kulingana na ukubwa wa tatizo na vile vile hazitolewi kwa wakati;

**NA KWA KUWA,** kuendelea kutegemea fedha kutoka kwa wafadhili wa nje haitoi uhahika wa mapambano endelevu dhidi ya maambukizi ya VVU na ugonjwa wa UKIMWI ambayo yanahitaji rasilimali fedha za uhakika na za kutosha;

**NA KWA KUWA**, Utekelezaji duni wa Afua za UKIMWI unasababisha kuendelea kuchochea maambukizi;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali:-

i) Kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa afua hii ya UKIMWI;

ii) Wizara ya Fedha ihakikishe fedha zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa afua ya UKIMWI zinatolewa kwa wakati ili kunusuru afya za wananchi; na

iii) Mpango mkakati wa kupata vyanzo vingine vya ndani vya mapato uwekwe kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**b) Ongezeko la Maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI**

**KWA KUWA,** kumekuwa na ongezeko la Maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI kwa baadhi ya Mikoa kama vile Mikoa ya Geita na Mwanza;

**NA KWA KUWA,** ongezeko hilo la maambukizi linasababisha Taifa kupoteza nguvu kazi na kuongeza gharama na mzigo kwa Taifa ya manunuzi ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Mamlaka husika kuweka mikakati ya kutoa elimu na afua mbalimbali katika Mikoa hii ili kupunguza maambukizi mapya.

**c) Ukosefu wa Elimu ya UKIMWI katika Maeneo ya Mialo**

**KWA KUWA,** katika maeneo mengi ya mialo wananchi hawana elimu ya kutosha kuhusu UKIMWI;

**NA KWA KUWA** ukosefu huo wa elimu unasababisha wananchi kuwa na mwitikio mdogo wa upimaji wa VVU, matumizi hafifu ya Kondomu, kushindwa kuchukua tahadhari ya kujikinga na hivyo kuchochea ongezeko la maambukizi ya VVU;

**KWA HIYO BASI,** Mamlaka husika zitoe kipaumbele katika maeneo haya kwa kuhakikisha afua zote ikiwemo kutoa elimu itakayosaidia kupunguza maambukizi.

**d) Utekelezaji wa Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF 2018/19 – 2022/23)**

**KWA KUWA,** malengo ya utekelezaji wa malengo ya Mkakati huu ambayo ni kupunguza maambukizi mapya ya VVU, maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto, idadi ya vifo vinavyotokana na UKIMWI unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya WAVIU yanapaswa kufikiwa Mwaka huu wa 2023;

**NA KWA KUWA**, maambukizi mapya ya VVU, maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto, idadi ya vifo vinavyotokana na UKIMWI na unyanyapaa na

ubaguzi dhidi ya WAVIU miongoni mwa jamii bado vyote vipo juu;

**KWA HIYO BASI,** Serikali ihakikishe inaweka mkazo zaidi ili kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya VVU, maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto na vifo vitokanavyo na UKIMWI. Aidha, elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu kupunguza unyanyapaa.

### 3.2 Magonjwa Yasiyoambukiza

**KWA KUWA,** bado wananchi wengi hawana uelewa juu ya namna ya kujikinga na athari kubwa za Magonjwa Yasiyoambukiza**;**

**NA KWA KUWA,** asilimia kubwa ya mgonjwa haya yamekuwa ni tishio kwa afya za Watanzania wengi kwani yamekuwa yanachangia takribani asilimia 33 ya vifo vyote nchini ambapo Tatizo la shinikizo la juu la damu ni chanzo kikuu cha pili cha vifo kwa watu wote wenye umri zaidi ya miaka 50 hapa nchini;

**NA KWA KUWA** Magonjwa haya yanaligharimu Taifa fedha nyingi kutokana na gharama kubwa na ni miongoni mwa sababu kubwa ya kurudisha nyuma uchumi wa mtu mmoja, familia na Taifa kwa ujumla. Tathmini ya haraka *(Rapid Assessment)* za matibabu zilizofanywa na Chama cha Kisukari nchini ili kutambua gharama ilibainika kuwa zaidi ya Shilingi bilioni 290 zinahitajika kwa mwaka kama gharama za dawa kwa wagonjwa milioni 1.5 ya watu wenye kisukari na shinikizo la juu la damu pekee. Gharama hizi ni karibu sawa na asilimia 20 ya bajeti ya Wizara ya Afya.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri yafuatayo:-

i) Mkazo wa Elimu uendelee kutolewa kwa jamii ili kufahamu sababu na madhara yanayotokana na magonjwa haya pamoja na umuhimu wa kujikinga; na

ii) Michezo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ikiwemo kukimbia mchakamchaka virudishwe kama ilivyokuwa zamani ili kuwajenga kiafya na kiakili.

### 3.3 Ugonjwa wa Kifua Kikuu

**KWA KUWA,** bado kuna kiwango kikubwa cha wagonjwa wa Kifua Kikuu katika baadhi ya Mikoa ambacho kinachochewa na masuala mbalimbali kama vile msongamano wa watu, wafungwa na mahabusu katika magereza; upungufu wa vifaa kama mashine za *X- Ray*, makopo au vifaa vya kuchukulia sampuli za makohozi na vitendanishi vya maabara;

**NA KWA KUWA,** ipo hatari ya kuongezeka kwa wagonjwa wengi na vifo na hivyo kupunguza nguvu kazi ya Taifa lakini pia kuongeza mzigo wa kugharimia matibabu;

**KWA HIYO BASI,** Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kununua vifaa kama *Xray machines,* makopo ya sampuli na ujenzi wa magereza ili kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani.

### 3.4 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

#### a) Sera ya Taifa ya kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya nchini

**KWA KUWA,** mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini umechukua muda mrefu na haujakamilika;

**NA KWA KUWA,** kukosekana na kuendelea kuchelewa kwa Sera hii kunaweza kupelekea kukosa mwongozo sahihi katika vita dhidi ya dawa za kulevya kwa ujumla wake;

**NA KWA KUWA,** Kamati inatambua mchakato wa utungwaji wa Sera hiyo kwa sasa upo katika hatua ya kupata maoni ya wadau;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali iharakishe mchakato huu ili kuwezesha Mamlaka kuwa na mwongozo sahihi ambao utasaidia kulinusuru Taifa na janga hili la matumizi ya dawa za kulevya.

#### b) Umuhimu wa Serikali kutenga bajeti ya Mipango ya Maendeleo

**KWA KUWA,** bado Mamlaka haitengewi fedha za utekelezaji wa mipango ya maendeleo;

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa fedha za maendeleo kunapelekea Mamlaka kushindwa kuwasaidia Waraibu wa Dawa za Kulevya ambao

wengi ni vijana pamoja na kushindwa kununua vifaa muhimu vya udhibiti wa dawa za kulevya nchini;

**KWA HIYO BASI,** Serikali itenge fedha za kutosha ili kuwezesha Mamlaka:-

i) Kuanzisha miradi itakayowasaidia waraibu wa dawa za kulevya ili wasiweze kurudi katika matumizi ya dawa za kulevya; na

ii) Kuboresha miundombinu ya udhibiti wa dawa za kulevya kwa mfano ununuzi wa boti na mashine za ukaguzi katika viwanja vyetu vya ndege, bandari na kwenye mipaka ya nchi yetu.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** nakushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi *(ndc),* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Namshukuru sana Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge – Ndg. Athumani Hussein *(ndc),* Mkurugenzi Msaidizi – Ndg. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Happiness Ndalu, Ndg. Asia Msangi, Ndg. Pamela Pallangyo na Msaidizi wa Kamati Ndg. Catherine

Kitutu kwa kuratibu vizuri shughuli zote za Kamati wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mhe. George Boniphace Simbachawene (Mb) na Manaibu Mawaziri Mhe. Ummy Khamis Nderiananga (Mb) na Mhe. Patrobas Katambi (Mb) kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Namshukuru pia Waziri wa Afya Mhe. Ummy A. Mwalimu (Mb) na Naibu Waziri - Mhe. Dkt. Godwin O. Mollel (Mb) kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati wote walipohitajika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Pamoja nao Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hizi mbili ambao ni Dkt. John Jingu na Prof. Abel Makubi pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Dkt. Leonard Maboko, Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya - Kamishna Jenerali Gerald Kusaya na Watendaji wote wa Wizara, Tume na Mamlaka kwa ushirikiano wanaoipatia na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali wakati wa vikao.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa umakini na kujitoa kwao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Amandus Julius Chinguile, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb- Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Justin Lazaro Nyamoga, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Oliver D. Semuguruka, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb -Mjumbe
18. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb -Mjumbe
19. Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mb -Mjumbe
20. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Neema William Mgaya, Mb - Mjumbe
27. Mhe. Juliana David Shonza, Mb - Mjumbe
28. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb- Mjumbe
29. Mhe. Esther Malleko, Mb - Mjumbe
30. Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile - Mjumbe
31. Mhe. Agnes Marwa, Mb - Mjumbe
32. Mhe. Asia Halamga, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo kuhusu shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya

Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**
**FEBRUARI, 2023**

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022 mpaka Januari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sura ya Kwanza, Utangulizi; napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai na kuweza kukutana siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023. Naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Taarifa; Kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, muundo wa Taarifa hii umegawanyika katika Sehemu kuu Tatu kama inavyoonekana kwenye taarifa ukurasa wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Njia na Mbinu Zilizotumika; kwa mujibu wa Kanuni ya 142(a) Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake;

(b) Ziara za ukaguzi wa maeneo mbalimbali kwa lengo la kuona na kujifunza; na

(c) Ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kuona pamoja na

kujiridhisha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhumuni ya Taarifa; kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inawasilisha Taarifa, lengo la kuonesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyo chini ya Sekta ya Nishati na Madini ili kuwezesha Bunge kuwa na picha nzuri ya kuweza kuishauri Serikali hatua za kuchukua kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sura ya Pili; shughuli zilizotekelezwa; katika kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023 kamati imetekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Maazimio; Kamati imepokea, imechambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa maazimio yaliyotolewa na Kamati Mwezi Februari; 2022 kutoka Wizara zote mbili inazozisimamia. Kamati imebaini kwa kiasi kikubwa Kamati Wizara imetekeleza maazimio ya Bunge. Baadhi ya maazimio ambayo yametekelezwa vizuri ni pamoja na:-

(a) Bajeti zimeongezwa kwa Wizara ya Nishati kwa asilimia 13 na Wizara ya Madini kwa asilimia 24.9;

(b) Bajeti ya matengenezo ya miundombinu ya *TANESCO* imeongezwa kufikia Shilingi Bilioni 500; na

(c) Kamati ya *TEITI* imeundwa ili kuharakisha ufanyaji wa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati imebaini maazimio matatu yafuatayo hayakutekelezwa kikamilifu:-

(a) Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* haujafanikiwa kupata kibali kutoka kwa Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)* cha kupitisha miundombinu ya umeme katika hifadhi ya misitu na hivyo kusababisha baadhi ya miradi kuchelewa;

(b) *STAMICO* haijapata kibali cha ajira licha ya kuwa na upungufu wa watumishi kwa asilimia 50.8; na

(c) Mgodi wa *STAMIGOLD* bado unakumbana na changamoto ya gharama kubwa za uendeshaji. Takriban shilingi milioni 700 kwa mwezi zinatumika kununua mafuta ya dizeli ili kuendesha mgodi kutokana na kutokamilika kwa kazi ya kuunganishiwa umeme wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa kuhakikisha inatekeleza maazimio haya ya Bunge mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbili; Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na mwelekeo wa bajeti wa mwaka wa fedha 2022/2023. Taarifa za kina ziliwasilishwa katika Mkutano wa saba wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka Julai – Desemba, 2022. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Wizara ya Nishati imekusanya maduhuli kwa asilimia 15.7 na imepata fedha za bajeti kwa asilimia 39.5 kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba moja kilichopo kwenye ukurasa wa 9 wa taarifa. Aidha, kwa Wizara ya Madini ukusanyaji wa maduhuli kufikia Desemba, 2022 ni asilimia 39.5 na upatikanaji wa fedha ni asilimia 39.32 kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatilia utekelezaji wa Wizara.

(a) Wizara ya Nishati, hali ya uzalishaji wa umeme nchini. Takwimu za Mwezi Januari, 2023 zinaonesha kuwa, kufikia mwezi Disemba, 2022 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyoungwa kwa mfumo wa Gridi ya Taifa ulifikia megawati 1,777.05, sawa na ongezeko la asilimia 4.87 ukilinganisha na Agosti, 2022 ambapo ilikuwa megawati 1,694.55 kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, hali ya umeme bado siyo ya kuridhisha kutokana na sehemu nyingi za nchi kuwa katika mgawo wa umeme. Serikali inapaswa kuchukua jitihada za makusudi hususani kutumia gesi asilia na kuhamasisha uzalishaji wa umeme wa nishati jadidifu ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini.

Athari za kiuchumi zitokanazo na kukatika kwa umeme ni kubwa sana.

(b) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa Bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere. Mradi huu ni moja ya Miradi ya Kimkakati ambayo pia imetajwa katika ilani ya uchaguzi wa CCM ya mwaka 2020 aya ya 63.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa mradi umeongezeka kutoka asilimia 53.25, Desemba, 2021 hadi kufikia asilimia 80.22 Mwezi Desemba, 2022 kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuendeleza umakini na kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi madhubuti ili mradi huu ukamilike kwa wakati kama ulivyopangwa ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa umeme nchini.

(c) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi wa Kituo cha Kuzalisha Umeme Kinyerezi *One*, Kinyerezi *one extension* megawati 185. Mradi huu unahusisha ujenzi wa mitambo minne ya kufua umeme ya kutumia gesi asilia (*gas turbines*) wenye lengo la kuongeza megawati 185 ili kuimarisha na kuongeza uwezo wa *grid* ya Taifa. Mradi umefikia asilimia 92 ya utekelezaji ambapo mitambo mitatu kati ya minne yenye uwezo wa kuzalisha megawati 135 imewashwa na mtambo wa nne uliobaki ulitarajiwa kuwashwa mwishoni mwa Mwezi Januari 2023, hata hivyo mpaka sasa bado haujawashwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa utekelezaji au ukamilishaji wa mradi sio mzuri. Serikali haina budi kuja na mpango madhubuti utakaowezesha *TANESCO* kujitoa katika tatizo hili la miradi yake kutokukamilika kwa wakati.

(d) Mwenendo wa biashara ya mafuta nchini; mwenendo wa biashara ya mafuta nchini umekuwa wa kuridhisha kutoka mwaka 2021 kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati ukurasa wa 18 mpaka 20 na kielelezo Na.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio Kamati imebaini changamoto hususani bei ya mafuta kuendelea kupanda kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo miundombinu duni ya Bandari ya Dar es Salaam ambazo zinachangia ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta na kusababisha uwepo wa gharama za ucheleweshaji kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.6 na Na.7. Ni rai ya Kamati suala la miundombinu lifanyiwe kazi ili kusaidia kupunguza bei ya mafuta nchini.

(e) Hali ya uzalishaji wa gesi asilia nchini na mikakati ya kuongeza uzalishaji; hali ya uzalishaji wa gesi asilia nchini imeendelea kuimarika kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati ukurasa wa 22 - 23. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado uzalishaji huu wa gesi hautoshelezi mahitaji kwani pindi inapotokea hitilafu kwenye mitambo ya uzalishaji nchi inaingia kwenye taharuki kubwa ya uhaba wa gesi na hivyo kuathiri uzalishaji wa umeme na shughuli zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini; moja, hali ya Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Nchini (Mwanza *Gold Refinery*). Ujenzi wa Kiwanda hiki ulianza rasmi tarehe 15 Machi, 2020 na kukamilika Desemba, 2020. Tangu kuanzishwa kwake kumekuwa na mafanikio kama inavyoonekana kwenye taarifa ukurasa wa 33. Pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini Kiwanda kilisimamisha uzalishaji wake mwezi Agosti, 2021 kutokana na kukosa ithibati. Kamati inasisitiza zoezi la ithibati liende sambamba na kufanyika kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, mafanikio na changamoto za utoaji na upatikanaji wa huduma kwa jamii, *corporate social responsibility*. Tangu Sheria ya madini Sura ya 123 ilivyofanyiwa maboresha zaidi ya bilioni 33.5 zimetumika katika miradi mbalimbali iliyotekelezwa na wamiliki wa leseni za madini katika mikoa mbalimbali hapa nchini kama inavyoonekana kwenye kelelezo Na.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyoelezwa, Kamati imebaini baadhi ya taasisi za Serikali kutokutekeleza miradi kwa wakati na hivyo kusababisha uandaaji wa mpango wa miaka inayofuata kuwa mgumu. Hata hivyo uelewa mdogo wa baadhi ya kampuni za madini juu ya wajibu wa kampuni kwa jamii na hasa wamiliki wa leseni za uchimbaji wa kati na mdogo.

(3) Utekelezaji wa Miradi ya madini yenye ubia baina ya Serikali na wawekezaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini Sura Na. 123 kifungu cha 10 ambayo inatoa nafasi kwa Serikali kushiriki katika miradi ya uchimbaji madini kwa kumiliki hisa huru au zisizolipiwa *(non-dilutable free carried interest*) zisizo pungua asilimia 16, tayari Serikali kupitia Wizara ya Madini na Msajili wa Hazina, imetia saini mikataba ya ushiriki kwenye miradi sita ya uchimbaji mkubwa wa madini kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 9.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua mbalimbali za utekelezaji zilizofikiwa na miradi hii, Kamati imebaini uwepo wa changamoto kuu mbili ambazo ni:-

(i) Kutokukamilika kwa wakati kwa baadhi ya mikataba ya kikodi baina ya Serikali na wawekezaji; na

(ii) Kuchelewa kuhuisha taarifa za upembuzi yakinifu kwa baadhi ya miradi. Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia bora itakayowezesha majadiliano kufanyika katika kipindi kifupi ili kukidhi matakwa ya sheria na hatimaye Taifa kuweza kufaidika.

(4) Hali ya uzalishaji wa madini ya almasi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa ujumla uzalishaji uliongezeka kuanzia mwaka 2016 hadi 2019 katika mgodi wa almasi wa kampuni ya *WDL* kutokana na matengenezo yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali kama inavyoonekana kwenye taarifa ukurasa wa 42.

(5) Hali ya uzalishaji wa gesi ya *Helium* nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, gesi ya *Helium* inatumiwa sana katika vyombo vya anga, kuendesha mashine za utabibu na kutengeneza vifaa vya maabara, mitambo ya *nuclear* na vifaa vya *electronic.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini changamoto za uendelezaji wa leseni za gesi ya *Helium* zilizopo kwenye maeneo ya hifadhi na leseni zilizopo katika maeneo ya mabonde. Serikali inapaswa kufanyia kazi.

(6) Hali ya Umiliki wa kitalu “C” Mererani na uendelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Franone Mining and Gems Ltd*. ilipata leseni rasmi tarehe 28 Julai, 2022 baada ya kukamilika kwa hatua mbalimbali ikiwemo Tume ya Madini kujiridhisha na uwezo wa kampuni. Maboresho mbalimbali yamefanyika kama inavyoonekana kwenye taarifa ukurasa wa 47 hadi 48.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini changamoto ya kukatika kwa umeme wa gridi ya Taifa mara kwa mara, hali inayosababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji sambamba

na kuendelea kwa utoroshaji wa madini hayo nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Kamati kuwa eneo ambalo liliingizwa kimakosa kwenye ramani ya kitalu "C" ugawaji wake ufanyike kwa makini ili usizalishe changamoto ya mitobozano.

(7) Mpango wa Serikali kuanza kununua dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania *(BoT),* kuanzia mwaka 1990 hadi 1994 iliwahi kununua dhahabu. Zoezi hilo lilifanyika kwa lengo la kulwezesha *BoT* kuwa na akiba ya dhahabu *(Monetary Gold Reserve)* na pia kununua dhahabu iliyokuwa ikizalishwa kwa wingi na wachimbaji wadogo wadogo. Hata hivyo ilikuwa hali …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, nenda kwenye maoni na mapendekezo.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI YA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sura ya tatu, maoni na mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya jumla:-

Kwa kuwa Bajeti zilizoidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini hazitoki kwa wakati, kwani kufikia Desemba, 2022 upatikanaji upo chini ya asilimia 40 kwa Wizara zote mbili;

Na kwa kuwa moja ya sababu ya kuchelewa kutolewa fedha imeelezwa kuwa ni kuchelewa kuwasilishwa hati za madai na Wakandarasi na mfumo duni wa upitiaji wa hati hizo;

Na kwa kuwa upatikanaji huo wa fedha za bajeti usioridhisha unasababisha Wizara kushindwa kutekeleza kikamilifu majukumu ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma;

Kwa hiyo basi:-

(a) Serikali ihakikishe kuwa fedha zilizoidhinishwa kwa Wizara hizi zinatoka zote na kwa wakati.

(b) Wakandarasi wakamilishe kazi kwa wakati na kuwasilisha hati za madai mapema kwa ajili ya malipo.

(c) Serikali iboreshe mfumo wa kupitia hati za madai ya Wakandarasi kwa ajili ya kuwahisha malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusuasua kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo:-

Kwa kuwa utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo upo nyuma ya muda uliopangwa

ikiwemo Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere *Megawatt* 2115, Mradi wa kufua umeme wa Rusumo *Megawatt* 80 na Mradi wa Umeme wa Kinyerezi I.

Na kwa kuwa kusuasua kwa utekelezaji wa miradi hii kunasababisha nchi kuendelea kuwa na uhaba wa umeme na hivyo shughuli za kiuchumi kutoteketelezwa kikamilifu;

Hivyo basi, Serikali ihakikishe miradi yote inasimamiwa kwa karibu na inakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kusuasua kwa utekelezaji wa Miradi ya *REA*:-

Kwa kuwa baadhi ya Miradi ya *REA* imekuwa haikamiliki kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kupanda kwa bei ya vifaa na baadhi ya wakandarasi kuwa na uwezo mdogo wa kiutendaji;

Na kwa kuwa, kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi hii kunasababisha vijiji kuendelea kukosa umeme na shughuli za kiuchumi kukwama;

Kwa hiyo basi:-

(a) Serikali ihakikishe inawasimamia kwa karibu wakandarasi ili miradi iweze kukamilika kwa wakati.

(b) *REA* iboreshwe ili iweze kusimamia Wakandarasi vizuri.

(c) Kwa lengo la kurahisisha taratibu za manunuzi, wawepo *pre-qualified* Wakandarasi ili waliopo wakishindwa wachukuliwe hawa *pre-qualified* ili kuondoa mlolongo wa manunuzi; na

(d) Taratibu za Kimkataba ziangaliwe na kuboreshwa ili Wakandarasi wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao wapokonywe miradi bila ya kufuata mlolongo mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mafuta:-

Kwa kuwa bei ya mafuta imeendelea kuwa juu kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za gharama za ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta kutokana na miundombinu duni ya Bandari ya Dar es Salaam na ukosefu wa maabara katika Bandari za Mtwara na Tanga;

Na kwa kuwa, kupanda kwa bei ya mafuta kunachangia pia Mfumuko wa bei nchini na hivyo kufanya wananchi wengi washindwe kumudu gharama za Maisha;

Kwa hiyo basi, Serikali ifanye yafuatayo:-

(a) Iboreshe Miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam ili kuwezesha upakuaji wa haraka wa mafuta;

(b) Isimamie *TBS* ili waharakishe ujenzi wa Maabara za Tanga na Mtwara.

(c) Ikamilishe mapema *Service Level Agreement (SLA)* ili Taasisi zinazohusika ziwajibike kubeba gharama za ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta (*demurrage charges)* na hivyo kumwondolea mzigo mlaji wa mwisho kubeba gharama kupitia bei ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa Sheria ya Joto Ardhi:-

Kwa kuwa Mchakato wa kuleta Muswada wa Sheria ya Joto Ardhi umechukua muda mrefu, Kamati hairidhishwi na mwenendo wa utekelezaji wake;

Na kwa kuwa ukosefu wa sheria unasababisha kusuasua…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ahsante. Malizia, muda wako umekwisha.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI YA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa mara nyingine tena napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako thabiti. Kamati inaendelea kukuahidi ushirikiano na tunakuombea kila la heri katika utekelezaji bora wa majukumu yako. Aidha, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa kamati ya Nishati na madini kwa ushirirkiano wao katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawapongeza na kuwashukuru sana Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Mkamba; Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Steven Byabato; Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dotto Biteko, na Naibu Waziri Dkt…

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante, ahsante, wameshakuelewa. Toa hoja.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI YA MADINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2022 HADI JANUARI, 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

## SURA YA KWANZA

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai na kuweza kukutana siku hii ya leo. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari 2022 hadi Januari 2023.Naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwene Hansard.

**Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Muundo wa Taarifa hii umegawanyika katika Sehemu tatu kama inavyoonekana kwenye taarifa ukurasa wa kwanza.

**Mheshimiwa Spika,** Njia na Mbinu Zilizotumika; Kwa mujibu wa Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Nishati na Madini ilitumia njia na mbinu mbalimbali kama ifuatavyo:-

Vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kwa lengo la kufahamu utendaji wao, mafanikio na changamoto wanazokutana nazo;

Ziara za ukaguzi wa maeneo mbalimbali kwa lengo la kuona na kujifunza; na

Ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kuona pamoja na kujiridhisha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Taarifa;kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inawasilisha Taarifa Lengo la kuonesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyo chini ya Sekta ya Nishati na Madini ili kuwezesha Bunge kuwa na picha nzuri ya kuweza kuishauri Serikali hatua za kuchukua kwa maslahi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** sura ya pili; shughuli zilizotekelezwa; katika kipindi cha kuanzia Februari 2022 hadi Januari 2023 kamati imetekeleza kazi zifuatazo: -

**Mheshimiwa Spika,** Kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa MaazimioKamati imepokea, imechambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa maazimio yaliyotolewa na Kamati Mwezi Februari 2022 kutoka Wizara zote mbili inazozisimamia. Kamati imebaini kwa Kiasi kikubwa Kamati Wizara imetekeleza maazimio ya Bunge. Baadhi ya maazimio ambayo yametekelezwa vizuri ni pamoja na

(a) Bajeti zimeongezwa kwa Wizara ya Nishati kwa asilimia 13 na Wizara ya Madini kwa asilimia 24.9;

(b) Bajeti ya matengenezo ya miundombinu ya TANESCO imeongezwa kufikia Shilingi Bilioni 500; na

(c) Kamati ya TEITI imeundwa ili kuharakisha ufanyaji wa maamuzi.

**Mheshimiwa Spika,** aidha Kamati imebaini maazimio matatu yafuatayo hayakutekelezwa kikamilifu.

(a) Wakala wa Nishati Vijijini (REA)haujafanikiwa kupata kibali kutoka kwa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) cha kupitisha miundombinu ya umeme katika hifadhi ya misitu na hivyo kusababisha baadhi ya miradi kuchelewa;

(b) STAMICO haijapata kibali cha ajira licha ya kuwa na upungufu wa watumishi kwa asilimia 50.8; na

(c) Mgodi wa STAMIGOLD bado unakumbana na changamoto ya gharama kubwa za uendeshaji. Takribani Shilingi Milioni 700 kwa mwezi zinatumika kununua mafuta ya dizeli ili kuendesha Mgodi kutokana na kutokamilika kwa kazi ya kuunganishiwa umeme wa Gridi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapaswa kuhakikisha inatekeleza maazimio haya ya Bunge mapema.
**Mheshimiwa Spika,** Mbili; Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na mwelekeo wa bajeti wa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni[1], mara baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za kina za Uchambuzi wa Bajeti za Wizara hizo na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2022. Kwa ujumla Bajeti za Wizara zimeongezeka; Kwa mfano: Bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) imeongezeka kutoka Shilingi 2,385,980,809,000/= Mwaka 2021/2022 hadi kufikia Shilingi 2,705,981,533,000/= sawa na ongezeko la asilimia 13. Kwa upande wa Wizara ya Madini (Fungu 100), Bajeti imeongezeka kwa asilimia 24.9 kutoka Shilingi 66,816,467,000.00 Mwaka 2021/2022 hadi kufikia Shilingi 83,445,260,000.00 Mwaka 2022/2023.

**Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2022)**

---

[1] Kanuni ya ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia msingi wa Ibara ya 63 (3)(b)ya Katiba pamoja na Nyongeza ya Nane (7)(1)(a), katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Januari 2023, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2022) za Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Lengo la kufanya hivyo ilikuwa ni kuona mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha ili kuweza kuishauri Serikali ipasavyo hasa ikizingatiwa kuwa inategemewa kufikia Disemba 2022 ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha uwe umefikia angalau asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

**Wizara ya Nishati**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Shilingi 20,393,000.00. Kufikia Disemba 2022, Kiasi cha Shilingi 3,210,099.03 kimekusanywa sawa na asilimia 15.7 ya lengo. Aidha, kwa upande wa bajeti, Wizara imepokea jumla ya Shilingi 1,147,257,887,141 ambayo ni sawa na asilimia 39.5 ya kiasi cha Shilingi 2,905,981,533,000 kilichoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, upatikanaji wa fedha za maendeleo hususan kutoka nje siyo wa kuridhisha kwani kiasi cha Shilingi 66,757,312,555.62 ndicho kimepokelewa kwa utaratibu wa D- Fund. Kwa mujibu wa utaratibu uliopo, taarifa ya fedha hizo zitaingizwa katika Hesabu za Wizara wakati mwaka

wa fedha unapokamilika baada kupokelewa kwa *dummy exchequer* kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

KIELELEZO Na.1: Upatikanaji wa Fedha Wizara ya Nishati kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2022


| AINA | KILICHOIDHINISHWA | KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 14,726,136,000 | 7,159,840,281 | 48.6 |
| OC | 15,025,821,000 | 5,868,410,363 | 39.1 |
| MAENDELEO NDANI | 2,708,756,128,000 | 1,134,229,636,497 | 41.9 |
| MAENDELEO NJE | 167,473,448,000 | | - |
| JUMLA | 2,905,981,533,000 | 1,147,257,887,141 | 39.5 |

Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Nishati ya Januari 2023 na Usanifu wa Kamati

**Wizara ya Madini**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Shilingi 894,278,406,800.00. Kufikia Disemba 2022, Wizara imekusanya Shilingi 353,429,346,684.78 sawa na asilimia 39.5 ya lengo kwa kipindi hicho. Kwa upande wa bajeti, Wizara imepokea jumla ya Shilingi 32,897,571,819.65 sawa na asilimia 39.32 kati ya Shilingi 83,445,260,000.00 zilizoidhinishwa na Bunge. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, fedha za OC na Mishahara ni asilimia 44.81 na 49.77 mtawalia. Aidha, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni asilimia 19.32 tu kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

KIELELEZO NA.2: Upatikanaji wa Fedha Wizara ya Madini kwa kipindi cha Julai -Disemba, 2022




Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Madini ya Januari 2023 na usanifu wa Kamati

**Kufuatilia utekelezaji wa Wizara**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni[2], Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kama ifuatavyo:-

**Wizara ya Nishati**

**Mheshimiwa Spika,** katika Wizara ya Nishati, Kamati ilipokea, ilijadili na kuchambua taarifa za utekelezaji zifuatazo:-

Hatua iliyofikiwa katika Muswada wa Sheria ya Joto Ardhi

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa rasilimali ya jotoardhi unapitia changamoto mbalimbali ikiwemo

[2] Nyongeza ya nane 7(1) (d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020

kukosekana kwa tafsiri ya kisheria ya jotoardhi, mwongozo wa umiliki, mfumo wa utoaji leseni, ushiriki wa sekta binafsi, miongozo ya kiusalama, ulipaji wa ada na tozo, na utaratibu stahiki wa uendelezaji wa jotoardhi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikisisitiza umuhimu wa kuletwa Muswada wa Sheria ya Jotoardhi ili kuweza kuziba ombwe la changamoto zilizoelezwa. Kamati inafahamu kuwa ukusanyaji wa maoni ya wadau umekamilika na Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria hii tayari umeshajadiliwa katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na kufanyiwa maboresho kwaajili ya kuwasilishwa kwenye *Inter –Ministerial Technical Committee*.

**Mheshimiwa Spika,** ukosefu wa sheria hii umekuwa ni kikwazo katika uendelezaji wa rasilimali hii muhimu na hivyo kushindwa kusaidia katika kuongeza upatikanaji wa umeme nchini. Ni imani ya Kamati kuwa muswada huu wa Sheria utaletwa mapema kuwezeshwa kutungwa kwa sheria hii muhimu na hivyo kuleta tija katika matumizi ya rasilimali hii.

**Hali ya uzalishaji wa Umeme nchini**


**Mheshimiwa Spika,** imekuwa ni utaratibu wa Kamati kupokea Taarifa ya hali ya uzalishaji wa umeme nchini. Lengo la kufanya hivi ni kuweza kufahamu mafanikio na changamoto ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya mwezi Agosti 2022 ilionesha kuwa hali ya upatikanaji wa umeme nchini

katika maeneo mbalimbali iliendelea kuimarika. Takwimu za Agosti 2022 zilionesha kuwa, uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyoungwa katika Gridi ya Taifa ulifikia MW 1694.55 kutoka vyanzo mbalimbali. Pamoja na uzalishaji huo, TANESCO imekuwa ikinunua umeme kutoka kwa wazalishaji wadogo binafsi wa ndani ya nchi jumla ya MW 26.86 na inanunua umeme kutoka nje ya nchi ikiwemo Uganda MW 17 kwa ajili ya Mkoa wa Kagera, Zambia MW 5 kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa,na Kenya MW 1 kwa ajili ya Wilaya ya Longido.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu za Mwezi Januari 2023 zinaonesha kuwa, kufikia mwezi Disemba, 2022 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyoungwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulifikia MW 1,777.05 sawa na ongezeko la asilimia 4.87 ukilinganisha na MW 1,694.55 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Agosti, 2022. Aidha, uwezo wa kuzalisha umeme kwa mitambo ambayo haijaunganishwa katika Gridi ya Taifa umefikia MW 39.302 na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini kufikia MW 1,816.352 ikilinganishwa na MW 1,733.38 zilizokuwepo mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 4.89. Ongezeko hili limetokana na kukamilika kwa ufungaji wa mitambo mitatu (3) kati ya minne (4) ya Kinyerezi 1 Extension yenye uwezo wa MW 135 ambayo inachangia MW 90 katika Gridi ya Taifa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.3.

KIELELEZO 3: Hali ya uzalishaji wa umeme nchini kwa kipindi cha Agosti - Disemba, 2022




*Chanzo: Taarifa za Wizara ya Nishati na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Mahitaji ya umeme nchini katika mfumo wa Gridi ya Taifa yameendelea kukua na kufikia MW 1,391.65 ambayo yalifikiwa tarehe 17 Januari, 2023 saa 2:00 usiku ikilinganisha na wastani wa mahitaji ya umeme kwa mwaka 2022 ambayo yalikuwa MW 1,324.12 sawa na ongezeko la asilimia 5.1.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, hali ya umeme bado siyo ya kuridhisha. Kuanzia mwezi Agosti 2022 sehemu nyingi za nchi zimekuwa katika mgao wa umeme. Wizara imekuwa ikieleza changamoto mbalimbali kama vile ukame ambao umesababisha vyanzo vya kuzalisha umeme kwa kutumia maji kutotumika kwa uwezo wake wa juu; uhaba wa gesi asilia ya kutosha inayoweza kuendesha mitambo ya gesi asili ambayo

ipo katika uzalishaji; na uchakavu wa miundombinu ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme. Kamati inaona Serikali ina kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha kunakuwa na umeme wa kutosha nchini. Itakumbukwa kuwa hata Miradi mingi ambayo ipo kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 na Ilani bado haijakamilika na mingine haijaanza kama ilivyopangwa. Serikali inapaswa kuchukua jihada za makusudi hususan kutumia gesi asilia na kuhamasisha uzalishaji wa umeme wa nishati jadidifu ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini. Athari za kiuchumi zitokanazo na kukatika kwa umeme ni kubwa sana.


Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa Bwawa la kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP)

**Mheshimiwa Spika,** katika vipindi tofauti Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi huu. Itakumbukwa kuwa Mradi huu ni moja ya miradi ya kimkakati ambayo pia imetajwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 aya ya 63

"*Katika miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kinakusudia kuimarisha zaidi sekta ya nishati kwa kuhakikisha kuwa nchi inazalisha umeme wa kutosha ili kukidhi mahitaji ya uchumi wa viwanda na soko la nje. Katika kufikia azma hii, CCM itaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:- Umeme (a) Kukamilisha ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project-JNHPP) unaotarajia kuzalisha MW 2,115*".

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa mradi umeongezeka kutoka asilimia 53.25 Disemba 2021 hadi kufikia asilimia 80.22 mwezi Disemba 2022 sawa na ongezeko la utekelezaji kwa asilimia 26.97. kwa kipindi cha mwaka mmoja na kutoka asilimia 67.18 mwezi Julai 2022 hadi kufikia asilimia 80.22 mwezi Disemba 2022 sawa na ongezeko la utekelezaji kwa asilimia 13.04 ndani ya miezi 6. Asilimia ya utekelezaji wa maeneo mbalimbali ya mradi ni kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 4. Kamati inaendelea kusisitiza kuendeleza umakini na kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi madhubuti ili mradi huu ukamilike kwa wakati kama ulivyopangwa. Hii itasaidia kuondoa changamoto ya upatikanaji wa umeme nchini na pia kuchochea maendeleo.

KIELELEZO NA. 4: Asilimia ya utekelezaji wa maeneo ya Mradi




Chanzo: Taarifa za Wizara ya Nishati na Usanifu wa Kamati

**Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa upanuzi wa Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I (Kinyerezi I Extension MW 185)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100. Mradi unahusisha ujenzi wa mitambo minne ya kufua umeme kwa kutumia gesi asilia (*gas turbines*) wenye lengo la kuongeza MW 185 na hivyo kufanya uwezo wa Kituo cha Kinyerezi I kuzalisha jumla ya MW 335 ambazo zitaimarisha na kuongeza uwezo wa Gridi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi umefikia asilimia 92 ya utekelezaji ambapo mitambo mitatu kati ya minne yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 135 imewashwa na umeme unaozalishwa kuingizwa katika Gridi ya Taifa. Mtambo wa nne uliobaki ulitarajiwa kuwashwa mwishoni mwa mwezi Januari, 2023. Hata hivyo, mpaka tunapowasilisha Taarifa hii, mtambo huu bado haujawashwa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mwenendo wa utekelezaji/ukamilishaji wa miradi kwa wakati siyo mzuri. Serikali ije na mpango madhubuti utakaowezesha TANESCO kujitoa katika tatizo hili la miradi yake kutokamilika kwa wakati kwa mujibu wa mpango kazi uliopo.Ni Rai ya Kamati kuwa ili kutoruhusu hali kama hii kujitokeza tena, Kamati inasisitiza kuwa, ni vyema Serikali ihakikishe kuwa inafanyika *due diligence* ya uhakika kabla ya kuwapa Wakandarasi kazi ili kuepuka changamoto kama hii. Ikumbukwe kuwa hali ya uzalishaji wa

umeme katika nchi yetu hairidhishi, hivyo kuchelewa kwa miradi kama hii ndiyo kunasababisha kuwa na umeme usiotosheleza mahitaji.
Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu (*Renewable Energies*) jotoardhi, upepo na jua.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania inakadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa Jotoardhi usiopungua MW 5000 zinazopatikana katika maeneo zaidi ya 50 ndani ya Mikoa 16 nchini. Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC) inaendelea na utekelezaji wa miradi mitano ya kipaumbele ili kufikia lengo la kuzalisha MW 200 ifikapo 2025 ukiwemo wa Ngozi (Mbeya) MW 70, Songwe MW 5 hadi 38, Kiejo Mbaka (Mbeya) MW 60, Luhoi Pwani MW 5 na Natron Arusha MW 60.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, pamoja na malengo ya miradi hii ambayo baadhi imepangwa kukamilika ifikapo 2024 na mingine 2025 utekelezaji wake utakuwa mgumu kwani miradi mingi ipo katika hatua za awali sana. Itakumbukwa kuwa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi aya ya 63 (m) inasisitiza kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu (*renewable energy*) ikiwemo miradi ya umeme jua, jotoardhi na upepo angalau kufikia MW 1,100 ifikapo 2025. Kamati inaona kuwa, ili kuweza kufikia lengo, ipo haja ya lazima kuweka mkazo katika chanzo hiki cha nishati ambacho ni rafiki wa mazingira na nafuu. Upatikanaji wa Sheria mahsusi ni katika kuwezesha kuvutia mitaji na kuendeleza chanzo hiki muhimu.

**Mwenendo wa Biashara ya Mafuta nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Wizara kuhusu mwenendo wa biashara ya mafuta nchini ya mwezi Agosti, 2022 ilionesha kuwa, katika kipindi cha miezi sita (Machi hadi Agosti 2022) Wakala ulifanikiwa kutoa zabuni 61 zenye jumla ya Tani 3,739,046 za mafuta ya dizeli, petroli, ndege na taa ambapo tani 1,613,003 sawa na asilimia 48.4 kwaajili ya matumizi ya ndani ya nchi na tani 2,126,043 sawa na asilimia 51.6 yanayopita kwenda nchi jirani. Kiasi ambacho kwa ujumla ni ongezeko la asilimia 39 la kiasi cha mafuta tani 2,689,738 kilichoagizwa katika Mwaka 2021. Ongezeko zaidi ni katika mafuta yanayopita kwenda nje kutokana na ufanisi mzuri wa mfumo wa uagizaji wa mafuta wa pamoja ambao umeendelea kuzijengea imani nchi jirani kuendelea kutumia mfumo huu. Aidha, umakini unatakiwa katika kuhakikisha kuwa fedha za kigeni zinazotumika kwa mafuta yanayokwenda nje haziathiri uchumi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya upatikanaji wa mafuta nchini katika kipindi hicho chote imekuwa ya kuridhisha kwani kulikuwepo na akiba kwa mahitaji ya miezi miwili ya mbele kama inavyopaswa. Kwa ujumla mwenendo wa biashara ya mafuta kuanzia Julai hadi Disemba 2022 ni kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.5.

KIELELEZO NA.5: Mafuta yaliyoingizwa Nchini kuanziaJulai - Disemba 2022

| MWEZI | LOCAL | % | TRANSIT | %2 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| JULAI | 337,863,260 | 48.6 | 357,987,929 | 51.4 | 695,851,189 |
| AGOSTI | 478,747,953 | 55.0 | 391,105,966 | 45.0 | 869,853,919 |
| SEPT | 326,177,942 | 50.7 | 317,441,548 | 49.3 | 643,619,490 |
| OCT | 346,659,735 | 43.7 | 447,413,291 | 56.3 | 794,073,026 |
| NOV | 296,671,777 | 44.2 | 373,966,224 | 55.8 | 670,638,001 |
| DEC | 309,060,296 | 47.3 | 343,757,675 | 52.7 | 652,817,971 |
| JUMLA | 2,095,180,963 | 48.4 | 2,231,672,633 | 51.6 | 4,326,853,596 |

Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Nishati Januari 2023

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio ambayo yamepatikana tangu kuanzishwa kwa mfumo huu, Kamati imebaini changamoto za ushiriki mdogo wa Kampuni za ndani kutokana na uwezo mdogo wa mtaji; na bei ya mafuta kuendelea kupanda kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za miundombinu duni ya bandari ya Dar Es Salaam, Ukosefu wa Maabara za kupima sampuli za mafuta katika bandari ya Tanga na Mtwara ambazo zote zinachangia ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta na kusababisha uwepo wa gharama za ucheleweshaji *(demurrage charges)* kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 6 na 7.

KIELELEZO NA.6: Kiwango cha gharama za ucheleweshaji

| Mwezi | KIWANGO CHA GHARAMA ZA UCHELEWESHAJI (*DEMURRAGE RATE*) | | |
|---|---|---|---|
| | Wastani (Dola/Tani) | | |
| | DSM | Tanga | Mtwara |
| Julai 2022 | 2.9151 | 0.5944 | 6.6511 |
| Agosti 2022 | 1.8611 | 0.2817 | 5.8318 |
| Septemba 2022 | 2.7293 | 0.2052 | 5.9647 |
| Oktoba 2022 | 4.2703 | 6.9655 | 5.9859 |
| Novemba 2022 | 6.9329 | 0.4819 | - |
| Desemba 2022 | 5.3934 | 0.0982 | 5.6278 |

KIELELEZO 6: Asilimia ya Gharama ya ucheleweshaji katika bei ya mafuta

| | Gharama za Ucheleweshaji (TZS/Lita) | | | | | | | Asilimia ya Gharama ya Ucheleweshaji katika Bei ya Mafuta | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwezi | Petroli (TZS/L) | | | Dizeli (TZS/L) | | | Mafuta ya Taa (TZS/L) | Petroli | | | Dizeli | | | Mafuta ya Taa |
| | DSM | Tanga | Mtwara | DSM | Tanga | Mtwara | DSM | DSM | Tanga | Mtwara | DSM | Tanga | Mtwara | DSM |
| Julai 22 | 5.07 | 1.01 | 11.30 | 5.64 | 1.14 | 13.02 | 5.37 | 0.16% | 0.03% | 0.35% | 0.18% | 0.04% | 0.41% | 0.16% |
| Agosti 22 | 3.23 | 0.48 | 10.33 | 3.58 | 0.55 | 11.37 | 3.43 | 0.10% | 0.01% | 0.30% | 0.11% | 0.02% | 0.34% | 0.09% |
| Septemba 22 | 4.75 | 0.36 | 10.42 | 5.34 | 0.40 | 11.61 | 5.06 | 0.16% | 0.01% | 0.34% | 0.17% | 0.01% | 0.37% | 0.15% |
| Oktoba 22 | 7.32 | 11.98 | 10.42 | 8.26 | 13.47 | 11.61 | 7.88 | 0.25% | 0.41% | 0.34% | 0.27% | 0.44% | 0.37% | 0.24% |
| Novemba 22 | 12.94 | 0.82 | 10.28 | 14.58 | 0.94 | 11.55 | 13.85 | 0.46% | 0.03% | 0.35% | 0.48% | 0.03% | 0.37% | 0.44% |
| Desemba 22 | 9.33 | 0.17 | 9.57 | 10.56 | 0.19 | 10.89 | 9.96 | 0.33% | 0.01% | 0.34% | 0.33% | 0.01% | 0.33% | 0.31% |

Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Nishati ya Januari, 2023

**Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi (*crude oil*) kutoka nchini Uganda hadi Chongoleani (Tanga) nchini Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya EACOP inayomilikiwa na wabia ambao

ni; TPDC (15%), UNOC (15%) CNOOC (8%) na Total Energies (62%). Mradi unahusisha ujenzi wa bomba la urefu wa Kilomita 1,443 na miundombinu yake na kati ya Kilomita hizo, Kilomita 1,147 sawa na asilimia 79.5 zitakuwa upande wa Tanzania na Kilomita 296 sawa na asilimia 20.5 upande wa Uganda. Bomba litapita katika Mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga na litakuwa na uwezo wa kusafirisha mapipa 216,000 ya mafuta ghafi kwa siku. Gharama za ujenzi wa Mradi inakadiriwa kuwa Dola za Marekani bilioni 5.144.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa mradi huu umefikia katika hatua mbalimbali kama vile malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha maeneo yao kwajili ya ujenzi wa Kambi umekamilika kwa asilimia 99.7; utwaaji wa Ardhi ya Mkuza wa Bomba, ulipaji wa fidia kwa wananchi Shilingi Bilioni 6.34 zimekwishalipwa kwa wananchi 1,275 waliosaini mikataba ya fidia na taratibu za malipo kwa wananchi waliobaki zinaendelea. Aidha, utwaaji wa Ardhi ya Ujenzi wa Kituo cha Chongoleani nao upo katika hatua ya uidhinishwaji.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja hatua hiyo iliyofikiwa, Kamati imebaini uwepo wa changamoto ya pingamizi la mradi kutoka kwa wanaharakati wa mazingira. Ni Rai ya Kamati kuwa, Serikali iendelee kutoa ufafanuzi dhidi ya taarifa kinzani za wanaharakati.

**Hali ya uzalishaji wa Gesi Asilia nchini na mikakati iliyopo ya kuongeza uzalishaji**

**Mheshimiwa Spika,** takwimu za Wizara zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Oktoba, 2022 jumla ya futi za ujazo trilioni 57.54 *(Trillion Cubic Feet*) za gesi asilia zimegunduliwa. Kati ya hizo, takriban futi za ujazo trilioni 47.13 zimegunduliwa katika bahari kuu katika vitalu namba 1, 2, 3 na 4; na futi za ujazo takribani trilioni 10.41 zimegunduliwa maeneo ya nchi kavu. Upatikanaji wa gesi umewezesha kuimarika kwa uzalishaji wa umeme nchini ambapo kwa sasa zaidi ya MW 1021.32 za umeme zinazalishwa kwa kutumia gesi asilia ambazo ni sawa na takribani asilimia 65 hadi 70 ya umeme wote unaozalishwa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** uzalishaji huu wa gesi umekuwa na mchango kwa Pato la Taifa kwani kuanzia mwaka 2016/2017 mpaka sasa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) limewasilisha jumla ya Shilingi bilioni 312.19 katika Mfuko wa Mafuta na Gesi na kupeleka Serikalini gawio la zaidi ya Shilingi bilioni 14.4 kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa hali ya uzalishaji wa gesi asilia nchini, ilielezwa kuwa hali inazidi kuimarika ambapo wastani wa futi za ujazo milioni 220.6 zinazalishwa kwa siku (220.6mmscfd) ikilinganishwa na mahitaji ya sasa ambayo ni futi za ujazo milioni 210 kwa siku (210mmscfd). Gesi hii inazalishwa kutoka Vitalu viwili vya Songo Songo wastani wa futi za ujazo milioni 130 (130mmscfd) kwa siku na Kitalu cha Mnazi Bay wastani wa futi za ujazo milioni 95 kwa siku (95 mmscfd).

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado uzalishaji huu wa gesi hautoshelezi mahitaji kwani pindi inapotokea hitilafu kwenye mitambo ya uzalishaji nchi inaingia kwenye taharuki kubwa ya uhaba wa gesi na hivyo kuathiri uzalishaji wa umeme na shughuli nyinginezo. Wizara ilieleza Mikakati mbalimbali iliyonayo katika kuongeza uzalishaji wa gesi ikiwemo ya Muda Mfupi itakayomalizika ndani ya mwaka mmoja hadi mitatu kama vile ukarabati na uchorongaji wa vitalu vya Songo Songo na Mnazi Bay na Ruvuma; Mikakati ya Miradi ya Muda wa Kati itakayokamilika ndani ya muda wa miaka mitatu hadi mitano ikiwemo miradi inayolenga kuongeza uzalishaji wa gesi asilia kwa kutekeleza katika vitalu vya Eyasi Wembere, Songo Songo Magharibi, Mnazi Bay Kaskazini; na Mikakati ya Miradi ya Muda Mrefu ya kipindi cha zaidi ya miaka mitano inayohusu miradi mbalimbali kama vile Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (LNG) ambao unalenga kuzalisha, kuchakata na kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika vitalu namba 1, 2 na 4 vilivyopo katika bahari ya kina kirefu (*deep sea*) katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

**Utekelezaji wa Kanuni ya Vituo vya Mafuta Vijijini (T*he Petroleum* (*(retail operations in townships and villages)* rules, 2020 gn 818)**

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2020, Wizara ya Nishati kupitia EWURA iliandaa Kanuni mahsusi kwa ajili ya vituo vya mafuta vijiji na kwenye miji midogo "*The Petroleum (retail operations in townships and villages) Rules, 2020 GN No. 818*". Lengo la Kanuni hizi ni kurahisisha mahitaji ya kupata vibali ya ujenzi na

leseni kutoka EWURA ili kurahisisha uwekezaji wa vituo vya mafuta vijijini na katika miji midogo.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni hizi zimeleta mafanikio ambayo ndiyo msingi wa utungwaji wake kwani kumekuwa na ongezeko la vituo vya mafuta vijijini na katika miji midogo kutoka vituo 165 (Septemba, 2020) hadi vituo 318 (Septemba, 2022) sawa na ongezeko la asilimia 48.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, kumekuwa na changamoto zifuatazo:-

Gharama kubwa za vibali kutoka taasisi mbalimbali nchini zikiwemo Halmashauri, Zimamoto, TANROADS, TARURA, NEMC na OSHA;

Maeneo ya Vijijini kutokuwa na mitaji imesababisha Wafanyabiashara wengi vijijini kushindwa kujenga vituo vya mafuta na hivyo kupunguza kasi ya ujenzi wa vituo;

Upatikanaji wa wasambazaji wa mafuta kwa wenye vituo vya mafuta vya vijijini ni mgumu kutokana na ujazo mdogo wa matenki; na

Utaratibu wa utunzaji, usafirishaji na usalama wa fedha kutoka kwenye vituo vya vijijini kutokana na ukweli kuwa taasisi za fedha sehemu hizi ni haba.

Ziara ya Mafunzo katika Sekta ya Nishati

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya mafunzo katika Mkoa wa Mtwara, Lindi na Dar Es Salaam.

Ziara hizo zililenga kujionea na kujifunza utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara ya Nishati inayohusu Gesi na Umeme. Kamati ilitembelea maeneo yafuatayo:-

**Visima vya kuzalisha gesi vya Msimbati/Mnazi Bay - Mtwara**

**Mheshimiwa Spika,** Visima hivi vinaendeshwa na Kampuni ya Morel & Prom katika eneo ambalo lina jumla ya visima vinne (4) vilivyopo nchi kavu na kimoja (1) kipo baharini. Visima hivi vitano (5) vina uwezo wa kuzalisha futi za ujazo Milioni 90 kwa siku ambazo huchukuliwa na TANESCO na GASCO kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, matumizi ya nyumbani lakini pia matumizi mbalimbali kama kutengeneza saruji kwa Kampuni ya Dangote. Aidha, Maurel & Prom wana kiwanda cha kuchakata gesi katika kitalu cha Mnazi bay chenye uwezo wa kuchakata hadi futi za ujazo 10 kwa siku za gesi ambayo inatumika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, nishati ya uendeshaji wa viwanda, matumizi ya kupikia majumbani na kwenye magari.

**Mitambo ya Kuchakata Gesi Asilia-Madimba**

**Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Madimba kina vinu vitatu vyenye ukubwa sawa na uwezo wa kuchakata gesi futi za ujazo milioni 210 kwa siku (210mmscfd). Kiwanda hiki kilianza uchakataji wa gesi asilia mwezi Septemba 2015 kwa uchakataji wa gesi ghafi kwa wastani wa 25 - 45 mmscfd kutoka katika kitalu cha Mnazi Bay kinachoendeshwa na kampuni ya Morel and Prom (M&P). Kwa sasa matumizi ya gesi asilia yameongezeka na kiasi cha wastani wa futi za ujazo milioni 85 - 90 kinachakatwa kwa siku.

**Mheshimiwa Spika,** Mitambo hii inasimamiwa na kuendeshwa Kampuni tanzu ya GASCO. Kamati ilijionea uwekezaji mkubwa uliofanyika na ilifarijika kutokana na Kituo chote kuendeshwa na Wazawa kwa ufanisi na usalama wa hali ya juu; ambapo kwa kipindi cha miaka 5 jumla ya saa 1400 za kazi zimetumika na hakuna ajali yoyote iliyotokea. Kamati inapongeza sana kazi nzuri inayofanywa na wazawa hawa.

**Kitalu cha Gesi cha Ntorya**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea kitalu cha gesi cha Ntorya na kushuhudia kazi ya ukusanyaji wa data ikiendelea. Aidha, tayari kuna visima vimechimbwa vyenye uwezo wa kuzalisha jumla ya futi za ujazo za gesi Milioni 30. Eneo hili ambalo kwa ujumla ni la PSA ya Ruvuma kwa sasa lipo chini ya Ubia wa Kampuni ya ARA asilimia 75 na Ndovu Resources asilimia 25.

**Mitambo ya Kuzalisha Umeme ya Kinyerezi II**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi II. Kituo kina mitambo nane (8) ambapo sita (6) inatumia gesi asilia (*gas turbines*) na 2 inatumia mvuke (*steam turbines*). Kamati ilijulishwa kuwa Mitambo sita inayotumia gesi kuzalisha umeme imefungiwa Mitambo ya kuchemsha maji kupata mvuke na kasha mvuke huo kutumika kwenye Mitambo mingine Miwili ili kuzalisha Umeme.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyokuwa kwa miradi ya Mtwara, Uendeshaji wa kituo hiki unafanywa na

wataalam wazawa kwa asilimia 100. Aidha, matengenezo kinga *(Preventive maintenance)* ya mitambo yamekuwa yakifanyika ipasavyo kwa kufuata maelekezo ya watengeneza mitambo (*Original Equipment Manufacturers*).

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla katika ziara hiyo Kamati imebaini pamoja na kazi nzuri inayofanywa na wazawa bado maslahi yao siyo ya kuridhisha. Ni Rai ya Kamati kuwa, ni vyema maslahi ya wataalam hawa yaboreshwe.

**Wizara ya Madini**

Mheshimiwa Spika, Kupitia Wizara ya Madini, Kamati ilpokea, ilichambua na kujadili Taarifa mbalimbali kama ifuatavyo:-

**Hatua iliyofikiwa katika kuhuisha Sera ya Madini ya Mwaka 2009**

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Madini ya mwaka 2009 inalenga katika kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta nyingine za uchumi, kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuongeza faida zitokanazo na uchimbaji madini, kuboresha mazingira ya kisheria, kuimarisha uwezo wa usimamizi wa Sekta ya Madini, kuendeleza wachimbaji wadogo, kukuza na kuwezesha uongezaji thamani wa madini na kuimarisha usimamizi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kutokana na uwepo wa Sera hiyo. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na kutungwa kwa Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Madini, Sura 123 na kanuni zake. Vilevile Sheria

mbalimbali zinazohusiana na masuala ya fedha zilifanyiwa marekebisho kwa lengo la kuweka mfumo wa kifedha wenye ushindani na unaotabirika kwa wawekezaji katika Sekta ya Madini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini uwepo wa changamoto zikiwemo za kitakwimu ambazo zimepitwa na wakati na zinahitaji kuhuishwa. Kamati ilihakikishiwa kuwa Wizara inaendelea na tathmini ya sera hii na baada ya kukamilika kwa hatua hiyo, itaratibu zoezi la ukusanyaji wa maoni ya Wadau mbalimbali ndani na nje ya Wizara. Aidha, hatua itakayofuata baada ya maoni ya wadau ni kuandaa rasimu ya sera na mkakati wa utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza kuwa, mchakato huu wa kupokea maoni ya wadau ukamilike haraka ili Rasimu ya Sera hiyo itoke mapema kwa manufaa ya Taifa hili na ustawi wa wananchi.

**Mpango wa Serikali wa kuandaa Mkakati wa kuendeleza Madini (Mineral Development Strategy-MDS)**

**Mheshimiwa Spika,** Mkakati wa Uendelezaji wa Sekta ya Madini (MUSM) ni mpango utakaosaidia kuiongoza Serikali kuchukua hatua stahiki zinazolenga kukuza na kudumisha ukuaji wa Sekta ya Madini. Lengo ni kuliwezesha Taifa kupata manufaa makubwa zaidi kutoka kwenye Sekta ya Madini. Aidha, Mkakati huu unalenga kuhakikisha uwajibikaji na kuweka mipango itakayowezesha kuendeleza shughuli za uchimbaji na biashara ya madini kwa tija.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini Wizara haina Mkakati huu ambao ni nyenzo muhimu sana katika kuhakikisha wananchi wananufaika na rasilimali hii muhimu na hivyo kuleta ustawi kwao ambao ndiyo msingi Mkuu wa uwepo wa Serikali. Kwa sasa Wizara imeunda timu ya wataalam inayohusisha taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa kuzingatia taaluma mbalimbali pamoja na Mpango kazi wa utekelezaji wa Mpango huo. Ni Rai na matarajio ya Kamati kuwa kazi hii itafanywa kwa haraka na kwa ufanisi ili kukuza na kudumisha ukuaji wa Sekta ya Madini nchini kwa manufaa ya nchi na watu wake.

**Hali ya Uendeshaji wa Masoko ya Madini nchini;**

**Mheshimiwa Spika,** Matarajio makuu ya uanzishwaji na uwepo wa masoko ya madini nchini ni pamoja na kusaidia wachimbaji wadogo kupata uhakika wa huduma ya masoko kwa madini yao, upatikanaji wa bei stahiki za madini yanayouzwa na wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa madini; Uwazi katika biashara ya madini; Upatikanaji wa mapato stahiki ya Serikali kupitia tozo za mrabaha na ada ya ukaguzi kutokana mauzo ya madini kwenye masoko; Upatikanaji wa takwimu sahihi za uzalishaji na mauzo ya madini yanayozalishwa na kuuzwa na wachimbaji pamoja na wafanyabiashara wa madini nchini kupitia masoko na Kupungua kwa matukio ya utoroshwaji wa madini nchini kutokana na kuanzishwa kwa mfumo rasmi unaorahisisha biashara ya madini kufanyika nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa, kuanzia mwezi Machi, 2019 hadi kufikia mwezi Juni, 2022 usimamizi wa masoko ya madini nchini

umeendelea kuimarika ambapo kiasi cha kilogramu 51,539.61 za dhahabu; karati 58,747.78 za madini ya almasi; kilogramu 606,253.82 za madini ya bati; kilogramu 284,670.66 na karati 344,370.28 za tanzanite; na kilogramu 10,985.79 na karati 65,033.72 za madini ya vito mbalimbali kiliuzwa kupitia masoko hayo na kuipatia Serikali jumla ya Shilingi bilioni 422.32.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umegundua kuwa, mchango wa mapato yatokanayo na masoko ya madini umeongezeka kutoka asilimia 2.62 toka kuanzishwa kwake hadi kufikia asilimia 28.36 katika Mwaka wa Fedha 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 25.74. Kamati inaipongeza sana Wizara kwa jitihada hizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa jitihada hizi kwani zitasaidia katika kuhakikisha Taifa na wananchi kwa ujumla wananufaika na rasilimali ya madini.

**Hali ya Kiwanda cha kusafisha dhahabu nchini (Mwanza Gold Refinery)**

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha kusafisha dhahabu kilichopo Mwanza ni miongoni mwa viwanda vikubwa vya kusafisha dhahabu katika bara la Afrika. Kiwanda kipo chini ya Kampuni ya ubia ya Mwanza Precious Metals Refinery Ltd ambayo inamilikiwa na STAMICO kwa asilimia 25 na wabia (kampuni za Rozela ya Dubai na ACME ya Singapore) wanaomiliki asilimia 75. Kwa mujibu wa mkataba hisa za STAMICO zitaongezeka hadi kufikia asilimia 30 baada ya miaka mitano na baada ya hapo hisa hizo zitakuwa

zikiongezeka kwa asilimia 5 kila baada ya miaka miwili hadi kufikia asilimia 51 (*majority shareholder)* na wabia kuwa na asilimia 49.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa kiwanda hiki ulianza rasmi tarehe 15 Machi, 2020 na kukamilika mwezi Desemba 2020 kwa gharama ya dola za Marekani milioni 7.2 Kwa sasa miundombinu wezeshi ya kuendesha kiwanda tayari imekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha awali cha majaribio (Aprili hadi Juni, 2021) kiwanda kilinunua dhahabu halisi (*pure gold*) kiasi cha kilogramu 146.85 zenye thamani ya dola za Kimarekani Milioni 8.5. Aidha, kiwanda kilinunua kilogramu 24 za madini ya fedha zenye thamani dola za Kimarekani 17,760 kutoka kwa wachimbaji wadogo, madalali (*dealers*/*brokers*) na wafanyabiashara kutoka Jamhuri ya Afrika ya Kati. Dhahabu kutoka Afrika ya Kati ni gramu 7,472.11 ambayo thamani yake ni Shilingi milioni 519.4. Hii ni ishara njema kuhusu upatikanaji wa dhahabu kutoka nje ya nchi na imeongeza uzalishaji wa kiwanda.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo Kamati imebaini kuwa Kiwanda kilisimamisha uzalishaji wake mwezi Agosti 2021 kutokana na kukosa ithibati kwani Ili bidhaa inayozalishwa iweze kutambuliwa katika masoko ya Ndani na Nje ya Nchi ni lazima ikidhi vigezo vya kimataifa yaani 'International Organization for Standardization (ISO)'. Taarifa ya Wizara ya mwezi Januari, 2023, inaonesha imekamilisha hatua 3 kati ya 6 zinazotakiwa katika mchakato wa kupata Ithibati. Aidha, inatarajiwa

kuchukua hadi miezi minne kuanzia sasa kukamilika kwa hatua zilizobaki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwepo kwa mkanganyiko wa wabia kusimamisha uzalishaji ili kupisha zoezi la Ithibati, uhalisia zoezi la Ithibati liende sambamba na kufanyika kwa uzalishaji. Pamoja na uchelewaji wa upatikanaji wa Ithibati kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa malighafi endelevu na ya kutosha kwa ajili ya kiwanda hivyo kuchelewesha wakaguzi wa kiwanda ambao wanatakiwa kuendelea na hatua za ukaguzi wakati kiwanda kinaendelea kufanya kazi ya kusafisha dhahabu.

**Mafanikio na changamoto za utoaji na upatikanaji wa huduma kwa jamii (Corporate Social Responsibility)**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini imepewa Jukumu la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mipango ya Wajibu wa Kampuni kwa jamii (CSR) kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu cha 22(u) cha Sheria ya Madini Sura 123[3]. Kifungu hiki kinamtaka mmiliki wa leseni ya madini kila mwaka kuandaa Mpango unaoaminika (*Credible CSR Plan*) ambao umekubaliwa kwa pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushauriana na Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na Waziri anayehusika na masuala ya fedha. Mpango unatakiwa kuzingatia mambo ya mazingira, kijamii, kiutamaduni na kiuchumi kwa kutoa kipaumbele kwa jamii inayozunguka mgodi.

---

[3] https://www.madini.go.tz/media/Miscellaneous-amendment-no.-7-of-2017-clean-copy-final-Hansard-CHAPA.pdf

**Mheshimiwa Spika,** tangu Sheria ya Madini, Sura 123 ilivyofanyiwa maboresho na kuwekewa kifungu cha 105 ambacho kinaelezea utaratibu mzima wa kuandaa na kutekeleza mipango ya wajibu wa kampuni kwa jamii, kumekuwa na mafanikio ikilinganishwa na kipindi cha nyuma ambapo kampuni zilikuwa zikiwajibika kwa jamii kwa utaratibu wanaojiamulia. Takwimu zinaonesha kuwa, tangu kufanyika kwa maboresho hayo, zaidi ya Shillingi Bilioni 33.5 zimetumika katika miradi mbalimbali iliyotekelezwa na wamiliki wa leseni za madini katika mikoa mbalimbali hapa nchini wakiongozwa na Mgodi wa Dhahabu wa Geita ambao umetumia zaidi ya Shilingi Bilioni 13.6 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 8.

KIELELEZO NA. 7: Kiasi kilichotumika kwa CSR kwa baadhi ya Migodi nchini kwa Kipindi cha 2019 - 2022

| MGODI | KIASI CHA FEDHA ZA CSR |
|---|---|
| Geita Gold Mining Limited | 13,613,937,674.00 |
| North Mara Gold mine Limited | 6,841,743,931.00 |
| Williamson Diamonds Limited | 204,604,960.00 |
| Bulyanhulu Gold Mine Limited | 6,339,393,000.00 |
| Pangea Minerals Limited | 5,380,880,226.93 |
| Mantra Tanzania Limited | 143,805,200.00 |
| Dangote Cement Limited | 523,752,415.00 |
| Uranex (Tanzania) Limited | 18,752,000.00 |
| Busolwa Mining Limited | 15,050,000.00 |
| Cata Mining Company Limited | 48,496,454.50 |
| Lake Cement Limited | 148,552,346.00 |
| Shanta Mining Company Limited | 184,535,900.00 |
| Zem Development (T) Co. Limited | 46,455,000.00 |
| JUMLA | 33,509,959,107.43 |

Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Madini Oktoba 2022

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyoelezwa, Kamati imebaini changamoto kuu mbili ambazo zimekuwa ni kikwazo katika utekelezaji wa CSR:-

Baadhi ya Halmashauri kutotekeleza Miradi kwa Wakati hasa zenye migodi mikubwa na hivyo kusababisha uaandaaji wa mpango wa miaka inayofuata kuwa mgumu kutokana na sera ya kampuni ya usimamizi wa fedha; na

Uelewa Mdogo wa baadhi ya Kampuni za Madini juu ya wajibu wa Kampuni kwa jamii hasa wamiliki wa leseni za uchimbaji wa kati na mdogo. Kampuni nyingi zimekuwa zikiona suala la uwajibikaji kwa jamii ni suala la hisani hivyo kutofuata matakwa ya Sheria.

**Hatua iliyofikiwa katika kuandaa Kanuni za huduma kwa jamii (*Corporate Social Responsibility Regulations*)**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikishauri juu ya umuhimu wa kuandaliwa kwa Kanuni za Huduma za Jamii ili kuhakikisha kunakuwa na mwongozo sahihi wa utoaji wa huduma kwa Jamii zinazozunguka migodi.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa utekelezaji wa Sheria kuhusu CSR kumejitokeza changamoto mbalimbali na hivyo kusababisha tofauti za kimaendeleo ikiwa ni pamoja na namna bora ya matumizi ya fedha hizo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona ipo haja ya kuwa na kanuni zitakazosimamia masuala ya CSR ili kuboresha na kuweka usawa kwenye matokeo ya utekelezaji miradi hiyo Kamati imearifiwa kuwa

Wizara imekamilisha Rasimu ya Kanuni za Madini (Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii) za Mwaka 2022. Uandaji wa Rasimu ya Kanuni tajwa umezingatia matakwa ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009 ambayo, pamoja na mambo mengine, inaelekeza umuhimu wa kuimarisha ushiriki wa jamii katika miradi ya madini na kuhimiza kampuni za madini kuongeza uwajibikaji kwa jamii. Aidha, Rasimu ya Kanuni husika imetungwa kwa mujibu wa Kifungu cha 129 cha Sheria ya Madini, Sura 123 kinachompa mamlaka Waziri wa Madini ya kutunga kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kuzipitia Kanuni hizo ambazo ni muhimu kwa kuwa zinalenga kuondoa mapungufu yaliyokuwepo katika utekelezaji kwenye eneo la wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii (CSR) kwa watekelezaji ikiwa ni sehemu ya matakwa ya Sheria ya Madini, Sura 123. Ni Rai ya Kamati kuwa wadau wote muhimu wapate fursa ya kuzipitia na kutoa maoni yao kabla ya kuzitangaza.

**Hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa miradi ya madini yenye ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi nchini**

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi yenye ubia baina ya Serikali na Sekta binafsi nchini unafanywa kwa mujibu wa sheria ya Madini, Sura ya 123 kupitia Kifungu cha 10 ambayo inatoa nafasi kwa Serikali kushiriki katika miradi ya uchimbaji madini kwa miradi yenye leseni za uchimbaji wa kati na uchimbaji mkubwa, kwa kumiliki hisa huru au zisizolipiwa (*Non dilutable free Carried Interest*) zisizopungua asilimia 16. Kufuatia matakwa hayo ya kisheria, Kamati ya

Kitaifa ya Majadiliano (GNT) na Kamati ya Majadiliano ya Wizara ya Madini (MMTC) zimefanya majadiliano na baadhi ya wawekezaji na kukubaliana kuhusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na hisa katika miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Tayari Serikali kupitia Wizara ya Madini na Msajili wa Hazina imetia saini Mikataba (*Framework agreements*) ya ushiriki kwenye miradi sita (6) ya uchimbaji mkubwa wa madini. Utiaji saini huu ulipekea kuundwa kwa kampuni hizo na umiliki wa hisa na hatua za utekelezaji wake ni kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.9

KIELELEZO NA. 8: Hali ya Umiliki wa Hisa na Hatua za utekelezaji wa Miradi ya Ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi

| KAMPUNI | % SERIKALI | % MWEKEZAJI | HATUA YA UTEKELEZAJI ILIYOFIKIWA |
|---|---|---|---|
| Twiga Corporation Ltd | 16 | 84 | Mgodi unaendelea na uzalishaji. |
| Tembo Nickel Corporation LTD | 16 | 84 | Mradi unaendelea na hatua ya ukamilishaji wa Mapitio ya Taarifa ya Upembuzi Yakinifu na Uthaminishaji, ulipaji wa fidia na uhamishaji wa wanachi watakaopisha mradi. Vilevile, taratibu za kupata eneo la ujenzi wa Mitambo ya Kusafisha Madini (Kahama Multi Element Refinery Plant) zinaendelea kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Kahama. Uzalishaji wa madini ya nickel unatarajiwa kuanza katika robo ya nne (4) yam waka 2025. |
| Sotta Mining Corporation Ltd | 16 | 84 | Mradi unaendelea na hatua ya ujenzi wa mgodi, uthaminishaji, ulipaji wa fidia na uhamishaji wa wananchi watakaopisha mradi. |
| Faru Graphite Corporation LTD | 16 | 84 | ujenzi wa Mgodi na kufanya mapitio ya mpango wa uthaminishaji, ulipaji wa fidia na uhamishaji wa wananchi watakaopisha mradi. |
| Williamson Diamonds LTD | 37 | 63 | Mgodi unaendelea na uzalishaji. |
| Nyati Mineral Sands LTD | 16 | 84 | Mradi umetolewa leseni Mwezi Oktoba, 2022 na unatarajia kuanza shughuli za ulipaji wa fidia na uhamishaji wa wanachi watakaopisha mradi kabla ya kuanza ujenzi wa Mgodi. |

Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Madini na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua mbalimbali zilizofikiwa za utekelezaji wa miradi hii, Kamati

imebaini uwepo wa changamoto kuu mbili zifuatazo:-

Kutokamilika kwa wakati kwa baadhi ya mikataba ya kikodi baina ya Serikali na Wawekezaji hali iliyosababisha kuchelewa kwa ujenzi wa miundombinu ya migodi kwa baadhi ya miradi; na
Kuchelewa kuhuisha taarifa za upembuzi yakinifu (feasibility study) kwa baadhi ya miradi kulingana na hali halisi ya sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini vilevile kuwa jumla kuna Kampuni mbalimbali zinazomiliki leseni za uchimbaji wa Kati na uchimbaji Mkubwa na zinapaswa kuingia kwenye mfumo wa majadiliano kwa lengo la kuiwezesha Serikali kuwa na hisa. Hata hivyo, majadiliano kati ya Serikali na Kampuni hizi unakwenda taratibu sana. Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia bora itakayowezesha majadiliano kufanyika katika kipindi kifupi ili kukidhi matakwa ya Sheria na hatimaye Taifa kuweza kufaidika.


**Hali ya uzalishaji wa Madini ya Almasi Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu za uzalishaji na usafirishaji wa madini ya almasi hapa nchini zilianza kutunzwa katika kanzidata ya *Kimberley Process Certification Scheme* (KPCS) kuanzia mwaka 2004 baada ya Tanzania kujiunga na mfumo wa usimamizi na udhibiti wa biashara ya madini ya almasi ghafi ili kuzuia uwezekano wa almasi kutumika kugharamia vita. Mfumo huu ulianzishwa mwaka 2003 na umeweka miongozo na matakwa ya kimataifa ambapo kila nchi mwanachama inatakiwa kutimiza

katika kusimamia uzalishaji na biashara ya madini ya almasi ghafi.

**Mheshimiwa Spika,** kiasi cha madini ya Almasi kilichozalishwa na Kampuni ya Williamson Diamond Ltd (WDL), El-Hillal na Wachimbaji wadogo kuanzia Mwaka 2004 hadi kufikia 2021 ni kiasi cha karati 3,907,315.44 zenye thamani ya dola za marekani 789,215,555 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 10. Aidha, Mgodi wa kampuni ya WDL ambao unasifika kwa uzalishaji wake wa almasi za kipekee za rangi ya pinki kwa kipindi cha miaka mitano umezalisha jumla ya karati 139.93 zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 48.4.

KIELELEZO NA. 9: Hali ya Uzalishaji wa Madini ya Almasi Nchini kuanzia 2005 - 2022




Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Madini ya Oktoba 2022 na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa ujumla uzalishaji uliongezeka kuanzia mwaka 2016 hadi 2019 katika mgodi wa almasi wa kampuni ya WDL kutokana na matengenezo yaliyofanyika katika mtambo wake wa uzalishaji, ambapo almasi ndogondogo zenye ukubwa wa chini ya milimita 1 ziliweza kuzalishwa. Vilevile hisa za Serikali zimeongezeka kutoka asilimia 25 hadi asilimia 37.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini uwepo wa changamoto zifuatazo:
Kupungua kwa uzalishaji kulikosababishwa na kusimama kwa uzalishaji katika mgodi wa kampuni ya *El-Hillal Minerals Limited* kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019 hadi sasa, ambapo mgodi huo ulikuwa ukichangia takribani asilimia 2 hadi 3 ya uzalishaji wa almasi nchini kwa mwaka;

Kuongezeka kwa almasi zinazotengenezwa kwenye maabara (*lab grown diamond)* mwaka 2018 kunaashiria vihatarishi vya kupungua kwa uwekezaji wa uchimbaji wa almasi halisi (*natural diamonds*); na

Kusimama kwa uzalishaji wa almasi kwenye mgodi wa kampuni ya Williamson Diamond Limited (WDL) kuanzia mwezi Aprili 2020 hadi Agosti 2021, ili kuhifadhi ukwasi wake baada ya bei ya almasi kuporomoka kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO 19.

**Hali ya uzalishaji wa Gesi ya Helium nchini**
**Mheshimiwa Spika,** moja ya sifa ya gesi ya *helium* ni kuwa gesi ya pili nyepesi kuliko gesi zote baada ya

gesi ya *hydrogen*. Kutokana na kuwa na sifa hiyo, gesi hii ndiyo inayotumiwa zaidi katika vyombo vya anga, kama vile *rockets, helicopter* na maputo mbalimbali yanayorushwa angani kwa ajili ya utafiti. Mbali na matumizi hayo, gesi ya *helium* hutumika kuendesha mashine za utabibu zijulikanazo kama *MRI scanners*, pia hutumika katika teknolojia ya kutengeneza vifaa vya maabara, mitambo ya nyuklia na vifaa vya kieletroniki.

**Mheshimiwa Spika,** gesi ya *helium* imegunduliwa katika eneo la bonde la Rukwa. Kwa mujibu wa makadirio yaliyofanyika, inaonesha kwamba gesi ipo kwa kiasi kisichopungua futi za ujazo bilioni hamsini na nne (54cf). Aidha, gesi iliyogunduliwa ina uwezo wa kujaza cylinders za gesi milioni 1.2 za mashine za MRI. Tayari jumla ya leseni 34 za utafutaji wa gesi ya *helium* zinazomilikiwa na Kampuni Rocket, Antares, Infinite Reserves na Kampuni ya *Helium* One kupitia Kampuni zake tanzu za Njozi, Stahamili na Gogota na leseni 12 za uchimbaji mdogo wa gesi hiyo zinazomilikiwa na Bi. Sarah S. Masasi zimeshatolewa katika Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Arusha, Songwe, Simiyu, Manyara, Singida na Dodoma. Aidha Kampuni ya *Helium One Limited* ilianza kufanya uchorongaji mwaka 2018 kwa lengo la kupata kiasi halisi kilichopo katika maeneo ya leseni ili uchimbaji uanze rasmi. Inatarajiwa uzalishaji, kuanza rasmi mwaka 2025 endapo shughuli za utafiti zitakamilika kama ilivyopangwa na Kampuni ya *Noble Helium Limited* katika maeneo ya bonde la Rukwa, Ziwa Nyasa na Eyasi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa takribani asilimia 40 hadi 50 ya gesi ya *helium* duniani huzalishwa nchini Urusi na uwepo wa mgogoro kati ya Urusi na Ukraine huenda ukachochea ongezeko la mahitaji ya gesi hii kutoka katika vyanzo vingine ikiwemo Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri inayafanywa katika kuendeleza rasimali hii, Kamati imebaini changamoto zifuatazo:-

Uendelezaji wa leseni za gesi ya Helium zilizopo kwenye maeneo ya hifadhi unakumbwa na changamoto ya Sheria ya uhifadhi kutumia utaratibu usiofanana na Sheria ya Madini katika kupata ridhaa ya kufanya shughuli za utafutaji katika maeneo hayo; na
Leseni za gesi ya helium zilizopo kwenye maeneo ya mabonde kumekua na mgogoro wa mwingiliano wa shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

**Utendaji wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) ilijiwekea jumla ya malengo saba (7) ya kutekeleza katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyoainishwa katika Mpango Mkakati wake wa Miaka Mitano (2020/2021 - 2024/2025. Utekelezaji wa malengo haya saba unajumuisha suala la ukusanyaji wa maduhuli kiasi cha Shilingi Bilioni 2. Aidha, GST imepangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 11.6 kutoka katika makusanyo yake.

**Mheshimiwa Spika,** kufikia Septemba 2022, GST ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni 2.5 sawa na asilimia

21.5 ya bajeti yote ya Wizara kwa Mwaka 2022/203. Fedha hizi zimewezesha GST kutekeleza baadhi ya majukumu yake iliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri inayofanywa na GST, Kamati imebaini uwepo wa changamoto zifuatazo:-

Upungufu wa wataalamu katika kada za kemia, jiolojia, TEHAMA na uhandisi jiolojia. GST ina kadirio la uhitaji wa idadi ya kada ya kemia (5), jiolojia (12), TEHAMA (4) na uhandisi jioloji (fundisanifu 14);

Mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa taarifa na takwimu zinazozalishwa na kukusanywa na Taasisi kutoendana na mabadiliko ya haraka na ukuaji wa teknolojia;

Upungufu wa vitendea kazi kama vile magari na zanatepe (sotwares) kwa ajili ya uchakataji na uhakiki wa taarifa na takwimu za jiosayansi, miundombinu ya kanzidata na vifaa vya ugani; na

Ufinyu wa bajeti katika kukamilisha uanzishwaji wa ofisi za kanda za GST ili kusogeza huduma kwa wadau.

**Utendaji wa Kituo cha Jeomolojia nchini (TGC)**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Kituo kilipanga kutekeleza majukumu mbalimbali. Ili kuwezesha kutekeleza majukumu haya, Kituo kiliidhinishiwa na Bunge Shilingi Milioni 595. Kufikia Septemba, 2022, Kituo kimepokea jumla ya Shilingi Milioni 166 sawa na asilimia 28 ya fedha

iliyoidhinishwa na Bunge kiasi ambacho kimewezesha Kituo kutekeleza baadhi ya majukumu yake iliyojipangia. Aidha, kwa upande wa makusanyo ya maduhuli, Kituo kilipanga kukusanya jumla ya Shilingi Milioni 250. Kufikia Septemba 2022 kiasi cha Shilingi Milioni 166 kilikuwa kimekusanywa sawa na asilimia 66.7.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi zilizofanywa na Kituo, Kamati imebaini uwepo wa changamoto zifuatazo:-

Ukosefu wa watumishi wa kutosha kwani watumishi wengi wameajiriwa kwa ajira za mikataba ya muda mfupi;

Kituo kutoanzishwa kisheria (*Establishment Order*); na

Ufinyu wa miundombinu yakiwemo mabweni ya kulala wanafunzi na upungufu wa vitendea kazi kama magari.

**Hali ya umiliki wa Kitalu C Mererani na hatua iliyofikiwa katika uendelezaji wa shughuli za uchimbaji katika leseni hiyo.**

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya *Franone Mining & Gems Limited (FMGL)* ilipata leseni rasmi tarehe 28 Julai, 2022 baada ya kukamilika kwa hatua mbalimbali ikiwemo Tume ya Madini kujiridhisha na uwezo wa Kampuni. Hatua hii ilitokana na Kampuni za awali yaani Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* na Kampuni ya *TanzaniteOne Mining Limited (TML)* zilizopewa leseni za uchimbaki katika eneo hili

kutojiendesha kwa Tija na kuwa na manufaa madogo kwa Serikali hali iliyopelekea mradi kusimama mnamo Novemba, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** hatua mbalimbali zimechukuliwa kuhakikisha mgodi unafanya kazi vizuri. Baadhi ya hatua zilizofikiwa ni pamoja na:-

Kuboreshwa kwa miundombinu ya mgodi kwa ujumla wake kama vile (*main shaft)*, marekebisho ya reli kwa ajili ya kuruhusu kiberenge kupita;

Kufungwa kwa mitambo mipya inayotumia teknolojia ya kisasa ya uendeshaji wa mgodi ;

Kuboreshwa kwa mifumo ya umeme ikiwa ni pamoja na kusimikwa kwa kangavuke kubwa mbili zenye ukubwa wa KV350, transfoma ya ukubwa wa KV 500 na njia mpya ya umeme kwa kujenga kituo kidogo cha kupokelea umeme *(sub-station)* unaotumika katika mgodi huo pekee katika kuendesha mitambo ya shughuli za uchimbaji madini; na

Kufungwa kwa mifumo ya utoaji wa maji, udongo na hewa.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia maboresho hayo, Kampuni imefanikiwa kuzalisha jumla ya kilo 7.42 za madini ya Tanzanite yaliyokuwa na *grades* tofauti yenye thamani ya Shilingi 88,145,721.49 ambapo Serikali itapata mapato ya jumla ya Shilingi 6,170,250. Kamati inashauri matokeo haya iwe chachu ya uendelezaji wa muda mrefu wa madini ya *Tanzanite* kwa kuwekeza zaidi kwenye utafiti wa chini ya ardhi

unaofanyika sasa (*underground mineral exploration*) ili kuweza kupata njia bora zenye uzalishaji mkubwa.

Kutokana na umuhimu wa kitalu hiki, na kwa kuzingatia upekee wa Madini ya Tanzanite Ulimwenguni, Serikali iharakishe majadiliano na mmiliki wa Leseni ya kitalu hiki ili kuliwezesha Taifa kuweza kumiliki hisa kama ambavyo sheria ya madini inaagiza.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini changamoto zifuatazo:-
Kukatika mara kwa mara kwa umeme wa Gridi ya Taifa hali inayosababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji sambamba na kuendelea kwa utoroshaji wa madini hayo nje ya nchi.

Eneo ambalo liliingizwa kimakosa kwenye ramani ya Kitalu C ugawaji wake ufanyike kwa makini ili usizalishe changamoto ya mitobozano.

**Mpango wa Serikali kuanza Kununua Dhahabu**
**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*) kuanzia mwaka 1990 hadi 1994 iliwahi kununua Dhahabu. Zoezi hilo lilifanyika kwa lengo la kuwezesha *BoT* kuwa na akiba ya dhahabu *(monetary gold reserve)* na pia kununua dhahabu iliyokuwa ikizalishwa kwa wingi na wachimbaji wadogo lakini ilikuwa haina soko na hivyo kuchochea vitendo vya utoroshaji.

**Mheshimiwa Spika,** Madini ya dhahabu hutumika kama dhamana ya kupata na kulipa madeni ya nchi na kuilinda thamani ya fedha ya nchi. Aidha,

inaweza kutumika pia wakati wa misukosuko ya kiuchumi inapoathiri nchi husika na kwamba akiba hiyo *(monetary gold reserve)* hutunzwa katika Benki Kuu ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** BoT ilisitisha kununua dhahabu kutokana na hasara iliyopata iliyosababishwa na kushindwa kuhakiki kiwango cha ubora wa dhahabu kabla ya kununua. Hata hivyo, Taarifa ya hivi karibuni inaonesha kuwa kuanzia Novemba 2022, BoT imeanza ununuzi wa dhahabu baada ya kukamilika kwa Miongozo na Taratibu mbalimbali za ununuzi wa dhahabu hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mafanikio ya Sekta ya Madini nchini, Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuona umuhimu wa kuanza kununua dhahabu ili kuliwezesha Taifa kuwa na hifadhi yake ambayo italisaidia kudhibiti thamani ya fedha yake. Kwa upande wake, Serikali kupitia BoT, imekuwa ikisistiza kuwa ununuzi wa dhahabu utaanza pindi viwanda vya kusafisha dhahabu vitakapoanza kazi na kuweza kusafisha dhahabu kwa ubora wa kiwango cha asilimia 99.99.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini masuala yafuatayo:-
Hadi sasa kuna Viwanda Vinne vya kusafisha Dhahabu hapa nchini, hivyo Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa kunakuwa na mazingira wezeshi yatakayosaidia viwanda vya kusafisha dhahabu kupata dhahabu ghafi kwa ajili ya kusafishwa;

Serikali imepunguza mrabaha wa dhahabu inayouzwa kwenye viwanda kutoka asilimia 6 hadi asilimia 4 jambo ambalo limechochea kuongezeka kwa upatikanaji wa dhahabu;

Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikubaliana kuwa na umoja na sarafu ifikapo mwaka 2024, Kamati inaona ipo haja ya Serikali kufanya jitihada zaidi katika ununuzi wa dhahabu ili kuwezesha Taifa letu kuingia kwenye Umoja huo likiwa na sarafu yenye nguvu/imara.

**Mheshimiwa Spika,** Ni Rai ya Kamati kuwa, dhahabu itakayonunuliwa iwe ni ile tu ambayo imesafishwa kwenye viwanda vyetu na kufikia ubora wa asilimia 99.99

Chanzo, madhara na hatua zilizochukuliwa kutokana na kupasuka kwa Bwawa la tope la Mgodi wa Almasi wa Williamson Diamond Ltd.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 7 Novemba, 2022, ukuta wa Bwawa *(slimes dam)* la Mgodi wa Williamson Diamond ulipasuka na inakadiriwa kiasi cha mita za ujazo milioni 16.8 za tope zilimwagika kutoka katika bwawa hilo na kusambaa kwenye mazingira. Chanzo cha kupasuka kwa ukuta wa bwawa hilo ni udhaifu wa ukuta wa bwawa kutokana na udongo kutoshikana vizuri hali iliyosababisha kujitokeza kwa nyufa ndogondogo (*micro-fractures*) na tetemeko la ardhi lililotokea katika mikoa ya Dodoma na Geita tarehe 7 Novemba, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maelezo yaliyotolewa kuhusu sababu za kupasuka kwa bwawa hilo, Kamati imebainika kuwa mgodi ulishindwa kuchukua hatua madhubuti na kwa wakati ili kudhibiti hatari hiyo. Kupasuka kwa bwawa hilo kumeleta madhara kwa jamii ikiwa ni pamoja na nyumba na mashamba kufukiwa na tope;  kukosekana kwa huduma ya maji kwa matumizi ya nyumbani kwa wananchi waliopo vijiji vya jirani kutokana na bwawa la maji la New Almasi linalotumika kwa matumizi hayo kujaa tope kutoka kwenye bwawa lililopasuka; uchafuzi wa mazingira yaliyo ndani ya leseni ya mgodi; kufungwa kwa baadhi ya njia zinazounganisha eneo moja na jingine zilizokuwa zinatumiwa na wananchi; na kusimama kwa uzalishaji wa mgodi na hivyo kusababisha kukosekana kwa mapato kwa kampuni na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hii, Kamati ilielezwa hatua zilizo chukuliwa na Serikali ikiwa ni pamoja na:-

Kukamilisha ujenzi wa mifereji mbadala ya kuzunguka eneo lote lililofunikwa na tope kwa ajili ya kupitisha maji na pia kuzuia umwagikaji wa tope kwenda kwenye mazingira ya wananchi;
Kukamilisha ujenzi wa barabara kuzunguka eneo lililofunikwa na tope ili kuwezesha kufanya ukaguzi wa eneo husika muda wote;

Kukamilisha ujenzi wa ukuta/tuta katika maeneo yote yenye tope yaliyoanishwa ili kuzuia uwezekano wa tope hilo kutiririka kwenda kwenye mazingira ya wananchi;

Kuimarisha ukuta wa bwawa la *New* Almasi ili kuzuia uwezekano wa kupasuka na tope kusambaa kwenda maeneo ya wananchi;

Kumaliza zoezi la tathmini (*valuation*) kwa eneo lililoathirika na tope kwa ajili ya fidia, ambapo tathmini imefanyika kwa eneo lenye ukubwa wa ekari 558;

Kuendelea kutoa gharama ya pango pamoja na huduma za kijamii (chakula, nguo, posho ya kujikimu, dawa na mahitaji ya shule kwa watoto) kwa wananchi wapatao 145, ambao nyumba zao zimeathiriwa na tope; na

Mgodi kupewa adhabu na *NEMC* ya kulipa faini ya jumla ya Shilingi bilioni moja kutokana na uchafuzi wa mazingira kwa tukio la kupasuka kwa bwawa hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Ni Rai ya Kamati kuwa ili kudhibiti matukio ya kupasuka kwa mabwawa ni vyema kukafanyika ukaguzi wa mara kwa mara kwenye migodi na maeneo ya uchimbaji nchini ili kubaini mapungufu mbalimbali na kuelekeza migodi husika kurekebisha mapungufu hayo. Aidha, kwa wananchi wote walioathiriwa na tope ni muhimu tathmini ifanywe haraka walipwe fidia inayoendana na thamani ya mali zao kwa sasa.

**Yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa Sekta**

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia ufuatiliaji uliofanywa na Kamati kwa Wizara inazozisimamia kwa mujibu wa

Kanuni[4]. Kamati imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zinakwamisha lengo la nchi katika ustawi wa wananchi[5]. Katika ufuatiliaji huo, Kamati imebaini masuala yafuatayo:-

Bajeti za Wizara hazitoki kwa wakati. Kwa mfano kufikia Disemba upatikanaji upo chini ya asilimia 40 kwa Wizara zote mbili;

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo upo nyuma ya muda uliopangwa. Kwa Mfano Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, Rusumo na Kinyerezi I Extension;

Upatikanaji wa Umeme nchini bado hauridhishi kutokana na baadhi ya maeneo umeme kuendelea kukatikakatika;

Utekelezaji wa Miradi ya REA kwa baadhi ya maeneo siyo wa kuridhisha;

Bei ya mafuta kuendelea kuwa juu kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za miundombinu duni katika bandari ya Dar Es Salaam inayochangia meli kuchelewa kushusha mafuta;

Ukosefu wa Maabara za kupima sampuli za mafuta katika bandari ya Tanga na Mtwara;

Kuchelewa kwa mchakato wa kutungwa kwa Sheria ya Jotoardhi;

---

[4] Nyongeza ya nane (7) !1) (d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020

[5] Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya  Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

Kusuasua kwa utoaji na upatikanaji wa huduma kwa jamii (*Corporate Social Responsibility*);

Kupasuka kwa Bwawa la tope la Mgodi wa Almasi wa Williamson Diamond Ltd; na
Mpango wa Serikali kuanza kununua dhahabu

## SURA YA TATU

## MAONI NA MAPENDEKEZO

### Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwaka mmoja wa utekelezaji wa shughuli za Kamati, kumekuwa na mafanikio mbalimbali ambayo Kamati imebaini katika utendaji kazi wa Wizara inazozisimamia. Aidha, Kamati imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali kama zilivyoainishwa ambazo ni muhimu kuziwasilisha ili Bunge lako Tukufu ambalo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndicho chombo kikuu cha uwakilishi wa wananchi katika kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake[6] liweze kuzifanyia maamuzi.

### Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Mafanikio, Changamoto na yaliyobainika katika kipindi cha Februari 2022 hadi Januari 2023, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

[6] Ibara 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

**Mapendekezo ya Jumla**
**Bajeti**
**Mheshimiwa Spika,** KWA KUWA Bajeti zilizoidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini hazitoki kwa wakati kwani kufikia Disemba 2022 upatikanaji upo chini ya asilimia 40 kwa Wizara zote mbili;

NA KWA KUWA moja ya sababu ya kuchelewa kutolewa fedha imeelezwa kuwa ni kuchelewa kuwasilishwa hati za madai na Wakandarasi na mfumo duni wa upitiaji wa hati hizo;

NA KWA KUWA upatikanaji huo wa fedha za bajeti usioridhisha unasababisha Wizara kushindwa kutekeleza kikamilifu majukumu ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi;

KWA HIYO BASI, ili Serikali ihakikishe kuwa fedha zilizoidhinishwa kwa Wizara hizi zinatoka zote na kwa wakati;
Wakandarasi wakamilishe kazi kwa wakati na kuwasilisha hati za madai mapema kwaajili ya malipo; na

Serikali iboreshe mfumo wa kupitia hati za madai za Wakandarasi kuwahisha malipo yao.

**Kusuasua kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, KWA KUWA utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo upo nyuma ya muda uliopangwa ikiwemo Ujenzi wa Bwawa la

Mwalimu Nyerere MW 2115, Mradi wa kufua umeme wa Rusumo MW 80 na Mradi wa umeme wa Kinyerezi I Extension MW 185;

NA KWA KUWA kusuasua kwa utekelezaji wa miradI hii kunasababisha nchi kuendelea kuwa na Uhaba wa Umeme na hivyo shughuli za Kiuchumi kutoteketelezwa kikamilifu;

KWA HIYO BASI, Serikali ihakikishe miradi yote inasimamiwa kwa karibu na inakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

**Wizara ya Nishati**

**Hali ya Upatikanaji wa Umeme nchini**

**Mheshimiwa Spika,** KWA KUWA hali ya upatikanaji wa umeme nchini siyo ya kuridhisha kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za Miundombinu chakavu, Ukame na uhaba wa gesi ya kutosha;

NA KWA KUWA ukosefu wa umeme wa kutosha na uliopo kukatika mara kwa mara kunachangia kukwama kwa shughuli za kiuchumi;

KWA HIYO BASI, Serikali Ihakikishe:-
Mitambo ya kufua umeme kwa gesi inakamilika haraka kama vile Kinyerezi I extension,
Vitalu vya gesi viongezewe uwezo wa kuzalisha na kubuni maeneo mapya ya kuzalisha gesi; na
Fedha zilizotengwa kwaajili ya miradi ya kuboresha umeme zipewe kipaumbele kwa kutolewa mapema ili miradi yote iliyopangwa itekelezwe na kukamilika kwa wakati.

**Kusuasua kwa utekelezaji wa Miradi ya REA**

**Mheshimiwa Spika,** KWA KUWA baadhi ya miradi ya REA imekuwa haikamiliki kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kupanda kwa bei ya vifaa na baadhi ya wakandarasi kuwa na uwezo mdogo wa kiutendaji;

NA KWA KUWA, Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi hii kunasababisha Vijiji kuendelea kukosa umeme na shughuli za kiuchumi kukwama;

KWA HIYO BASI, Serikali ihakikishe:-

Inawasimamia kwa karibu wakandarasi ili miradi iweze kukamilika kwa wakati;

REA inaboreshwea ili iweze kusimamia wakandarasi vizuri;

Kwa lengo la kurahisisha taratibu za manunuzi, wawepo *pre-qualified* wakandarasi ili wakandarasi waliopo wakishindwa wachukuliwe hawa (pre-qualified) ili kuondoa mlolongo wa manunuzi; na

Taratibu za Kimkataba ziangaliwe na kuboreshwa ili wakandarasi wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao wapokonywe miradi bila ya kufuata mlolongo mrefu.

**Bei ya Mafuta**

**Mheshimiwa Spika,** KWA KUWA Bei ya mafuta imeendelea kuwa juu kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za gharama za ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta kutokana na Miundombinu

duni ya Bandari ya Dar Es Salaam na ukosefu wa Maabara katika Bandari za Mtwara na Tanga;

NA KWA KUWA, kupanda kwa bei ya mafuta kuna changia pia Mfumuko wa bei nchini na hivyo kufanya wananchi wengi washindwe kumudu gharama za maisha;

KWA HIYO BASI, Serikali ifanye yafuatayo:-

Iboreshe Miundombinu ya Bandari ya Dar Es Salaam ili kuwezesha upakuaji wa haraka wa mafuta;

Isimamie TBS ili waharakishe ujenzi wa Maabara za Tanga na Mtwara; na

Ikamilishe mapema *Service Level Agreement* (SLA) ili Taasisi zinazohusika ziwajibike kubeba gharama za ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta (*demurrage charges)* na hivyo kumuondolea mzigo mlaji wa mwisho kubeba gharama kupitia bei ya mafuta

**Ukosefu wa Sheria ya Joto ardhi**
**Mheshimiwa Spika,** KWA KUWA Mchakato wa kuleta Muswada wa Sheria ya Joto ardhi umechukua muda mrefu na Kamati hairidhishwi na mwenendo wa utekelezaji wake;

NA KWA KUWA ukosefu wa Sheria unasababisha kusuasua kwa uendelezaji wa rasilimali hii muhimu kwa uchumi wa nchi katika upatikanaji wa umeme kunakosababishwa na wawekezaji kukosa mvuto katika kuwekeza;

KWA HIYO BASI, Serikali iharakishe mchakato huu ili kabla Mwaka 2023 kuisha Muswada huu uje Bungeni na Sheria iweze kutungwa.

**Wizara ya Madini**

**Upatikanaji wa huduma kwa jamii (*Corporate Social Responsibility*)**

**Mheshimiwa Spika,** KWA KUWA kumekuwa na kusuasua kwa utoaji na upatikanaji wa huduma za kijamii kutokana na baadhi ya wenye migodi kuona CSR ni hisani na baadhi ya taasisi za Serikali kuwa na mivutano isiyo na tija katika kufanya maamuzi;

NA KWA KUWA kusuasua huku kunasababisha jamii zinazozunguka migodi kukosa fursa za kimaendeleo na kuendelea kuwa duni;

NA KWA KUWA tayari Serikali imetunga Kanuni za utekelezaji wa CSR ili kuondoa sintofahamu na mivutano katika jamii,

KWA HIYO BASI, Wizara ya Madini ihakikishe inajenga uelewa wa Kanuni hizo kwa wadau wote ili utekelezaji wa CSR uwe na ufanisi.

**Upungufu wa wataalamu katika Sekta ya Madini**

**Mheshimiwa Spika,** KWA KUWA Taasisi nyingi zilizo chini ya Wizara ya madini zina upungufu wa wataalam kama vile STAMICO (50.8%), GST (40%) na TGC (16%);

NA KWA KUWA upungufu wa Wataalam hao unasababisha Taasisi kushindwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa majukumu yao;

KWA HIYO BASI, Serikali itoe kipaumbele cha ajira kwa Watumishi wa Sekta hii ambayo ina mchango mkubwa katika Pato la Taifa ili kufikia 2024 idadi ya watumishi ifikie angalau asilimia 70 (70%).

Kupasuka kwa Bwawa la tope la Mgodi wa Williamson Diamond Ltd.
Mheshimiwa Spika, KWA KUWA kumekuwa na uzembe uliosababisha Bwawa la tope la Mgodi wa Almasi wa Williamson Diamond Ltd kupasuka;

NA KWA KUWA Kupasuka kwa bwawa hilo kumeleta kadhia na athari kwa wananchi ikiwemo kukosa huduma muhimu za kijamii kama vile maji, barabara na nyumba kufukiwa;

KWA HIYO BASI, Serikali ihakikishe:-
Watu wote waliosababisha uzembe wawajibishwe; na Maeneo yote yenye mabwawa ya aina hii Mamlaka husika zihakikishe yanafanyiwa ukaguzi ili kubaini viashiria vya hatari na hatua za haraka zichukuliwe kurekebisha kasoro hizo.

**Mpango wa Serikali kununua dhahabu**
**Mheshimiwa Spika,** KWA KUWA Mpango wa sasa wa Serikali ni kununua dhahabu ghafi kutoka kwa wachimbaji na wauzaji wa dhahabu hapa nchini baada ya dhahabu hiyo kuthibitishwa na kiwanda chenye Mamlaka ya Kimataifa ya kuthibitisha kiwango cha usafi;

NA KWA KUWA Viwanda hivyo vitakavyotumika kuthibitisha usafi wa dhahabu inayokusudiwa

kununuliwa navyo ni wanunuzi wa dhahabu kutoka kwa wachimbaji na wazuaji hao hao;

NA KWAKUWA ili kuepuka kuwepo kwa mgongano wa kimaslahi kati ya BoT na Viwanda husika;

KWA HIYO BASI, Benki Kuu ya Tanzania ijielekeze tu kwenye kununua dhahabu ambayo tayari imesafishwa katika viwanda vilivyopo nchini hadi kufikia ubora wa asilimia 99.99 ya usafi wa dhahabu.

## SURA YA NNE

### HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya kina pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kuhitimisha na kufunga hoja ya Kamati kama ifuatavyo:-

### Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako thabiti. Kamati inaendelea kukuahidi ushirikiano na tunakuombea kila la kheri katika utekelezaji bora wa majukumu yako. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb | - | Mwenyekiti |
| Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| Mhe. Salim Alaudin Hasham, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Amina Bakari Yussuf, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Hamis Mwagao Tabasam, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Salim Mussa Omar, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Robert Chacha MaboTo, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Ameir Abdallah Ameir, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Mohamed Said Issa, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Mwita Mwikabe Waitara, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb | - | Mjumbe |
| Mhe. Martha Festo Mariki, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawapongeza na kuwashukuru sana Waziri wa Nishati Mhe. January Yusuf Makamba (Mb), Naibu Waziri Mhe.Steven Lujwahuka Byabato (Mb), Waziri wa Madini Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Mb) kwa ushirikiano mzuri wanaoipa Kamati wakati wote na hivyo kusaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Pamoja nao Kamati inawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini wakiongozwa na

Makatibu Wakuu wao ambao ni Mhandisi Felchesm Mramba (Katibu Mkuu Nishati) na Naibu wake Ndg. Khery Mahimbali. Pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Madini Ndg. Adolph Ndunguru na Naibu wake Ndg, Msafiri Mbibo.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi (*ndc*) kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu bila mkwamo wowote. Aidha, namshukuru sana Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein (*ndc*), Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Chikokoto (*ndc)* pamoja na Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Pamela Pallangyo, Ndg. Onesmo Laulau na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rukia Shaban kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati.

**Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Dunstan Luka Kitandula, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

Februari, 2023

**MHE. IDDI KASSIM IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono. Wazee wa kubadilisha nembo hawa! Ahsante bwana. *(Makofi)*

Waheshimiwa sasa tunaanza kuchangia na mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Tabasam, halafu Mheshimiwa Neema Gerlad Mwandabila, Mheshimiwa Josephine Gezabuka na Mheshimiwa Nusrat Shaaban wajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami nitoe mchango wangu katika sekta hii ya nishati na madini. Ni kwamba, pamoja na kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, na-*declare interest* kwamba pia mimi ni mfanyabiashara wa mafuta ya reja reja hapa nchini na pia ni mchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Wizara ya Nishati kupitia *TANESCO* na *REA* kuwa wasikivu kwa kukubali kupitia upya mpango wa uunganishwaji umeme majumbani kutoka shilingi 360,000 kurudi shilingi 27,000 katika maeneo maalumu ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni kwamba, kuna miji ambayo inaonesha ni Majiji, Manispaa, lakini Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Miji, wana maeneo yao ambayo yako vijijini. Kwa mfano,

Dodoma hapa kuna maeneo ambayo yako vijijini kabisa, lakini yanasomeka yako katika Jiji la Dodoma. Kuna maeneo yako Mwanza yanaonekana yako Nyamagana, lakini ukitoka Nyamagana kwenda huko ni kilometa zaidi ya 30. Pia kuna maeneo yako kwa mfano Sengerema Mjini, lakini zinasomeka ni Kata za Sengerema Mjini lakini ni kilometa zaidi ya 30 mpaka 60 ndiyo unafika katika maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hili ambalo wamelichukua watu wa Wizara kurudi upya kupitia maeneo haya kwa kutushirikisha Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Madiwani na Wakuu wa Wilaya kupita kwenye maeneo hayo kurudia upya na kushusha bei hizo, tunaipongeza sana Wizara kwa jambo hilo. Naomba waharakishe, wananchi wetu wamekaa, wanasubiri kuunganishiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni umeme unaoenda kuunganisha vijiji na vijiji, wilaya na mikoa. Maeneo haya wana ujenzi wa *transmission*. Haya maeneo miradi iko mingi sana. Kwa mfano, miradi iliyopo tu ni zaidi ya 26, na yote umilikishaji wake hatujui je, ni matatizo ya fedha kutoka Wizara ya Fedha? Hatujui tatizo ni nini? Ni Makandarasi! Sasa tunaomba Wizara ifanye haraka kuharakisha huu ujenzi wa hizi *transmission* unakamilika, wananchi wanaohitaji umeme waweze kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna maeneo ya migodi. Tunaishukuru sana Wizara kwamba kupitia *REA,* migodi yote mikubwa na midogo inaanza kupelekewa umeme. Kwa hiyo, hili

tunaipongeza sana, lakini bado hawajaharakisha upelekaji wa umeme migodini, bado watu wanatumia *diesel.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama kwangu Sengerema tuna ujenzi mkubwa wa Mgodi wa *Sotta Mining*, ni zaidi ya kilometa 38 hadi 40 kufika kule kutokea Sengerema Mjini. Ila iliko *submission* ya *TANESCO* kule Geita kutoka Mpomvu kuja Sengerema ni zaidi ya kilometa 60. Sasa tunaomba watuharakishie kutujengea *line* mpya kwa ajili ya mgodi huo. Kwa sababu mgodi ukishaanza kufanya kazi na umeme haupo, na kuna umeme mwingine, waangalie njia rahisi kutokea Kakola - Geita kupitia Msalala - Karumwa au watoe Geita. Kwa hiyo, tunamwomba Waziri katika jambo hili aharakishe kwenye maeneo ya migodi mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vinasaba limekuwa ni tatizo kubwa katika nchi hii. Tulipiga kelele hapa, vinasaba vilikuwa bei kubwa, *tulizungumza na baadaye vinasaba vikashushwa bei mpaka Shilingi saba kwa cubic meter* za lita za mafuta. Pamoja na hali hiyo, hivi tunavyozungumza uwekaji wa vinasaba unalalamikiwa na wafanyabiashara wa reja reja walioko katika Mikoa. Wao wanatuma madereva wao wanakuja kupakia katika malori, lakini vinasaba vinawekwa kama *seal.* Ni jambo ambalo katika ma-*depot* hawajaweka wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawajaweka wazi kuonesha ma-*depot* yale, lita 7,000 inawekewa miligramu ngapi? Lita 10,000 miligramu ngapi?

Waweke vibao vikubwa. Wakishamaliza kuweka vinasaba, tunaiomba sana Wizara, kwa sababu ni Wizara mbili; Wizara ya Nishati na Wizara ya Biashara na Viwanda ambao wako *TBS,* na wao wafunge *seal.* Kwa hiyo wafunge *seal* watu wa *depot* na watu wa *TBS,* Kwa sababu suala la vinasaba linabeba uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa *dumping* katika nchi hii ni kwamba lazima vinasaba sasa viwekwe kwa *seal.* Halafu vinasaba kutokea huko vinakotoka visindikizwe ama na Jeshi au na watu wa usalama wa Taifa. Jamani suala la vinasaba kuuzwa mitaani ni suala la hatari katika uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *demurrage charges,* Mwenyekiti wa Kamati amelizungumza jambo hili kwa ukubwa kutokana na muda. Hata hivyo, suala la miundombinu toka tunaingia Bungeni hapa tunazungumzia suala la miundombinu. Suala la mafuta limekuwa na changamoto kubwa kwa sababu linachangia Wizara tano. Wizara tano zote hizi zinamulika katika eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wizara ya Fedha. Kwa mfano, kama sasa hivi uagizaji wa mafuta, meli zinafika hapa zinashindwa kulipiwa kwa sababu ucheleweshaji wa Dola kutoka Benki Kuu unakuwa ni tatizo. Tunaiomba sana Wizara ya Fedha iharakishe mpango wa uagizaji mafuta linalobeba uchumi wa nchi. Tunahitaji katika sekta hiyo zaidi ya Dola milioni 700 kwa miezi mitatu. Sasa hili ni jambo ambalo linachangia waagizaji wa mafuta kupata *demurrage*

*charges* kule, nao wanaileta huku kwa mlaji. Mtu wa mwisho anayekuja kuumia ni mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *flow meter* zinasimamiwa na watu wa Wizara ya Biashara. *Flow meter* nne ziko kule Kigamboni, ni mbovu leo mwaka wa nne hazitengenezwi. Hata hivyo, suala la ushushaji wa mafuta linasimamiwa na Wizara ya Ujenzi (Bandari). Sasa pale na penyewe ushushaji wa mafuta…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ya pili hiyo. Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Neema Gerald.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika taarifa hizi ambazo zimewasilishwa; Taarifa ya Kamati ya Ukimwi na taarifa ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba ninayo furaha kubwa kuipongeza Hospitali ya Muhimbili kwa kuanzisha huduma ya Puto. Nadhani niwahamasishe wale watu waliozidi uzito ule uliokithiri, waende wakaweke. Kimsingi tumeona ushahidi kwa Peter Msechu, ndani ya wiki tu amepunguza kilo saba. Kwa hiyo, nawahamasisha sana Watanzania wenzangu, Wabunge wenzagu kutumia hii huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nirejee kwenye hoja zangu za msingi kuhusiana na Kamati ya UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya. Ninarejea kwamba katika Mji wangu wa Tunduma, Mbozi na kanda nzima hii ya barabara ya *Tanzam,* ni moja ya maeneo yanayoathirika sana na masuala ya UKIMWI. Maeneo yote ambayo yana vituo vya ulazaji wa malori, watoto wa maeneo yale wengi wamekuwa wanatumika ndivyo sivyo, wanaharibiwa sana. Sijajua ni kwa nini madereva hawa na makonda wao wamekuwa ni watu wasio na huruma au watu wasiokuwa wa kujali kuangalia kwamba watoto wanaowaharibu ni kizazi kijacho. Kwani wanaweza wakawa wanawaharibu wale, lakini kwa sababu tunachangamana, kwa hiyo, wanapowaharibu wasidhani kwamba watoto wao wanakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu, *TACAIDS* waje na mkakati maalumu wa ku-*control* hawa madereva wanaoharibu watoto wetu kwenye hivi vituo ambako malori yanalala. Kwa sababu kanuni na sheria ndogo ndogo zipo na zinatungwa. Kitendo cha kusababisha uharibifu wa Watoto na kuwasababishia maradhi, ni kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe tu watu wa *TACAIDS* kwenye hili watutazame. Watoto wetu wanaharibika sana, wanaacha shule kisa, Shilingi mia mbili mia mbili wanazokuwa wanapewa. Kwa hiyo, kwa hili naomba pia waweze kuliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona miradi mingi imelenga kuwasaidia wale wanaojiuza, wale ambao wanafanya ushoga na vitu kama hivyo, lakini kuwatazama wale watoto wanaotoroka shuleni na kwenda kuwakimbilia wale wa malori wapate chochote kwa sababu aidha ya njaa na nini miradi mingi katika maeneo hii haijazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendelee kuipongeza Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya kwa namna ambavyo imekuwa ikiendelea kupamba na tumekuwa tukiona Kamishna wa madawa ya kulevya ambavyo amekuwa akiendelea kutoa taarifa mbalimbali kwamba wamekamata dawa kwa kiwango gani na ni watu gani wanahusika, japo wengine wamekuwa wanakasirika wakitajwa lakini ukweli ni kwamba madawa ya kulevya ni kitu ambacho kama nchi tumeendelea kukipinga na hatukitaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kusema nini kwenye upande wa madawa ya kulevya kwamba waraibu ni watu ambao kwa namna moja au nyingine tuna wa-*term* kama ni waathirika, ni watu ambao wameshakuwa dhaifu hawawezi kujitegema kiuchumi bila kuwa-*supported,* sasa mpaka saa hizi hatujaona mkakati ambao upo wa kuhakikisha kwamba katika kila Halmashauri kumekuwa na mratibu wa masuala ya madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Halmashauri ndiyo kiungo cha Serikali Kuu na kule wananchi chini, kwa hiyo watusaidie kuweza kupata Waratibu kwenye Halmashauri zetu ambao

wao watakuwa wanaendelea kusimamia haya masuala ya vilevi na madawa ya kulevya ili kupunguza vijana wetu na watoto wetu kuona kwamba masuala ya vilevi kama fasheni. Kwa sababu wakati mwingine masuala ya uvutaji bangi, masuala ya unywaji wa pombe uliokithiri au matumizi ya madawa ya kulevya yamekuwa yakiambatana na tabia hizi wanazoita tabia za kisasa za kuona kwamba haya mambo ni fasheni. Kwa hiyo, kama tutakuwa na waratibu kule ina maana kwamba watakuwa na programu zao kupitia Halmashauri za kufanya unasihi pia kuweza kufanya hamasa kwenye jamii ya kuzuia matumizi ya madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme tu kwamba nitakuwa sijajitendea haki kama nitashindwa kuongelea kuhusu Wilaya ya Songwe na mradi huu wa *Peak Resources* wa kuzalisha madini adimu ya *magnet* ambayo Tanzania nzima yamepatikana katika Kata ya Ngwala Wilayani Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaliongea hili na kwa uchungu mkubwa nikiiomba Serikali yangu wawape *Peak Resources* leseni, ni miaka minne tangu utafiti umekamilika. Ni kitu gani kinawafanya wao washindwe kutoa leseni kwa *Peak Resources*. Wamekuwa wanafanya majadiliano, makubaliano ni miaka minne ni majadiliano gani hayo yasiyoisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Songwe tunaamini kabisa kama ule mradi ukianza kufanya kazi wanawake wetu wa Mkoa wa Songwe kipato kitainuka. Wataweza kuuza hata mayai, wataweza

kuuza hata kuku. Watusaidie kampuni hii ya *Peak Resources* iweze kupata leseni, maana tumekuwa tunafuatilia amekaa hapa Mheshimiwa Mbunge wa Songwe Mheshimiwa Phillipo Mulugo kila siku analia na hicho kitu, kuna wakati amejibeba toka Songwe kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya kupokea hiyo leseni, lakini bado hiyo leseni hawakuweza kupata, sasa *you can imagine* kwamba ni kwa namna gani alifurahi siku hiyo na ni kwa namna gani siku aliweza kupata huzuni ya kukosa hiyo leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini hakuna mjadala unaoweza kwenda zaidi ya miaka mitano mnajadiliana tu namna ya kufanikisha hilo suala, wakati ni kitu ambacho kina maslahi kwa Taifa! *Imagine magnet* Tanzania nzima inapatikana Songwe, mbona madini mengine wanapewa haraka haraka dhahabu na mengineyo. Hapa nimeona kwamba wanaenda kutoa leseni za *helium why not* katika huu mradi wa *Peak Resources*?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie *forum* hii kuwaomba Serikali watupe leseni kwenye hiyo kampuni ya *Peak Resources* ili madini yaanze kuvunwa. Nitaendelea kuwahamasisha wanawake wa Jimbo langu waione hiyo fursa itakayopatikana kule kulingana na uwepo wa hii kampuni kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikiendelea kufanya kazi zake. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Genzabuke, jiandae Mheshimiwa Nusrati

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hizi mbili. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema kunijalia afya na kunipa kibali cha kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali namna inavyofanya kazi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Januari Makamba, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. Wasichoke waendelee kuwa wabunifu na kuendelea kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafsu hii kumponeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu kipenzi Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyoandika historia Tarehe 22/12/2022 kwa uzinduzi wa ujazaji maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. Nampongeza sana Mama kwa kazi nzuri aliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza kwenye maeneo mawili. Eneo la kwanza, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuandika historia kwa mara ya kwanza mwaka jana kuweza kuwasha umeme wa Gridi ya Taifa katika Mkoa wetu wa Kigoma. Nashukuru sana Mungu aendelee kuibariki Serikali

yetu inayoongozwa na Mama yetu mpendwa kwa kuweza kuukumbuka Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma wakiwemo wanawake tunatoa shukrani nyingi sana kwa kuweza kutuunganisha kwenye Gridi ya Taifa. Mkoa wetu una Wilaya Sita, Wilaya zilizokwisha pata umeme huo ni Wilaya ya Kakonko Kibondo, Kasulu na Buhigwe. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri Januari Wilaya zile ambazo bado hazijapata neema ya kupata umeme huo, kwa maana ya Wilaya ya Kigoma Vijijini, Kigoma Mjini na Uvinza nazo ziweze kunufaika kwa kupatiwa umeme pindi itakapowezekana, kwa sababu tukipata umeme watu wa Kigoma tutaweza kuzalisha na kuweza kuwahamasisha wawekezaji waje kuwekeza katika Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu tayari umefunguka kwa sababu barabara zinaendelea kujengwa na tukipata umeme tutaweza kukimbia sawasawa na wenzetu ambavyo wamekuwa wakikimbia. Kwa mara ya kwanza umeme ule ulipokuja changamoto kidogo huwa hazikosi, ulikuwa unakatika katika lakini kwa sasa kutokana na jinsi Serikali inavyoendelea kuimarisha miundombinu nafikiri tutaenda vizuri tutaondokana na kukatika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya miradi ya umeme, miradi yake inatekelezwa kwa kusuasua nilikuwa ninaomba sasa, Serikali ijitahidi kuhakikisha miradi inakamilika. Kwa mfano, mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, mradi wa Rusumo na mradi wa

Kinyerezi. Miradi hiyo ikikamilika itatusaidia sana kwa sababu umeme utakuwa ni wa uhakika na ninyi mnafahamu kabisa umeme ukikatika katika hatuwezi kufanya shughuli za uzalishaji kwa maana hiyo basi umeme huo wa miradi hiyo mikubwa ukikamilika utaweza kutusaidia kuondokana na tatizo la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Bwawa la Mwalimu Nyerere lingekuwa limeshakamilika sasa kwa vile mmeongezewa muda mjitahidi kuhakikisha mradi huo unakamilika mara moja. Pia, nilikuwa ninashauri upande wa *REA*, baadhi ya miradi ya *REA* imeshindwa kukamilika kwa wakati hali inayosababisha vijiji vingi kukosa umeme, kumekuwa na malalamiko wakati mwingine kwamba kuna ukosefu wa vifaa kwa ajili ya kuunganishia umeme, naomba Serikali ijitahidi kuwasimamia wale Wakandarasi ambao walichukua kazi maeneo mbalimbali ili waweze kukamilisha kazi kwa wakati na kuweza kuwaondolea wananchi wetu adha ya ukosefu wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba niendelee kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya, ninaamini mkifanya kwa kudhamiria tutaweza kuondokana na tatizo la umeme. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Nusrat, jiandae Mheshimiwa Issaay, jiandae Mheshimiwa Iddi Kassim Idd.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye taarifa ya Kamati ya UKIMWI lakini taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, lakini nitachangia maeneo mawili kwenye Kamati ya Nishati na Madini, upande wa nishati na upande wa madini na muda ukibaki nitachangia jambo la tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza upatikanaji wa umeme katika *Grid* ya Taifa nchini, kwa ujumla ukweli uhitaji wa umeme kwenye nchi yetu ni mkubwa sana ukilinganisha na umeme ambao tunao. Labda nitaje vyanzo vya umeme ambavyo vina-*feed* kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo kikubwa kinacho-*feed* Gridi ya Taifa kinachoongoza ni gesi asilia ambayo ni asilimia 62 ambayo ni megawati 1,103 lakini kuna umeme wa maji megawati 574 sawa sawa na asilimia 32 lakini kuna chanzo cha mafuta ambayo ni megawatit 88.13 sawasawa na asilimia 4.96 lakini umeme kutokana na tungamo taka ambayo ni megawati 10.50 sawasawa na asilimia 0.57 ambayo inatengeneza jumla ya megawati 1,777 ambayo ni asilimia 100 ya umeme wetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za Serikali tumeziona kwa sababu mradi wa umeme wa Mwalimu Nyerere unaweza kwenda kutengeneza megawati 2,115 ambayo itaongeza nguvu kwenye Gridi ya Taifa kufikia megawati 3,892.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetaja takwimu hizi ili tuone namna ambavyo bado tunauhitaji mkubwa wa umeme kwenye Taifa, na ni lazima watu wafahamu kwamba pamoja na miradi, huu ni mradi mkubwa kabisa ambao nimeutaja kwa sababu ni mradi ambao ni *flagship* ni mradi ambao ni wa kimkakati na ni mradi ambao wote tumetolea macho huko, lakini bado hata tiukipata megawati hizi bado uhitaji wa umeme ni mkubwa sana kwa sababu tunategemea umeme nchi nzima, kuna biashara, kuna maisha ya kawaida ya Watanzania kwa hiyo uhitaji bado ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni miongoni mwa watu wanaoamini katika nishati jadidifu ikiwemo mradi wa Mwalimu Nyerere ndiyo maana tunaushikia bango kwamba mradi wa Mwalimu Nyerere ni lazima ukamilike, kwa sababu ukikamilika tunaongeza *base-load* kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme kitaalamu ili uzalishe umeme wa nishati jadidifu nyingine kama nishati ya upepo na nishati ya jua ni lazima *base-load* iwe na umeme ambao ni *sufficient* umeme ambao ni wa uhakika na ni umeme wa maji pekee ambao ndiyo umeme pekee wa uhakika dunia nzima. Kwa hiyo, kukamilisha umeme wa Mwalimu Nyerere ni kuongeza *base-load* ili tuweze ku-*feed* kwenye Gridi ya Taifa kwenye umeme mwingine, kwenye nishati jadidifu kwa sbababu kuna madhara mengi sitayazungumza hapa kuhusiana na sasa hivi chanzo cha umeme ambacho kinaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sasa hivi tungekuwa tumekamilisha mradi wa Mwalimu Nyerere kama ambavyo ilitakiwa mwanzo, tungekuwa bado hatuwezi kuutoa umeme pale kwenye mtambo Selous Bwawani kuupeleka kwenye kituo, kwa sababu *transmission line* imefika asilimia 83.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu umeme pale tunaweza tukaona mitambo inafanya kazi lakini kuutoa pale kuupeleka kwenye kituo cha kupoozea umeme kuna *line* inatakiwa ijengwe iko asilimia 83 haijakamilika. Kwa hiyo, kama ile kudra za Mwenyezi Mungu paap maji yamejaa Mwalimu Nyerere hatuwezi kuutoa ule umeme tutabaki tunauangalia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha kupooza umeme Chalinze ambapo ndiyo umeme ule unaenda kupoozwa pale, kiko asilimia 47. Kwa hiyo, niseme naomba nipendekeze kwenye maazimio, Bunge hili liitake Serikali kuharakisha ujenzi wa *transmission line* kupeleka kwenye kituo lakini pia kujenga kituo cha kupooza umeme cha Chalinze, kwa sababu maji mvua zinaendelea kunyeesha tumeshafanya marekebisho huko kwenye vyanzo vya maji ambavyo vina-*feed* Bwawa la Mwalimu Nyerere, hamadi! bwawa limejaa hatuna sehehmu ya kupeleka umeme, hatuna njia, hatuna mtambo, maji yanaendela kujaa. Kwa hiyo, tuweke pia azimio la kuhakikisha kwamba *transmission line* na kituo kinajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni Mwanza *Refinery,* mwaka 2021 Juni, Mheshimiwa Rais

Samia alizindua kituo cha kusafisha dhahabu cha Mwanza kwa masikitiko makubwa sana mpaka leo bado kituo hakijapata ithibati na sababu ya ile *refinery* ya Mwanza kukosa ithibati ni kwa sababu hatuna rasilimali ya kutosha ku-*feed* ile *refinery* tuliyoijenga pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili mwaka 2017 lilitunga sheria inaitwa Sheria ya Madini ya mwaka 2017 ambayo sheria hiyo Sura ya 123 kifungu cha tisa, lengo lake ilikuwa ni kwamba dhahabu inayozalishwa Tanzania kabla haijapelekwa nje isafishwe hapa ili kuiongezea thamani, na lengo lilikuwa zuri. Mikakati ya Serikali kwa sababu mtu hawezi kuelewa, kwa siku kile kiwanda kinahitaji kilo 59 sawasawa na kilo 1,770 kwa mwezi kile kiwanda kinahitaji ili kifanyekazi, kinakosa ithibati kwa sababu hatuna rasilimali ya kutosha ku-*feed* kile kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato ya Serikali wanataka wakanunue dhahabu Congo *it is well and good,* lakini mimi nazungumza kwa ajili ya Watanzania, vijana ambao tunataka tufaidike na *value chain*, mnyororo wa thamani, ardhi yetu Tanzania ina dhahabu. Kwa sababu hilo soko la Congo*, East Africa* yote inaangalia soko la Congo, Rwanda wanaangalia soko la Congo na nchi nyingine, kwa sababu sidhani kama Wakenya nao hawaangalii, soko la Congo ni *probability*. Hebu tuangalie hapa Tanzania dhahabu yetu kweli haitoshi ku-*feed* kile kiwanda mpaka tuende Congo? Ni kweli ni *initiative* nzuri kwa sababu tunataka wauze hapa na maendeleo yataendelea vuzuri nami niwapongeze, lakini *GST* imekosa uwezo wa kusaidia

vijana wetu kiteknolojia, kuwafanya vijana wetu wapate uhakika na sampuli za madini wanazozipeleka pale, kwa sababu eti hatuna *certified reference materials,* kutoa ithibati, kuthibitisha uhakika wa madini yanayopatikana ardhini matokeo yake tunategemea nchi nyingine zituuzie dhahabu wakati vijana wetu nasi tunataka waendelee!

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechoka kuona migodi kule Mwanza yamebaki mashimo vijana wetu wamebaki na umaskini, tunatamani tushiriki kwenye mnyororo wa thamani ili nasi tuendelee na tunufaike. Kwa hiyo niwaombe sana liongezeke azimio la kuitaka *STAMICO* na *GST* ishirikiane kwa ukaribu kutafuta mbadala, kutafuta suluhisho la dharura ili *GST* iwe na uwezo wa kiteknolojia na hizo sampuli zinazopelekwa pale kwenye maabara za *GST* zituletee majibu ambayo yana uhakika ili vijana wetu wakachukue mikopo benki na hayo majibu ya *GST*, waende wakachimbe dhahabu, dhahabu iende ika-*feed* Mwanza *refinery* kwa sababu mwaka mzima tumeshindwa, ni kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kile kiwanda kinauwezo mkubwa kwa sababu kwa viwango vya kimataifa kile kiwanda kinauwezo wa kusafisha dhahabu 99.9 *purity* ambao tunaweza tukawa ni kiwanda kikubwa Tanzania na Afrika ikiwezekana hata Afrika Mashariki, kwa hiyo ni kitu kikubwa, haiwezekani tukawa tumepoteza rasilimali mwaka mzima kama hivyo halafu ikabaki hatusemi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda kuna jambo moja ambalo limefanyika *for the first time in our country,* Mfuko wa Nishati safi ya Kupikia *(Cook Fund)*. Ninaipongeza sana Wizara ya Nishati pia ninaipongeza Serikali kwa ujumla, kwa sababu ni miaka mingi lakini *for the first time* tumefanya mjadala wa Kitaifa kuhusiana na nishati safi ya kupikia, na kwa sababu mimi ni mama pia napika lakini pia natoka kijijini kabisa ambako tunajua kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante kengele ya pili. Ombi lako hilo la azimio la *transmission line* tayari Kamati wanalo na wameshalitangaza hapa, kwa hiyo haina haja tena kulizungumzia azimio lako jipya, na kama una azimio jipya kwa mujibu wa Kanuni lazima ulilete kwa maandishi kabla Bunge halijatoa maamuzi. Kwa vile azimio tayari limo kwenye ripoti ya Kamati, kwa hiyo suala lako nakushukuru kwa mchango wako. Ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Issaay, ajiandae Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi na Mheshimiwa Hawa Chakoma ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Nichukue pia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia kuona siku ya leo; lakini pia nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa inayofanyika kwenye Jimbo la Mbulu Mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze na hoja chache. Mwaka huu wakati wa bajeti hii inayoendelea tulileteWa muhtasari wa mpango wa utekelezaji wa umeme vijini. Tulifurahishwa sana na huu mpango wakati ule ukiwa unaelezea jinsi ambavyo mpango huu utataekelezwa kwenye maeneo yetu, hasa miradi ya umeme. Tuna changamoto kubwa sana kule vijijini kwa sababu tunapofika muda fulani wa kuhitimisha Bunge hapa tunalazimika kwenda kule vijijini ili tuweze kuwaambia wananchi walau Serikali yetu ina mpango upi kwa upande wa kila sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hoja yangu kubwa ni kwamba miradi hii ya *REA* Vijijini imekuwa michache na inasubiriwa sana na wananchi kwa jinsi ambavyo umeme ni nishati muhimu sana kwa maisha ya kila siku na kwa huduma mbali mbali za jamii. Kwa hiyo katika taarifa ambayo ninaijengea hoja muda huu ni taarifa ya utekelezaji wa mpango huu kwa sababu viko vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme hadi sasa kwenye maeneo mbali mbali hususan Jimbo lile la Mbulu Mjini. Jimbo la Mbulu Mji lina vijiji na mitaa. Eneo la vijijini kuna vijiji ambavyo na kata hadi sasa umeme haujafika lakini mkandarasi ana miaka miwili. Ni kwa kiasi gani tunafuatilia utekelezaji huu wa mpango wa umeme vijijini? Na kwamba unafanyiwa tathmini inapofika muda fulani na wakandarasai wanaopewa hii kazi na *REA* nao wanafuatiliwa ili walau wanachi wapate huduma kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyowasilishwa ya mpango huu ilitupa matumaini kwa sababu katika bilioni 2.705 ya fedha za Wizara hii, kama tulivyoambiwa kwamba hela nyingi za miradi, kwa asilimia karibia 99, ilikuwa ya fedha za ndani; pengine tumekwama huko. Hata hivyo, sasa wananchi kule vijijini hawajapata umeme. Mimi nilikuwa naishauri Serikali, kabla hatujaenda kwenye bajeti ya mwaka unaokuja, huu wa 2023/2024 kwanza tujitathmini hao wakandarasi wamefanya kazi zao kwa kiwango kilichokusudiwa na mipango kazi yao ilienda vizuri? Na kama haikwenda vizuri basi tujitathmini na kuona namna gani tunachukua hatua sasa ya kubadilisha utararibu ule wa kazi zilizoko kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mkandarasi anatekeleza kwenye mikoa mitatu ndani ya miaka mitatu lakini hakuna eneo liliowasha umeme. Vilevile unakuta ni nguzo tu zimesimikwa, maeneo mengine hakuna nguzo na maeneo ya visima vya maji hakuna umeme, na maeneno mengine yanakosa umeme kwa sababu ya maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikua naona kama inawezekana historia ya wakandarasi hawa itazamwe upya na hasa yule aliyepewa kazi Mkoa wa Manyara, kwa sababu bado tuna tatizo kwenye mkoa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, ni eneo la ujazilishi. Kwenye taarifa hii ya Wizara, nitampatia Mheshimiwa Waziri baadaye; kuna maeneo ambayo tulitegemea sana, maeneo ya ujazilishi yanapata

miradi lakini kwa bahati mbaya miradi hii ya ujanzilishaji haijaanza hadi sasa. Kwa hiyo, mimi nadhani pia tujikite kwenye utaratibu wa ujazilishi kwa sababu katika kijiji unakuta kuna kaya 20. Kaya zingine zote takriban 200 na kitu hazina umeme kwa sababu hatujaweza kusambaza kwenye vitongoji. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kuwa mpango wetu wa awali huu wa mwaka 2022/2023 ulikuwa unagusa maeneo ya ujazilishi, na huu mradi wa ujazilishi uje vizuri kwenye mpango unaokuja ili tuweze kufanikisha adha hii na njia hii ya huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni eneo la ruzuku ya Serikali kwenye mafuta. Tunaipongeza Serikali kwa mpango wake wa kuweka ruzuku kwenye mafuta, na tulitegemea itapunguza makali, na kwa sehemu imepunguza. Hata hivyo tunachoona mafuta yanaposhuka bei ya usafirishaji inabaki pale pale. Mafuta yanapopanda bei ya usafirishaji inabaki pale pale. Sasa hapo ndipo mwananchi mtumia huduma anajiuliza; ni kwa kiasi gani walau ruzuku yetu ya Serikali imekua na tija? Na kama ni kipindi cha tathmini hapo pia tunatakiwa tufanye tathmini ili tuweze kufanya utaratibu mzuri wa ruzuku uwe na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kutokana na muda niseme pia, kwenye maeneo ya mijini na maeneo ya vijijini sasa hivi *TANESCO* wametowa utaratibu mpya wa umeme kwa 320,000 na umeme wa 27,000 ubaki kwenye maeneo ya vitongojini. Hata hivyo kwenye miji mingi, hasa Mji wa Mbulu, mitaa kumi ndiyo

*center* ya mji, mitaa mingine 48 na vijiji 34 vilivyoko vijijini ni maeneno ya wananchi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kwa kuwa tunajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, na tuwaombee viongozi wetu walioanzisha wazo hili; tuone utaratibu wa maeneo ya vijijini ni kwa namna gani basi umeme ule wa vijijini unarudi katika kiwango cha 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi tunavyokwenda kwenye baadhi ya mitaa na baadhi ya maeneo hata pembezoni mwa miji wananchi wengi hawataweza 320,000. Kwa hivyo kuna haja ya kuona kama tunajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere na eneo hili la ujazilishi na eneo hili la uunganishwaji wa umeme litazamwe katika mpango wa bajeti unaokuja, ili kufanikisha taarifa nzima ya utaratibu ambao unaweza ukasaidia wananchi hao ambao tayari wengi wao wamefanya *wiring*. Tayari wengi wao wana hamu ya kuunganisha. Hata hivyo, *wiring* tu laki tatu na kitu mpaka laki nne, ukichanganya na laki tatu nyingine na ishirini hizo ni laki saba. Kwa hali ya kawaida ya mwananchi wa kijijini au mwananchi anayetegemea hiyo nishati, kwa kweli hataweza kuunganisha umeme kwa jinsi ambavyo uwezo wa mwananchi ulivyo na hali halisi ilivyo na hatuwezi kuwa na manufaa kwa umeme huu ambao sahizi tunajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere. Lengo letu ni umeme uzalishe kwa kasi, lengo letu ni kuangalia kiasi gani wananchi wengi wanaunganisha umeme na wakishaunganisha umeme wanufaike na fursa hii ya kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu huu wa kuangalia shughuli mbali mbali za miradi ya

maendeleo tumekuwa na mipango mizuri sana, mipango ambayo tukienda kutafsiri kwa wananchi baadaye wanachi nao wanatuhoji mbona ule mpango wenu mlioutafsiri kwetu haujatekelezwa. Mimi nilikua nafikiri kama inashindikana wakati fulani tuanze na vipaumbele kama vinavyoainishwa kwenye Wizara mbali mbali na hasa hii Wizara ya Nishati ili mwisho wa siku tuweze kuona ni namna gani tunapata umeme kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine; ni dhahiri wazi 2015 tulisema tutapeleka umeme kila kijiji na kila kitongoji 2020 kwenye…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Issaay ahsante, kengele ya pili. Mengine unaweza ukayaandika. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, jiandae Mheshimiwa Hawa Mchafu, jiandae Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. IDDI K. IDDI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika nchi yetu hii. Tunaona kabisa katika sekta ya nishati, umeme vijijini kuimarisha miundombinu ya umeme, ujenzi wa uzalishaji umeme katika maeneo mbali mbali, kazi inaendelea. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu lakini pia Mkurugenzi Mkuu wa

*REA* vijijini kwa kazi kubwa ambayo wananendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri mara nyingi akisimama hapa anazungumzia habari ya nishati kwamba ni mambo matatu. Jambo la kwanza anasisitiza habari ya uzalishaji na sina shida na uzalishaji, naomba nimpongeze sana kazi nzuri inaendelea kwenye uzalishaji. Jambo la pili anazungumzia habari ya usafirishaji, sina shida na usafirishaji kwa sababu miundombinu mpaka sasa inaendelea kurekebishwa na naamini baada ya muda mchache miundombinu hii itakuwa tayari imekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la tatu ni suala la usambazaji wa umeme na hapa nilitaka nijikite kwenye kuzungumzia kwenye suala nzima la usambazaji. Nijikite kwenye Wilaya yetu ya Kahama. Wilaya ya Kahama ina halmashauri tatu ina vijiji zaidi ya 323, na tuna mkandarasi mmoja tu anayesambaza umeme wa *REA* ambaye bado mpaka sasa ana mkataba wake unaosema ni ndani ya miezi 18 awe amemaliza. Hata hivyo, mpaka sasa ni asilimia 23 tu ya kazi aliyoweza kuifanya kwenye Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, Mkandarasi huyu anayesambaza uememe kwenye Wilaya ya Kahama kwa maana ya Majimbo matatu; Ushetu, Msalala na Kahama, bado uwezo wake unaonekana kuwa chini sana kwa sababu mpaka sasa ameshamaliza miezi saba na miradi bado ipo asilimia 23 tu. Nikuombe Mheshimiwa

Waziri na hapa niombe uchukulie Wilaya ya Kahama kama *special case*, kwa sababu Wilaya ya Kahama ni Wilaya kubwa ina vijiji vingi ina halmashauri nyingi. Tumeahidi wananchi wetu kwamba ndani ya miezi 18 umeme huu utakuwa umekamilika kusambaa kwenye vijiji vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani kwenye Jimbo langu la Msalala tuna zaidi ya vijiji 62 havijapatiwa umeme. Sambamba na hili tuna migodi mikubwa na midogo ambayo inaenda na inakuwa kwa kasi na inategemea nishati. Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe utakuwa shahidi ulifanya ziara kwenye Jimbo la Msalala na ulienda kwenye maeneo ya migodi, ulitembelea Ntambalale, ulitembelea Mwanzimba na maeneo mengine na uliahidi kwamba umeme baada ya wewe kutoka umeme utaenda; lakini mpaka leo Mheshimiwa Waziri bado umeme haujafika kwenye maeneo hayo. Ninaomba muichukulie Wilaya hii ya Kahama kama *special case* ni tofauti na Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wilaya nyingine utaona kijiografia eneo lao ni dogo sana tofauti na Wilaya ya Kahama. Ukichukua Jimbo la Msalala tu lenye kata 18 lina *square* mita nyingi sana, kazi iliyofanyika ni kata moja na maeneo machache sana mapka sasa. Kwa hiyo niendelee kumuomba Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushangaza hapa wamemuongezea tena mkandarasi huyu zile kilometa zingine mbili kwenye kila kijiji. Kazi ya kwanza bado hajamaliza na yuko asilimia 23 lakini mmeenda

tena Mheshimiwa Waziri kumuuongeza tena *extension* ya umeme kwa kilometa mbili kila kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wasiwasi wangu ni kwamba wananchi tumewaahidi ndani ya miezi 18 umeme utakuwa umekamilika na wamepatiwa huduma hiyo; na baadhi ya wananchi tayari wameshafanya *wiring* kwenye nyumba zao. Sasa kama tu kazi ya kwanza ambayo zaidi ya vijiji 323 hajamaliza, je, tumemuongeza tena kila kijiji hicho hicho kilometa mbili, kwa maana ya nguzo 40. Je, kazi hii itakamilika kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri baada ya hapa, mimi naomba tukae, tuwasiliane tuzungumze tuone namna ya kukaa mkandarasi huyo ili atahakikishie, kama uwezo ni fedha ama kuna mambo memngine basi muone Wizara mnaweza kumsaidiaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie usambazaji wa umeme kupitia *TANESCO*. Tunafahamu kwamba *TANESCO* kwa sasa bado wana fedha, Wilaya ya Kahama tuna bajeti ya fedha ya kuweza kusambaza umeme kwenye maeneo mengine. Changamoto ya sasa ni nguzo. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba utusaidie kwamba kama fedha tunayo Wilaya ya Kahama lakini nguzo hazipatikani naomba Wizara itusaidie ili nguzo hizi ziweze kupatikana na wananchi waweze kupata huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nijielekeze kwenye sekta ya madini, nimpongeze

sana Mheshimiwa Waziri wa Madini kwa kazi kubwa ambayo anayoendelea kuifanya. Leo hii utaona mchimbaji na Mtanzania wa kawaida anamiliki leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa niseme tu, pamoja na kazi kubwa anayoendelea kuifanya kumekuwa na baadhi ya watu wanamvuta shati nyuma. Sisi kama Kamati tunaendelea kukupa moyo tunasema kwamba wale ambao wanakuvuta shati nyuma. Tutaenda kupamba nao ili kufanikisha adhma ya kuhakikisha unachangia asilimia 10 kwenye Pato la Taifa. Mambo ambayo yanamkwamisha Mheshimiwa Waziri, na hili nimuombe sana Waziri wa Fedha; Wizara ya Fedha imekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwenye sekta ya madini. Leo tunazungumzia habari ya umiliki wa leseni; na niwapongeze sana Mtendaji Mkuu wa Tume na Mheshimiwa Waziri, wameweza kuwapatia leseni wengi, wananchi wanajivunia kuwa na leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama alivyosema dada yangu hapo Mbunge wa Viti Maalum hapo, Nusrati Hanje, kwamba sasa mahitaji makubwa kwa wachimbaji ni mambo mawili tu. Jambo la kwanza ni hitaji la mtaji; na hapa niombe sana *BOT*, ambao mara kwa mara wamekuwa wakisisitiza benki kuwakopesha wachimbaji wadogo wadogo lakini benki hizo zimekuwa *in reality* haziendi kuwakopesha wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wadogo wanalia, leo hii wana leseni lakini wamekosa mitaji. Kwa hiyo, niendelee kuomba sana Wizara ya Fedha na hasa *BOT* kwenda

kuhakiki kwamba ni wachimbaji wangapi ambao wameshakopeshwa fedha na benki hizi ambazo mpaka leo zinaweza kuwasaidia katika uchimbaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni suala linalohusu ripoti ya *GST*. Nipongeze sana kazi kubwa ambayo inafanywa na *GST;* na nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, ikimpendeza hebu tuone namna ya kutenga fedha ya kuiwezesha *GST* ije iweke maabara ya upimaji wa madini katika Wilaya ya Kahama ili wananchi wanaozunguka Wilaya ya Kahama, ambako ndiko madini mengi yanatoka waweze kupata fursa ya kupimiwa madini yao kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, niendelee kuomba sana muweze kutenga bajeti kubwa kuiwezesha *GST* iweze kununua mitambo ya *drilling* ili iweze kufanya tafiti za kutosha. Mchimbaji mdogo mdogo huyu anayemiliki leseni akiweza kupatiwa mtaji, akaweza kupatiwa *data* za kwenye eneo lake maana yake ni kwamba tutakuwa tumemkuza mchimbaji mdogo mdogo huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anapambana na mambo mengi sana kwenye Wizara hii; lakini pia aende sasa matapeli yaliyoko kwenye Wizara hii. Leo utaona Mheshimiwa Waziri watu wanatoka huko nje na *briefcase* wanakuja hapa. Watanzania tunaomiliki leseni na rasilimali tunabaki kuwa maskini lakini hizi kapuni nyingine; na hasa niseme tu, zile zinazotoka nje, zinakuja na

*briefcase* pekee, lakini hapa wakiondoka wanaondoka na fedha nyingi zimejaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kuna kampuni moja, na Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, kampuni hii wewe mwenyewe unaifahamu, ni *QATAR Mining*. Hii inachukua fedha kwenye benki zetu hizi hizi, lakini pia inachukua fedha za Watanzania. Vilevile imeanza kudhulumu hawa watu. Niombe uchukue hatua za haraka sana kwenye kampuni hii ambayo inaendelea kudhulumu Watanzania, Watanzania waweze kupata haki zao za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa Mchafu, wajiandae Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Waziri Dotto, Mheshimiwa Makamba na Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia ripoti za Kamati zilizoletwa mbele yetu. Nitapenda kujielekeza kwenye ripoti ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Madawa ya Kulevya na Magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende sana kuipongeza Serikali, Wizara na taasisi kwa namna

zinavyopambana na masuala haya ya UKIMWI; lakini pia nipende kuwapongeza wadau kwa kushirikiana na Serikali kwa namna wanavyopambana na kutokomeza haya masuala ya UKIMWI kwa kufanya tafiti, kutoa huduma, kutoa vifaa tiba na kuwezesha matumizi ya takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni juu ya miradi inayoendelea kutekelezwa na Serikali ukiwemo ule Mradi wa Fikia *Plus*, Mradi wa Timiza Malengo na Mradi wa THIS *(Tanzania HIV Impact Survey)*. Miradi hii ni mizuri na ina malengo mazuri kwa Taifa letu kwa kuwa ina dhamira njema ya kupambana na kutokomeza masuala ya UKIMWI, lakini pia inataka kuja na *data* na takwimu sahihi kabisa. Vilevile wanahitaji kuibua wanaohitaji tiba ya *methadone* kwa upande waraibu pamoja na matibabu ya UKIMWI na Virusi vya UKIMWI kwa watu walioathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetangulia kusema miradi hii ni mizuri isipokuwa kuna changamoto kubwa kwenye Mradi wa *THIS*. Tama unavyojieleza ni *Tanzania HIV Impact Survey* kwamba una lengo la ku - *survey* masuala haya ya UKIMWI. Changamoto iliyokuwepo kwenye mradi huu, mradi hauwatambui watoto wenye umri chini ya miaka 15 ilhali tunafahamu sasa hivi kumekuwa na hatari kubwa kwa watoto wetu. Tunafahamu kuna maambukizi ya UKIMWI toka kwa mama kwenda kwa mtoto, kumekuwa na vitendo vikubwa vya ubakaji kwa watoto. Kumekuwa na vitendo vikubwa vya ulawiti kwa Watoto, lakini pia kumekuwa na tabia ama wimbi limezuka la watoto kufanya mapenzi ya

jinsia moja halafu Serikali inafanya mradi kabambe ya masuala ya UKIMWI wanawaacha watoto wenye umri chini ya miaka 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo hapa niseme kwamba haijafikiriwa ama haijawekwa sawa sawa…

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Hawa Mchafu kwa mchango wake mzuri, hususan kuhusu kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Nataka tu kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba juzi Mawaziri wa nchi 12 za Afrika tumekubaliana kwa vitendo kwamba tutaweka *program* maalum za kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto hususan watoto wenye umri wa miaka 18. Kwa hiyo, hili tunalifanyia kazi na Tanzania ndiyo nchi ya kwanza Barani Afrika ambayo imekubali kufanyiwa tathmini na nchi zote duniani katika mpango huu wa kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa taarifa hiyo.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ninaipokea. Ninachokisema Dada yangu Ummy, Mheshimiwa Waziri, mradi unaoendelea wa *THIS* ambao ni 2022/2023 unaelekea mwisho. Mradi hauwatambui watoto kwa maana hiyo sasa tutakuwa sasa tumeshafanya mradi kwa lengo la kutafuta *data* na takwimu za UKIMWI tunaacha kundi muhimu la watoto halafu tunasema tuje kufanya tena mradi mwingine? Hebu tuangalie kama tunaenda sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaipongeza miradi hii ni mizuri ina nia nzuri ila tunachopaswa, hata huo mradi unaokuja tuzingatie na tuangalie watoto kwa sababu wimbi la ubakaji, wimbi la ulawiti na vitendo vya mapenzi ya jinsia moja kwa watoto wetu, watoto wamekuwa ni kundi la hatari sana. Watoto wapo kwenye kundi hatarishi. Kwa hiyo nitaomba sana na mradi mwingine na mwingine uweze kuzingatia hilo. Nimeipokea taarifa na nakushukuru Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango mwingine ni kuhusiana na masuala ya UKIMWI na Virusi vya UKIMWI kwenye maeneo ya visiwani. Hapa najumuisha visiwa vyote na nikizungumza kwa maeneo ya mialo ama visiwani kule Mwanza. Mkoa wa Mwanza hususan kwenye maeneo yake ya visiwa, maeneo mengi yanaongoza ya wagonjwa kutokufikiwa na huduma ya 953 kwa sababu ya nature ya jiografia ya mazingira yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali wana mpango kwamba ifikapo 2030, kuwa na maambukizi sifuri.

Kwa hiyo nataka tuangalie kama kwa namna hivi tunavyoenda, maeneo ya visiwani, matibabu ya huduma ya afya hayapo sawasawa. Utakuta tunacho kituo cha afya lakini idadi ya Madaktari hawatoshi ama vifaatiba havitoshi ama niseme kwamba wataalam hawatoshi kwa hiyo tunajikuta tunapambana ifikapo 2030 kufikia maambukizi sifuri, lakini kwenye maeneo kama hayo unakuta bado hatujafanya ama hatujayafikia sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusiana na magonjwa yasiyoambukiza. Nataka kusema kama kuna kitu muhimu Watanzania tunakihitaji ni bima ya afya kwa wote. Tunahitaji bima ya afya kwa wote kuliko kitu kingine chochote. Watanzania tuache masihara na afya zetu, tunahitaji bima ya afya kwa wote. Nitakupa mfano, mgonjwa mwenye Virusi ya UKIMWI ama mwenye UKIMWI. Tunashukuru kwa mgonjwa huyu ambaye anapata matibabu ama niseme dawa bure kutoka Serikalini lakini ni vipi akipata magonjwa nyemelezi na hana bima ya afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, matibabu yamekuwa ghali sana, kwa maana hiyo kama hauna bima ya afya, mgonjwa anaumwa UKIMWI ama ana Virusi vya UKIMWI halafu ana *diabetes,* mgonjwa ana UKIMWI ama ana Virusi vya UKIMWI ana *hypertension,* mgonjwa mwenye UKIMWI ama ana Virusi vya UKIMWI ana *hepatitis B* ama *C*. Hebu angalia mgonjwa huyu atakuwa yuko katika hali gani. Ama hakika atakuwa yuko katika hali ya hatari sana kwa sababu magonjwa ya sukari, presha ni sehemu ya magonjwa yanayochukua bajeti kubwa ya Serikali

kwa ajili ya kuwatibu Watanzania. Kwa hiyo naomba sana hili jambo Watanzania na Serikali tuliangalie ili tuweze kuharakisha jambo hili la bima ya afya kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwapongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya na dhamira yao njema ya kutaka kuhakikisha wanafikia maambukizi sifuri ifikapo 2030, lakini nitapenda kujua, Serikali ina mpango gani, ina mkakati gani na imejipanga vipi kuondokana na maambukizi mapya na tusifikie maambukizi sifuri ikifika mwaka 2030 kwa kuyafikia makundi yafuatayo:-

(a) Wanaojidunga;

(b) Wanaojiuza; na

(c) Wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema maambukizi sifuri 2030 lakini leo tuko 2023 na bado ipo changamoto kubwa kuyafikia makundi haya. Kwa hiyo nitapenda kusikia kauli ya Serikali mpango mkakati tumejipangaje kuweza kuyafikia makundi haya matatu ili kutimiza dhamira njema ya kufikia maambukizi sifuri ifikapo 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, ajiandae Mheshimiwa Dotto.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hii Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Musoma Mjini, Jimbo langu lilibahatika kupata na lenyewe ule mpango wa umeme wa *REA* hasa katika yale maeneo au mitaa ya pembezoni pamoja na kwamba liko mjini. Baadhi ya mitaa iliyofaidika na mpango huo iliyoanza kufaidika ni pamoja na ule Mtaa wa Bwiribukoba, Nyabisare, Songambele, Kwangwa, Zanzibar, Bukanga ni mitaa ambayo ilibahatika na ilianza kubahatika na huo mpango. Baada ya 2015 - 2020, tulipoanza 2021 mpaka leo ule mpango kwa pale Musoma Mjini ukaondoka na baada ya kuondoka tunaishukuru kwamba *TANESCO* imeendelea kusambaza hata zile *transformer* katika hiyo mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu yale maeneo mitaa ya pembezoni ni maeneo ambayo yanafanana na maeneo ya vijijini. Kwa hiyo unakuta *transformer* imepelekwa lakini watu walioweza ku-*tap* pale umeme hawavuki watu watatu, wanne na sababu ni rahisi tu kwamba sasa kwa sababu ile miji inakaa mbali mbali lazima mwananchi aweke nguzo zaidi ya mbili. Sasa nguzo mbili unazungumzia zaidi ya shilingi 500,000. Sasa hebu tuliangalie hili kwamba yule aliyebahatisha 2015 - 2020 aliweka umeme kwa shilingi 27,000. Leo huyu mwingine jirani yake ambaye

wakati ule aliomba lakini hakupta nafasi anaambiwa aweke umeme kwa zaidi ya shilingi 500,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutokana na hali hiyo, kwa hiyo watu wangu wengi wote walioko maeneo ya pembezoni wameshindwa kuweka umeme na kama tunavyofahamu mahitaji ya umeme ni makubwa na hasa katika mazingira ya sasa, wananchi wangependa wapate huo umeme. Sasa leo cha ajabu sasa ukija pale Musoma Mjini na nimwombe Mheshimiwa Waziri Makamba aje pale Musoma mwenyewe ashuhudie kwamba leo jirani yangu ni Butiama, pale kuna Kijiji cha Nyabange, pale wanapata umeme wa shilingi 27,000, hapa kwangu Bwiribukoba wanapata umeme wa shilingi 500,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo matokeo yake leo watu badala ya kukimbilia mjini watu wengi wanahamia pale jirani kwa sababu pale ndipo sasa gharama za kuishi zimekuwa nafuu. Sasa kutokana na hali hiyo, watu wangu wameshindwa kufahamu kwamba hivi wao kumbe kuingia mjini tena imekuwa adhabu kwao? Sasa natambua kabisa na wote tunatambua kwamba bado ile miradi ya *peri urban* bado ipo na kama ipo, sasa sisi ambao tayari tulibahatika kuingia kwenye huo mpango wa *REA,* leo tuna dhambi gani, badala ya kuendelea kulipa kwa shilingi 27,000 ili watu wote waweze kupata hiyo huduma sasa matokeo yake wao wanalipa umeme kuanzia shilingi 300,000 mpaka zaidi ya shilingi 500,000?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningependa wakati Mheshimiwa Waziri anajibu, ni vyema awaambie kabisa watu wa Musoma watambue kwamba sasa ule mpango utarudi au ndiyo wameendelea kuusahau. Kama wameendelea kuusahau hata umuhimu wa zile *transformer* haupo kwa sababu Serikali inapoteza *resource* pale inapopeleka *transformer* halafu wanaweza ku-*tap* watu wanne au watu watatu peke yake. Kwa hiyo nadhani kuna haja ya kuliangalia hilo ili tuone namna ya kuwasaidia watu wetu wa Musoma kwa sababu nao wangependa kupata hiyo huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, liko jambo ambalo vile vile huwa linanichanganya kidogo. Leo unakuta kwamba kuna mtu anahitaji umeme na kwa sababu anahitaji umeme akienda *TANESCO,* wanamwambia hawajawa tayari au hawana bajeti kwa mwaka huu kwa ajili ya kumsogezea umeme. Yule mwananchi anasema sawa, mimi nina hiari sasa kulipia *in advance*. Sasa akikubali kulipia *in advance, TANESCO* wanasema ukishalipia kwa hiyo gharama labda ya kupeleka pale umeme kununua *transformer* pamoja na zile nguzo labda unakuta ni Sh.20,000,000. Sasa najiuliza kama yule mwananchi amekubali kulipia huo umeme *in advance,* ni kwa nini *TANESCO* wasiendelee kumrudishia aidha kwa kumkata pole pole mpaka zile fedha zake zitakapoisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tofauti na hapo anaambiwa wewe kaa subiri siku tukiwa tayari na bajeti tutakuwekea umeme. Kwa hiyo nadhani kuna kila aina ya sababu kwa yule ambaye

ameshajitolea amelipa *in advance* walau *TANESCO* wakubali kuja kumrudishia hizo gharama kuliko kusema kwamba hawako tayari tena kuja kumlipa hizo gharama wakati bado wanaendelea kumchaji ile bili yake ya kila mwezi. Kwa hiyo nadhani hapo napo kuna haja kidogo ya Serikali kuendelea kuliangalia hilo tatizo la kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye upande wa madini. Tunatambua kwamba *STAMICO* ni *caretaker* kwa ajili ya wale wachimbaji wadogo na kama kweli tunapenda kuwasaidia wale wachimbaji wadogo, hivi *STAMICO* Mheshimiwa Waziri, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inawasaidia *STAMICO* uwezo kwa kuwapa fedha za kutosha ili waweze kuwakopesha wale wachimbaji wadogo wadogo waweze kujenga uwezo? Kwa sababu leo hii ukiangalia hata katika takwimu wale wachimbaji wadogo ni kati ya watu ambao wanachangia sana pato la nchi hii, lakini wapo tu wala hakuna namna wanayosaidiwa ili waendelee kukua, waendelee kukuza mitaji na kutokana na hali hiyo wachimbaji wadogo uzuri wao ni kwamba leo ukimsaidia akijenga uwezo anarudi ku-*re invest* humu humu nchini tofauti na wale wachimbaji wakubwa ambapo unaambulia tu kile kifaida, fedha nyingine yote inayobaki anaipeleka kwao. Kwa hiyo kuna kila aina ya sababu ya kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo kwa sababu akishapata fedha hapo ataendelea kujenga hoteli, ataendelea kufanya miradi mikubwa ambayo itaendelea kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nadhani kuna kila aina ya sabau ya kuona namna ya kuwasaidia. Kwanza kuisaidia *STAMICO,* lakini vile vile aweze kuwasaidia wale wachimbaji wadogo na kwa kufanya hivyo watasaidia sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dotto, ajiandae Mheshimiwa Makamba, ajiandae Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ...

**NAIBU SPIKA:** Dakika tano tano.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kama walivyosema wengine nichukue nafasi hii kwa kweli kuipongeza sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwanza kwa umakini wao. Nimefanya nao kazi kwa muda sasa, ni Kamati ambayo kwa kweli weledi wake kwenye uchambuzi wa masuala ya madini hautiliwi shaka na ni watu ambao wanaenda kwenye *details* kwenye haya mambo yanayohusiana na Sekta ya Madini. Kwa kweli wametusaidia sana kama Wizara kuona namna gani tuipeleke mbele sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa niaba ya wenzangu Wizarani kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Nishati na Madini, Mheshimiwa Kitandula na Makamu wake Mheshimiwa Gulamali pamoja na Wajumbe wote kwa namna ambavyo wamekuwa wakitusaidia sana katika kutusimamia kwenye kuendeleza Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamesemwa mambo kadhaa na nisingependa kuonekana kama najibu. Nataka tu kuchangia hoja ya Kamati na nataka nizungumze mambo matatu. Jambo la kwanza, imeelezwa hapa juu ya upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu vya uchenjuaji au *refinery* zetu za dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kwa msaada wa Bunge hili. Wakati tunaanza kujenga *refinery* hapa nchini, changamoto na matishio ya *refinery* hizi kupata malighafi ilikuwa je, hawa *refiners* watapata dhahabu kutoka kwa wachimbaji? Kwa sababu bei wanayoweza kununua inawezekana kwenye soko ikawa ya juu zaidi kuliko wanayonunulia wenyewe. Kwa hiyo tulichofanya na tulileta hapa Bungeni tukapitishiwa na Bunge ni kutoa vivutio kwa ajili ya *refineries* hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kivutio cha kwanza tukashusha mrabaha wa dhahabu. Dhahabu ukitaka kwenda kuuza kwenye *refinery,* badala ya kuchajiwa 6% ya mrabaha, yule anayeuza kwenye *refinery* anachajiwa 4% peke yake na hii inatusaidia kuwapa nafasi wachimbaji wale kupeleka dhahabu na kulipa mrabaha kidogo zaidi na viwanda hivi viweze kupata malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ambalo ni muhimu Bunge tukalielewa na tusiliogope. Kwa kawaida kama una kiwanda kutafuta malighafi kutoka nje ya nchi siyo dhambi, *actually* ni jambo zuri sana. Kiu yetu ni kuifanya Tanzania kuwa *hub* ya biashara ya madini. Ni vizuri tukatengeneza mazingira rafiki ya kuwavutia majirani zetu walete madini yao hapa ndani waweze kufanya *refinery* na mwisho wa siku waweze kusafirisha. *Advantage* tuliyonayo sisi kama Taifa ni kwamba madini yanayochimbwa Tanzania kwenye masoko ya kimataifa hayatiliwi mashaka kwenye *ethics* zake. Yamechimbwa kwa kufuata utaratibu kwa kuzingatia haki za binadamu na kwa hiyo ukienda kwenye masoko ya kimataifa duniani yananunuliwa kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaangalia rasilimali zetu za ndani, lakini hatutaacha kuwavutia wengine kwa ajili ya kuja kuuza madini yao hapa kwetu. Yako Mataifa hayana hata shimo moja la dhahabu lakini yana *refinery* na yanatumia rasilimali za Mataifa mengine kwa ajili ya kufanya biashara. Fursa kama hiyo hatuwezi kujifungia tu ndani tukasema kwamba sasa sisi tutatumia madini yetu peke yetu halafu tufanye *refinery* mengine tuyaache. Ndiyo maana tunatoa wito na mataifa mengi yamekuja hapa kujifunza, tunatoa wito kwa majirani zetu kuleta madini yao kwa ajili ya kuja kufanya *refining* kwetu hapa nchini kwa sababu kwanza watapata bei ya uhakika. Wanunuzi wapo, masoko yapo na mifumo ambayo ni rahisi zaidi ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko lingine limezungumzwa juu ya leseni ya *Peak Resource*. *Peak Resource* wako Ngwara na Mheshimiwa Mulugo pamoja na Mheshimiwa Neema wanalizungumza kila wakati. Ni kweli kwamba tuliwahi kuwaalika kwa ajili ya kwenda kufanya *signing.* Tulivyofika siku ya *signing* wenzetu wakataka tubadilishe kipengele kimoja kwenye mkataba na kipengele ambacho tulikuwa tunabishania ni kimoja tu, kwamba uchimbe hapa uongeze thamani ya madini hayo hapa nchini. Wao wakawa wanataka wachimbe hapa wakaongeze thamani na tayari walishanunua eneo la kujenga hicho kiwanda London. Tukakubaliana Hapana, tunahitaji hicho kiwanda kijengwe hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetuchukua muda, baadaye tumekubaliana. Naomba niwape taarifa watu wa Ngwara, Mheshimiwa Neema na Mheshimiwa Mulugo. Habari njema tuliyonayo ni kwamba timu ya majadiliano imemaliza hiyo kazi, mikataba hiyo sasa iko kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya *vetting* na muda siyo mrefu tutafanya *ceremony* ya *signing* kwa ajili ya mkataba huo wa *rare-earth element.*

**NAIBU SPIKA:** Haya Mheshimiwa Waziri malizia sekunde 10.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nataka nimalizie tu lile la *STAMICO* na kuwasaidia wachimbaji wadogo. Ni kweli amesema Mheshimiwa Manyinyi, wachimbaji wetu wadogo wameongeza tija kubwa sana kwenye uzalishaji. Wametoka kwenye 4% ya mapato yote tunayopata

mpaka 40%. Tumeamua kuwasaidia kwa kuwanunulia mitambo kwa ajili ya kuwafanyia utafiti kwenye maeneo yao na kuwapatia leseni ili waweze kuchimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru Kamati na kwa kweli tutaendelea kuwapa ushirikiano na tunaomba Kamati waendelee kutupa ushirikiano ili tuweze kusukuma sekta yetu hii mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Makamba.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Taarifa hizi za Kamati hasa katika Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini. Nianze kwa kuwapongeza Kamati kuanzia Mwenyekiti, Mheshimiwa Kitandula, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Gulamali na Wajumbe wote kwa kweli kwa kazi nzuri na taarifa nzuri waliyoitoa, lakini vile vile kwa siku zote kuwa makini katika kushauriana na sisi na kusaidiana katika kupeleka mambo mbele yanayohusu sekta yetu na taarifa yao kama alivyosema Mheshimiwa Dotto Biteko, inadhihirisha umahiri, umakini na weledi iliyonayo Kamati katika kushughulikia mambo ambayo wanashughulika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nami ni mchangiaji siyo mjibuji wa hoja na napenda nitambue mchango mzuri sana wa Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Nusrat, Mheshimiwa Tabasam,

Mheshimiwa Iddi Kasim, Mheshimiwa Genzabuke na Mheshimiwa Issaay na niseme yale ambayo wameyaelekeza kwetu kama Wizara, basi tutayachukua na kuyafanyia kazi. Kwa kuwa muda hautoshi kuyazungumzia yote lakini niseme tu nimeyapokea, nimeyaandika na tutayashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda haraka haraka tu kuhusu *REA* nafahamu ni kweli kuna malalamiko mengi na changamoto nyingi kuhusu ucheleweshaji wa Miradi ya *REA*. Naomba nitoe faraja kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wa Tanzania kwamba baada ya kubaini changamoto zilizopo tumebadilisha utaratibu sasa wa manunuzi, usimamiaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi hii. Kuanzia sasa kwa mfano, vigezo vya mkandarasi kupata mradi vitakuwa tofauti kwamba mkandarasi hawezi kupata mradi mpaka alionao walau amefikia 60%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutakuwa na *pre-qualification* kama Kamati ilivyopendekeza kwamba kutakuwa na kundi la wakandarasi mahiri ambao watakuwa wamepitia vigezo na kazi zitakuwepo, atakayemaliza haraka ndiyo atapata kazi nyingine haraka. Hii itatoa *incentive* kwa wakandarasi kufanya kazi haraka. Sasa hivi haijalishi kama una kasi au huna kasi, unaingia kwenye tenda, unapata kazi nyingine. Kwa hiyo matokeo yake ni kwamba wakandarasi wamejilimbikizia kazi kwenye eneo letu la *REA* lakini kwa sababu ni wakandarasi wako kwenye madaraja na kwingineko, kwa hiyo unakuta wana kazi nyingi kuliko uwezo wa kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia taarifa nyingine kwa Kamati ni kwamba rasmi sasa *REA* tumeajiri vijana 136 ambao kazi yao itakuwa ni usimamizi wa Miradi ya *REA* tu katika majimbo ya Waheshimiwa Wabunge. Hawa watakuwa hawana kazi nyingine zaidi ya kufuatilia na kuripoti kwa Wabunge na Serikalini kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa miradi hii. Hawa watakuwa ni kiungo muhimu kati yetu sisi Wizarani, *REA, TANESCO* na viongozi wa kisiasa ili wakati wote tuwe katika ukurasa mmoja kuhusu changamoto zilizopo na tuweze kusaidiana kuzimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwenye Miradi ya Ujazilizi; hata tutakapomaliza kupeleka umeme kugusa vijiji vyote, bado kutakuwa na vitongoji vingi vitakuwa havina umeme. Kwa mfano, kwenye vijiji sasa hivi tuko 80% lakini kwenye vitongoji tuko 44%. Kwa hiyo utaona jinsi gani kufikia vijiji tafsiri yake siyo kupeleka umeme kwa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kama Serikali tumeamua kuja na mpango mkubwa wa kupeleka umeme katika vitongoji vyote ambao tutaufanya ndani ya miaka mitano. Ilikuwa tuanze mwaka wa fedha uliopita 2021/2022, tulipata changamoto kwa sababu ni fedha nyingi. Tutakuja wakati wa bajeti kuwaomba mtusaidie Waheshimiwa Wabunge kupitisha mpango huo kabambe na ambao utatekelezwa kwa namna tofauti kama inavyotekelezwa miradi ya sasa, kwani kwa sasa hivi ina changamoto. Kwa hiyo, mradi huu sasa utajibu maswali mengi ya ujazilizi kwa sababu utafikisha umeme katika maeneo yetu mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie shilingi 27,000 na shilingi 300,000, niseme tu taarifa imekuja kwetu na kwa sababu ya muda, tunaishughulikia na tutatoa mwongozo maalum wa namna ya kulifanya jambo hili. Jambo ambalo nilitaka Waheshimiwa Wabunge walifahamu, ni kwamba, gharama halisi ya kumwingizia mtu umeme kwenye nyumba yake ni shilingi 426,000 mpaka shilingi 800,000. Kwa hiyo, shilingi 27,000 ni chini sana ya gharama halisi. Shilingi 331,000 bado iko chini sana ya gharama halisi. Kwa hiyo, Serikali inatoa *subsidy* kwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapotoa shilingi 27,000 maana yake Serikali kupitia *TANESCO* inatoa ile ya ziada. Hii pesa inatoka katika shughuli nyingine za maendeleo ambazo tulikuwa tuzifanye. Kwa hiyo, ni muhimu tunapotaka hizi bei tujue gharama yake, na sisi tutakuja na mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme kukatika, niseme tu kwamba tunafahamu na tunakiri changamoto bado ipo. Ambacho nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania ni kwamba hivi tunavyoongea tunayo mipango madhubuti ya kuifumua *grid* nzima na kuirekebisha. Kwa sababu changamoto kubwa iliyokuwepo ni miundombinu chakavu. Hili jambo ukubali ukatae, ndiyo ukweli kwamba miundombinu yetu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme ilikuwa haitoshelezi mahitaji na haijafanyiwa marekebisho muda mrefu. Tarehe 15 Februari tutasaini mradi unaitwa Gridi Imara, ni miradi 26 ya takribani shilingi trilioni moja ku-*stabilize grid* yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, tutawaalika mshiriki kwa sababu ni jambo ambalo litaenda kuanza safari ya kumaliza changamoto ya miundombinu, na uzalishaji wa umeme tunaongeza ili tusiwe na *gap*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Julius Nyerere unaenda vizuri, tunashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamefika na wameona na wametushauri kuhusu namna ya kwenda vizuri. Ni kweli kulikuwa na changamoto ya *transmission line,* miundombinu ya kutoa umeme kule kuusambaza kuingiza kwenye grid. Mradi huu ulianza kutekelezwa Desemba 2018, lakini tulisaini njia za kutoa umeme pale Septemba, 2021 miaka mitatu, kulikuwa na *gap*. Ila tumeharakisha mpaka sasa kufikia asilimia 80, siyo jambo dogo. Kwa hiyo, mradi wa uzalishaji umeme utaisha pamoja na mradi wa kutoa umeme kwenye eneo lile na kuusambaza kwenye gridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya mafuta ya Mheshimiwa Tabasam tumeyapokea. Kama mnavyofahamu, hivi juzi juzi Serikali ilisaini mkataba wa uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya kupakua na kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam na…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Sekunde 30 malizia.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane kukubali mapendekezo ya Kamati na kuyaunga mkono na kuendelea kuahidi ushirikiano wa Wizara, Bunge na Kamati ya Bunge kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene, jiandae Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi, na nianze kwa kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI, Dawa za Kulevya na Magonjwa Yasiyoambukiza, Mheshimiwa Fatma Toufiq pamoja na Kamati yote kwa ujumla. Tunafanya nao kazi vizuri, na niseme tu kwa kweli maazimio yote saba ambayo wameyaleta katika taarifa yao, sisi Serikali tunayapokea yote kwa mikono miwili na tunahakikisha kwamba tunakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme tu katika kuchangia katika maazimio haya yaliyogawanyika katika maeneo matatu. Eneo la kwanza ni eneo la UKIMWI ambapo Kamati hii na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanaonisikia, tumemaliza mkakati wa nne wa mapambano dhidi ya UKIMWI, na sasa tumetengeneza mkakati wa tano. Katika mkakati huu wa tano, msisitizo mkubwa utakuwa ni kutoa elimu juu ya kupima virusi vya UKIMWI pia kufuatilia VVU wale watoro, ufuasi wa dawa na tohara kwa wanaume. Hayo ni maeneo ambayo yatatiliwa mkazo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuimarisha afua za udhibiti wa VVU na UKIMWI na hasa kwenye mikoa ile ambayo maambukizi yamefika asilimia zaidi ya 4.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kutoa elimu kuhusu unyanyapaa na ukatili wa kijinsia ili kupunguza hofu kwa waathirika. Eneo lingine ni kujenga uwezo wa Kamati za UKIMWI na kuhakikisha kuwa Kamati hizi zinakuwa na uwezo na kuchukua hatua na kutoa ushauri unaostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho katika eneo hili la UKIMWI ni kuhakikisha kuwa vituo vya kutoa huduma ya afya ya mama na mtoto vinatoa elimu pia kwa wamama wajawazito ili kuhakikisha kwamba maambukizi yale hayatoki kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni eneo la magonjwa yasiyoambukiza, ambapo hapa kulikuwa na azimio na azimio moja ambalo limesisitiza zaidi kwamba magonjwa haya ambayo hayaambukizi yanaweza tu kupungua pale ambapo elimu itatolewa kwa wananchi, na pia kuhimiza michezo shuleni. Sisi kwa ujumla tumepokea azimio hili na kazi kubwa ya Serikali ni kwenda kulitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Hapa yako maazimio mawili na msisitizo mkubwa umekuwa ni umuhimu wa kuhakikisha kwamba sera ya kudhibiti dawa za kulevya na mapambano dhidi ya dawa ya

kulevya inatiliwa mkazo na kuhakikisha kwamba inakamilika. Niseme tu hatua za utayarishaji wa sera hii zimekamilika na sasa tuko katika kupeleka kwa wadau ili tuweze kupata maoni na baadaye sera hii itakuwa imekamilika. Nataka niwahakikishie Bunge na Kamati kwamba tuko katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala zima ambalo limezunguzwa hapa pamoja na michango ya Wabunge ni umuhimu wa kuweka waratibu wa masuala ya UKIMWI katika Halmashauri zetu za Wilaya. Dawa za kulevya hazina uratibu kule kwenye ngazi za chini. Kwa hiyo, maoni haya yaliyotolewa, nadhani hata kama siyo sehemu ya azimio lililosemwa katika maandishi, lakini ni jambo zuri la kulichukua na sisi Serikali nadhani ni *administrative*, ni kusema tu katika kwamba masuala ya UKIMWI na dawa za kulevya, tutajaribu kuliangalia katika Serikali tuone namna gani litakavyotekelezwa, lakini siyo jambo baya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilizungumzwa hapa juu ya mradi wa *DHS* ambao ulikuwa ni mpango ambao unafuatilia na kuangalia hali ya UKIMWI katika makundi mbalimbali. Mheshimiwa Mchafu amezungumza suala hili akasema haishirikishi watoto katika utafiti huu. Ni kweli, nadhani pengine ni upungufu. Tujaribu kuona kwa *program* hii ambayo kwa kweli inaisha na sasa tunakuja *DHS* nyingine, tutaangalia namna ambavyo tunaweza tuna-*include* suala la watoto kuingia katika utafiti huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya iko kwenye mchakato wa kuanzisha mpango mkubwa

sana ambao utakuja na utafiti mkubwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI na madhara yake. Kimsingi nao nadhani wamelichukua hili, tutashirikiana kwa sababu tunafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kwamba katika mpango unaokuja basi tunahakikisha na watoto wanaingia katika nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Vinginevyo, naunga mkono hoja ya Kamati kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi ya kuja kuhitimisha hoja yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata wachangiaji wawili katika wengi lakini Mheshimiwa Waziri Simbachawene pia amesaidia kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo. Mheshimiwa Mwandamila alikuwa na hoja ambayo amezungumzia sana namna ya udhibiti wa madawa ya kulevya, waraibu wanavyoathirika na ukosefu wa waratibu kule kwenye Halmashauri zetu. Hili jambo ambalo tunaliomba, Kamati italisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo kama Kamati imeliona ililete katika Bunge lako

pamoja na mapendekezo ya Kamati kwamba zile Kamati za UKIMWI kule vijijini kwenye Halmashauri zetu zina Serikali kupitia TAMISEMI waone ni namna gani zitaweza kuhusishwa pia na dawa za kulevya. Maana yake zinajulikana tu kama Kamati za UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na mchangiaji mwingine ambaye ni Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, alizungumzia jambo ambalo Mheshimiwa Simbachawene pia amelitolea ufafanuzi. Nami pia niongezee kidogo. Hizi tafiti zinapofanyika zinalenga sana wale ambao wameathirika kwa kiwango kikubwa. Hii *DHIS* imechukua watu *above 18* kwa sababu waliozidi miaka 18 mpaka 24 ndio wenye maambukizi makubwa. Wale ndio waathirika wakubwa. Kwa hiyo, Unapochukua *sampling* za kupata *result* ya *research* yoyote; ili *sampling* ziwe na matokeo mazuri, NI lazima uchukue kundi ambalo linaathirika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu mradi huu unaenda kwisha na Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba mradi huu unaisha, lakini sababu ilikuwa ni hiyo, kwamba watu waliokuwa wameathirika sana ni zaidi ya miaka18. Kwa hiyo huku mbele tunakoenda nadhani Serikali itaona na italifanyia kazi. Nasi kama Kamati tutaendelea kuishauri Serikali kwamba ione hilo pia, lakini kupunguza gharama za *sampling.* Unapofanya utafiti wowote, ili mchukue sampuli za watu wachache upate uhalisia, watu wa chini ya miaka 18 utahitaji kundi kubwa sana na gharama zitakuwa ni kubwa sana. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati hii, naliomba Bunge lako Tukufu lichukue mapendekezo ya Kamati na kuyafanya kama mapendekezo ya Bunge pamoja na nyongeza hii ambayo nimeiwasilisha hapo kwako. Naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe mapendekezo ya Kamati kuwa mapendekezo ya Bunge ambapo Serikali itayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Haja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa namna ambavyo umeweza kusimamia hoja ya Kamati vizuri, nakupongeza sana.

Pili, nitumie fursa hii kuwapongeza Wabunge wanane ambao wamechangia hoja ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wabunge ambao wamechangia, Wabunge watano wamechangia sekta ya nishati na hususan hali ya upatikanaji wa umeme, utekelezaji wa mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kule Rufiji na utekelezaji wa mradi wa *REA*. Kamati inashukuru kwa kuunga mkono maoni na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa machache yaliyokuwa yamebainika kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia; Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Vedasto Manyinyi; na Mheshimiwa Josephine Genzabuke wamezungumzia upande hasa wa masuala mazima ya usambazaji wa umeme vijijini, *REA,* namna ambavyo utekelezaji wake unavyoenda na pia Mheshimiwa Waziri Januari amezungumza hapa kwa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia utekelezaji wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere kule Rufiji ambao amezungumza Mheshimiwa Nusrat Hanje, na namna ambavyo utekelezaji wa *transmission line* kutoka kwenye Bwawa la Mwalimu kuja Chalinze. Pia iende sambamba na ujenzi wa *substation* pale Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa bwawa lile unaenda sambamba pamoja na ujenzi wa *transmission line*. Kama ambavyo mchangiaji alivyozungumza kwamba tunaiomba pia Serikali

ihakikishe kwamba usimamizi wa ujenzi wa *transmission line* kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere kuja Chalinze ukamilike uende kwa haraka na ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukamilishaji wa *substation* iliyoko pale Chalinze na yenyewe pia kwa sababu inaonekana asilimia yake iko chini, tunaiomba pia Wizara ihakikishe kwamba suala hili inalikamilisha kwa haraka ili iende sambamba na ukamilishaji wa bwawa lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunampongeza Mheshimiwa Rais kipindi ambacho mwezi wa 12 wakati wa ujazaji wa maji katika lile bwawa, Mheshimiwa Genzabuke amezungumza hapa. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri na uendelezaji wa kutoa fedha kwenye mradi huu wa Mwalimu Julius Nyerere, kwamba haukwami na unaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo lilizungumzwa hapa na Mheshimiwa Tabasam ni suala la mafuta hususan kuchelewa ushushaji na hivyo kuongeza bei ya mafuta. Ni suala ambalo Kamati imekuwa ikilisema sana na Mheshimiwa Tabasam amelizungumza hapa. Kwa hiyo, naomba tu Serikali iboreshe miundombinu na Bandari ya Dar es Salaam kuhakikisha kwamba suala hilo la upakuaji mafuta linaenda kwa wakati ili kupunguza gharama kwa watumiaji wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kuhusu

kupeleka umeme kwenye migodi, na Mheshimiwa Waziri amelizungumza hapa, hivyo tumwombe Waziri alisimamie suala hili kuhakikisha kwamba migodi inapata umeme. Nimesikia Mheshimiwa Tabasam amezungumzia kule Sengerema na migodi mingine ambayo ipo ndani ya nchi yetu, hata kule Igunga, Nzega na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika upande wa madini, Wabunge wanne wamechangia; Mheshimiwa Iddi Kassim, Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Nusrat Hanje, pamoja na Mheshimiwa Waziri Dotto Biteko. Hususan kwenye suala zima la Mwanza *Refinery, GST, STAMICO,* na leseni za uchimbaji wa Magnet. Kamati inawashukuru sana na kweli suala la Mwanza *Refinery* ni lazima Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba kiwanda kile kisiweze kusimama au kisiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchangiaji wa maandishi Mheshimiwa *Engineer* Manyanya pia naye amezungumzia katika taarifa yake kwamba miundombinu ambayo inaweza kuirahisisha nchi yetu kufanya biashara na nchi jirani zetu kama Kongo, Serikali iboreshe miundombinu kuhakikisha kwamba sekta ya madini inakua na hasa ukizingatia nchi ya Congo ni *potential* katika eneo zima la rasilimali madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niliombe Bunge lako Tukufu lichukue mapendekezo ya Kamati kuwa mapendekezo ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja.

*(Hoja Imetolewa Iamuliwe)*

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji Kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati naMadini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii sasa kupongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili; Kamati ya UKIMWI na Kamati ya Nishati. Pia niwapongeze Wabunge kwa michango yenu mizuri, pamoja na majibu mazuri ambayo Serikali imetoa. Sasa hizi tena syio taarifa za Kamati, bali ni maagizo ya Bunge kwa Serikali kwa Kamati zote mbili. Tunategemea sasa Serikali kuzifanyia kazi na kuja majibu kuyarudisha Bungeni ili Bunge lijue kama maazimio yao yamefanyiwa kazi ipasavyo.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu sauala mafuta kuchelewa kushusha, kuna bandari Tanga ina *facilities* nzuri sana za kushusha mafuta. Shusheni Tanga kupunguza gharama na kupunguza ucheleweshaji wa mafuta ambayo yanasumbua wananchi kwa kutokupata huduma za mafuta. Kama Tanga kuna *facilities,* tumieni Tanga.

Mheshimiwa Ummy nafikiri unajua Tanga mna *facilities* nzuri sana pale. Kwa hiyo, mzingatie haya maoni na maagizo ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya, nawashukuru wote kwa ujumla. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.59 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 6 Februari, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*